BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KILIMO, BIASHARA NA UTALII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**FEBRUARI, 2022**

**RIPOTI YA KAMATI YA KILIMO, BIASHARA NA UTALII YA BARAZA LA WAWAKILISHI - KWA MWAKA 2021/2022**

**SEHEMU YA KWANZA**

**UTANGULIZI**

Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii ya Baraza la Wawakilishi imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha Kanuni cha 107 cha Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2020 na majukumu yake yametajwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni hizo kama ifuatavyo:-

(i) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliyotangulia.

(ii) Kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza.

(iii) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na miradi ya wananchi ya Wizara husika.

(iv) Kuchunguza na kufatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanya yalizingatia thamani halisi ya fedha.

(v) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.

(vi) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika

(vii) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.

(viii) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika

Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilianza shughuli zake za kufuatilia utekelezaji wa kazi za maendeleo ya Wizara zifuatazo:-

- Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo;
- Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda; na

- Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale

Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki kumi kwa Unguja Pemba na Dar es Salaam kwa mpango ufuatao:-

i) Unguja kwa wiki zote mbili kuanzia tarehe 18/01/2021 hadi tarehe 29/01/2021 kwa Wizara zote tatu.

ii) Tarehe 29/03/2021 hadi tarehe 03/04/20 kwa Pemba na tarehe 06/04/2021 hadi tarehe 10/04/2021 kwa Unguja, kwa Wizara zote tatu.

iii) Tarehe 09/08/2021 hadi tarehe 13/ 08/2021 kwa Pemba na tarehe 16/08/2021 hadi tarehe 20/08/2021 kwa Unguja.

iv) Tarehe 08/11 2021 hadi tarehe 12/11/2021 kwa Pemba na kuanzia tarehe 15/11/2021 hadi tarehe 19/11/2021 kwa Unguja.

v) Tarehe 17/01/2022 hadi 21/01/2022 kwa upande wa Pemba, tarehe 24/01/2022 hadi tarehe 26/01/2022 kwa Dar se Salaam na tarehe 27/01/2022 hadi tarehe 28/01/2022 kwa upande wa Unguja.

Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii wameshiriki kikamilifu katika kazi za Kamati kwa vipindi vyote hivyo, Wajumbe hao ni hawa wafuatao:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mheshimiwa Yussuf Hassan Iddi | Mwenyekiti |
| 2. | Mheshimiwa Aza Januari Joseph | Makamo Mwenyekit |
| 3. | Mheshimiwa Ali Abdulgulam Hussein | Mjumbe |
| 4. | Mheshimiwa Mwanajuma Kassim Makame | Mjumbe |
| 5. | Mheshimiwa Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| 6. | Mheshimiwa Saada Ramadhan Mwendwa | Mjumbe |
| 7. | Mheshimiwa Said Saleh Salim | Mjumbe |
| 8. | Ndugu Aziza Waziri Kheir | Katibu |
| 9. | Ndugu Mwaka Mwinyi Waziri | Katibu |

## SEHEMU YA PILI

### WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

Wiazara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inaundwa na Idara na taasisi mbali mbali ambazo kwa pamoja zina lenga kutoa huduma kwa wananchi wote bila ubaguzi wowote.

### IDARA ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

1. Idara ya uendeshaji na Utumishi
2. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
3. Idara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula
4. Idara ya Umwagiliaji Maji
5. Idara ya Misitu
6. Idara ya Maendeleo ya Mifugo
7. Afisi ya Afsa Mdhamini –Pemba

### TAASISI ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

1. Taasisi ya Utafiti wa Kilimo
2. Wakala wa Matrekta na Zana za Kilimo

Katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku Wizara ya Kilimo, Umwagilaji, Maliasili na Mifugo inajiendesha kupitia programu kuu tano ambazo ni:

1. Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo;
2. Programu Kuu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu;
3. Programu Kuu ya Maendeleo ya Mifugo; na
4. Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo.

**PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO**

Programu hii inajumuisha programu ndogo tano ambazo ni;

i) Programu ndogo ya Kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji maji,

ii) Programu ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo,

iii) Program ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo na uhakika wa chakula

iv) Programu ndogo ya uhakika wa chakula na lishe;

v) Programu ndogo ya huduma za Matrekta na zana nyengine za kilimo.

**ZIARA ZA KAMATI KUANGALIA MAENDELEO YA PROGRAMU ZA WIZARA**.

Kamati katika kazi zake ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali kwa lengo la kukagua miradi ya maendeleo na maeneo ya wakulima ili kuona mafanikio na juhudi zinazochukuliwa katika kuwasaidia wananchi ambapo ilifanya ziara maeneo yafuatayo:-

i) Ziara ya Kamati katika Wakala Serikali wa huduma za Matrekta na Zana za Kilimo;

ii) Vitalu vya Kilimo Weni na Chanjaani;

iii) Kituo cha Utafiti wa Kilimo Matangatuwani Pemba na Kizimbani Unguja;

iv) Kamati ilikutana na mabibi na mabwana shamba kwa Unguja na Pemba;

v) Kamati ilifanya ziara ya kukagua mradi wa ujenzi wa mabwawa katika bonde la Mlemele na Saninga kwa Pemba na Cheju na Kilombero kwa Unguja.

vi) Kamati ilifaya ziara ya kukagua ujenzi wa ghala jipya la kuhifadhia chakula kisiwani Pemba.

**PROGRAMU NDOGO YA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA NYENGINE ZA KILIMO**

Programu ndogo ya huduma za Matrekta na zana nyengine za Kilimo inatekelezwa na Idara ya Kilimo na ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, utoaji wa pembejeo na kutoa elimu ya uzalishaji na ushauri wa kitaalamu kwa wakulima.

**MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU HII**

Kamati ilipofanya ziara katika Wakala wa Serikali wa huduma za Matrekta na zana za kilimo kwa upande wa Unguja na Pemba na ilielezwa mafanikio yafuatayo ambayo yamepatikana tokea kuundwa kwa Wakala huu.

1. Kutungwa kwa Sheria ya kuanzishwa kwa Wakala.

2. Kupatikana kwa Muundo wa Taasisi ya Wakala.

3. Kupatikana kwa uongozi wa Wakala.

4. Matengenezo ya majengo pia ni miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana yenye lengo la kuandaa mazingira bora ya kazi kwa kuyafanyia ukarabati majengo ya ofisi zote ziliopo Mbweni kwa Unguja na Wawi kwa upande wa Pemba.

5. Wakala imefanikiwa kupata hati miliki ya eneo la ofisi ambapo awali eneo hilo lilikosa hati miliki.

6. Pia Kamati ilielezwa kuwa, Wakala kwa sasa wamefanikiwa kununua zana za kufanyia kazi yakiwemo matrekta mapya kwa Unguja na Pemba ambayo yanasaidia kutoa huduma kwa wananchi.

**CHANGAMOTO ZA WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO**

Kamati ilipofanya ziara yake katika Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na zana za Kilimo ilibaini changamoto zifuatazo:-

1. Ukosefu wa baadhi ya vifaa muhimu vya kutendea kazi. Kamati ilielezwa changamoto hii ambayo kwa kiasi kikubwa inapelekea usumbufu kwa wafanyakazi wa taasisi hii ambapo kazi zao nyingi ni za vitendo. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa, kuna baadhi ya vifaa ni vya muda mrefu sana tokea mwaka 1966 lakini vifaa hivyo baadhi yake bado ni vizima vinahitaji kufanyiwa '***service***' ya mara kwa mara ili viweze kutumika. Kwa upande wa Pemba Kamati ilielezwa uchakavu wa matrekta ambayo mengi ni ya muda mrefu ambayo hayamudu kazi ngumu na nzito kwa sasa.
2. Kamati ilielezwa changamoto ya Wakala kukosa fungu lake la bajeti ***'vote'*** jambo linalopelekea kuchelewa kufanyika kwa baadhi ya majukumu kwa wakati kutokana na uhalisia kuwa, kwa sasa kila kitu mpaka waombe kwa barua Wizarani.
3. Kamati ilielezwa changamoto ya ukosefu wa wataalamu wa kutosha ambapo kwa sasa baadhi ya wataalamu wenye ujuzi unaotumika ni wa zamani, baadhi yao wanakaribia kustaafu na pia ujuzi wao ni wa kizamani hauendani na teknolojia ya sasa kutokana na kukosa kwenda katika mafunzo ya mara kwa mara yatakayowasaidia katika kazi zao.
4. Kutokana na kutopata fedha kwa wakati zilizotengwa kwenye bajeti, Wakala inakabiliwa na changamoto ya kukosa vipuri na vilainishi vya matrekta, jambo linalopelekea baadhi ya matrekta kutofanyiwa '***service'***. Kamati pia ilielezwa kuwa suala la ukosefu wa vipuri vya kisasa linapelekea baadhi ya wakati wataalamu kuchukua vipuri vya matrekta ya zamani na kuviweka katika matrekta mapya ya kisasa jambo ambalo Kamati inaona haliko sawa kabisa kwa uhai wa matrekta hayo.

5. Kamati ilisikitishwa na taarifa ya baadhi ya wataalamu wa Wakala huu ambao walieleza kwamba hawalipwi stahiki zao kama ilivyoelezwa katika Sheria, ambapo Sheria imetoa muongozo wa uanzishwaji wa vitengo na divisheni mbali mbali katika Wakala, taarifa iliyotolewa mbele ya Kamati ilieleza kuwa, viongozi wa taasisi hii wamelifuatilia suala hili kwa kufuata taratibu zote za kisheria na hatimae kuwasilisha barua katika Wizara inayohusika ya Utumishi wa Umma, pamoja na kupewa agizo la Serikali kuu la kuwataka wahusika wote wanaostahiki kulipwa haki zao, kwa masikitiko makubwa Kamati imepewa taarifa kuwa, kuna baadhi ya viongozi kutoka Wizara ya Utumishi wa Umma waliweka kikwazo kutokana na mawazo yao kwamba hajaridhika na hawaoni sababu ya watu hao kulipwa. Aidha kwa upande wa Pemba Kamati ilielezwa changamoto ya kuchelewa kwa malipo ya muda wa ziada ***'overtime'*** na posho za likizo kwa wafanyakazi waliopo huko.
6. Wakala inakabiliana na kikwazo kitokanacho na wakulima kutochangia kwa wakati kiwango kidogo cha fedha kilichowekwa na Serikali kwa lengo la kuchimbia na kuburugia mashamba yao.
7. Kamati imebaini kuwa wafanyakazi wa Wakala wanafanyakazi katika mazingira magumu na hatarishi.
8. Kamati pia imebaini kwamba, vifaa vilivyomo ndani ya karakana havipo salama kutokana na mzingira ambayo si rafiki kuwekwa vifaa hivyo.
9. Kamati ilipofanya ziara kisiwani Pemba ilielezwa changamoto ya uhaba mkubwa wa wafanyakazi ambapo ilielezwa kuwa, mfanyakazi mmoja anapangiwa kazi zaidi ya moja jambo linalozorotesha utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Aidha kamati iliarifiwa kuwa katika ofisi hii kuna mlinzi mmoja tu jambo linalopelekea madereva wa matrekta baadhi ya wakati kufanya kazi ya ulinzi jambo ambalo si sahihi kwa mujibu wa Sheria za kiutumishi.

10. Kamati ilibaini changamoto ya ufinyu wa ofisi ya Wakala kwa Pemba jambo linalopelekea usumbufu mkubwa katika utekelezaji wa majukumu na usiri wa mambo ya kiofisi. Kwa mujibu wa maelezo yaliyopokelewa mbele ya Kamati ni kwamba, shughuli nyingi za kiofisi hasa za utunzaji wa fedha zinafanywa na Wizara..
11. Kamati pia ilielezwa changamoto ya upungufu wa madereva wa matrekta ambapo kwa sasa Serikali imesitisha suala la uajiri wa wafanyakazi na badala yake imeagiza kuchukua wafanyakazi kutoka taasisi nyengine kama mbadala. Hata hivyo kwa taasisi hii hasa madereva wa matrekta jambo hili ilimeshindikana kutokana na ukweli kwamba madereva wa gari za kawaida hawawezi kuendesha matrekta hasa ya kilimo kutokana na utaalamu maalum wanaofundishwa madereva wa matrekta ya kilimo.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na zana za Kilimo kuvihifadhi na kuvitunza vifaa vyote vilivyomo katika taasisi hii kwa kuweka mazingira mazuri hasa ukizingatia kwamba, vifaa hivi ni ghali na adimu kupatikana.  Aidha, Kamati inashauri kufanyiwa ***'service'*** vifaa vyote kwa wakati kutokana na vifaa hivyo kununuliwa kwa gharama kubwa ili kuepusha kuingia hasara mara mbili. Kamati inashauri kwa vile vifaa vya matrekta ya muda mrefu vinavyofaa vitolewe na visivyofaa viondolewe kwenye orodha ya daftari la mali za ofisi ili kuondoa mrundikano wa vifaa visivyohitajika. Tunasisitiza kurekebishwa kwa matrekta yanayofaa ksiwani Pemba ili yaweze kutumika katika shughuli za kilimo.
2. Kamati inaishauri Wakala kuweka utaratibu wa kuwapeleka wataalamu wake katika mafunzo ya mara kwa mara ili wataalamu hao waendane na mabadiliko ya teknolojia ambayo inakua kwa kasi mno. Utaratibu huu utasaidia sana kuziba pengo la kukosekana kwa madereva wa matrekta

pamoja na kuziba pengo linalotarajiwa kuongezeka katika taasisi hii kwa vile wataalamu wengi wanakaribia kustaafu. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuingiza fedha kwa wakati katika taasisi hii, kwa lengo la kuiwezesha Wakala kutekeleza majukumu yake kama ilivyojipangia katika bajeti. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Fedha tunaishauri kuangalia uwezekana wa kuipatia Wakala hii fungu lake la bajeti ***'vote'*** kutokana na unyeti wa shughuli zinazotekelezwa ambazo nyingi zinahitaji fedha za haraka.

3. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuwalipa stahiki zao wafanyakazi wote wa Wakala kwa mujibu wa Sheria, hasa tukizingatia kwamba wafanyakazi hawa wanafanyakazi katika mazingira magumu na hatarishi. Kamati inaiagiza Wizara kulifuatilia tena suala la Muundo wa Wakala pamoja na stahiki zake zote zilizopitishwa na ihakikishe kuwa wafanyakazi wote wanaostahili kulipwa haki zao wanalipwa kama Sheria ilivyoelekeza.
4. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuweka utaratibu maalum wa kuwapima afya wafanyakazi wote waliopo katika Wakala wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo, angalau kila baada ya miezi sita kutokana na ugumu wa mazingira ya kazi wanazozifanya, kwa lengo la kupata uwelewa juu ya afya zao na kuweza kuchukua tahadhari pale inapobainika udhaifu katika miili yao. Pia Kamati inaendelea kuwasisitiza watalaamau wa zamani kushirikiana na vijana wanaoajiriwa na Wakala kwa kuwapa ujuzi wao wa kizamani ambao ni wa thamani kubwa na bado unahitajika katika taasisi hiyo nyeti katika maendeleo ya taifa letu.
5. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuliangalia upya suala la wakulima kutochangia kwa wakati fedha za kuburugia mashamba yao jambo ambalo limekua likikwamisha shughuli za kilimo kwa baadhi ya maeneo. Kupitia ripoti hii, Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe washirikiane

na Wakala wa Huduma za mtrekta kuwahamasisha wananchi kutoa fedha hizo kwa wakati ili mashamba ya wakulima yaweze kutayarishwa kwa wakati na kilimo husika kifanyike kwa muda muwafaka. Kamati inaunga mkono wazo la Wakala la kuwaomba wananchi kuchangia kwa awamu ili watoe nafasi kwa Wakala kufanya kazi za kuwatayarishia mashamba yao kwa ufanisi mkubwa, endapo tu wananchi hao watafuata utaratibu maalum uliowekwa na taasisi hii, hasa tukizingatia kuwa Wakala ina uhaba mkubwa wa matrekta. Ilielezwa kuwa wananchi wanapofanya malipo wote kwa pamoja inakua ni vigumu sana kwa Wakala kuzikamilisha kazi hizo kwa wakati.

6. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wakala kuzitangaza huduma zake zaidi kwa taasisi mbali mbali za Serikali na hata kwa watu binafsi, ili waweze kuongeza kipato ambacho kitasaidia kutatua changamoto ndogo ndogo kwa zile fedha zitakazoingia.
7. Kamati inaishauri Wakala kuweka mkakati maalum wa kujenga ofisi za kudumu kwa Unguja na Pemba ili watumishi wa taasisi hii waweze kua na ari pamoja na kupata sehemu nzuri ya kufanyia kazi ambayo itawafanya wajisikie vizuri wawapo kazini.

**VITALU VYA KILIMO VYA SERIKALI VILIVYOPO CHANJAANI NA WENI**

Kamati ilibahatika kufanya ziara katika vitalu vya Serikali vinavyootesha miche ya aina mbali mbali ikiwemo mikarafuu, minazi na miti ya matunda vilivyopo Chanjaani na Weni kisiwani Pemba. Katika ziara zake hizi, Kamati ilibaini changamoto kadhaa ambazo kwa kiasi fulani zinakwamisha utekelezaji wa majukumu kwa watendaji na kuzorotesha uzalishaji wa miche hii.

**CHANGAMOTO ZINAZOKABILI VITALU VYA SERIKALI VILIOPO CHANJANI NA WENI**

1. Upatikanaji wa fedha kwa wakati ni tatizo kubwa linaloikabili Idara ya Kilimo Pemba, hali inayowakwaza watendaji wa Idara hii na kupelekea kushindwa kununua mahitaji muhimu kwa lengo la kuotesha miche,

mahitaji hayo ni pamoja na vifuko vya kuoteshea miche, mabero, mapanga, mindu na vifaa vyengine muhimu vinavyotumika katika uatikaji wa miche.

2. Kamati pia ilielezwa changamoto ya uhaba wa wafanyakazi ambapo takwimu halisi ya wafanyakazi katika kituo cha Chanjaani ni wafanyakazi 8 tu na kituo cha Weni kina jumla ya wafanyakazi 14 tu, jambo linalokwamisha utekelezaji wa majukumu ya kila siku na hatimae kurudisha nyuma malengo ya vituo hivi na kushindwa kufikia malengo yaliyopangwa na Serikali.
3. Kamati ilibaini kuwa kuna uzalishaji mdogo wa miche ya mikarafuu hali inayopelekea wakulima kukosa miche kwa mujibu wa mahitaji yao. Kwa mfano katika kitalu cha Chajaani, lengo lilikuwa ni kuzalisha miche 60,000 lakini hadi Kamati ilipotembelea kitalu hiki ilipewa taarifa kuwa miche iliyooteshwa ni miche 34,000 tu. Kwa upande wa kitalu cha Weni lengo lilikuwa ni kuzalisha miche 75,000 lakini hadi Kamati inafika katika eneo hilo ilibaini kuwa ni 38% tu ya miche ndiyo iliyooteshwa. Hali hii hairidhishi jambo linalopelekea wakulima kuishushia lawama Serikali jambo ambalo halifurahishi hata kidogo.
4. Changamoto ya ukosefu wa vitendea kazi inaonekana kuwa ni kikwazo kikubwa kinachokwamisha utekelezaji wa kazi za uoteshaji wa miche katika vitalu hivi. Mfano katika Kitalu cha Chanjaani na Weni wafanyakazi wanakabiliwa na upungufu mkubwa wa vitendea kazi ikwemo matangi ya kuhifadhia maji, keni, mabero, reki, mapanga na hata misaha. Maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati kuhusiana na vifaa vya kufanyia kazi si ya kuridhisha. Ilielezwa kuwa, kati ya kifaa kimoja hadi vitano kati ya vifaa tulivyovitaja ndivyo vilivyopo katika vituo hivi. Hali hii inawapa wakati mgumu wafanyakazi hawa katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.
5. Kamati ilielezwa kuwa tatizo la kukosekana kwa wataalamu wa masuala ya uatikaji wa miche ni kikwazo kikubwa kinachokwamisha shughuli nzima ya uoteshaji na ushughulikiaji wa miche ya mikarafuu. Katika Kitalu cha Chanjaani, Kamati ilibaini uwepo wa mtaalamu mmoja tu ambaye inaonekana wazi kwamba hayupo kituoni hapo kwa muda wote. Kwa mujibu wa maelezo iliyopokea Kamati, mtaalamu huyu hupita kituoni hapa wiki mara moja. Kamati inaliona suala hili haliko sawa.
6. Kama tunavyofahamu likizo ni haki ya kila mfanyakazi na pale mfanyakazi huyu anapokwenda likizo anapswa kupatiwa stahiki zake zote kwa lengo

la kujikimu kwa yale anayoyaendea katika likizo yake. Jambo la kusikitisha ni maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati kuwa, kuna baadhi ya wafanyakazi hawapatiwi fursa ya kwenda likizo wala hawapatiwi stahiki hii kama Sheria ya Utumishi wa Umma inavyoelekeza. Kamati ilishangazwa sana kusikia kuwa mtumishi wa umma anakaa kazini zaidi ya miaka ishirini na saba bila ya kupatiwa haki hii ya msingi.

7. Maji ni uhai kwa viumbe vyote ulimwenguni, Kamati imebaini changamoto ya ukosefu wa maji katika vitalu vyetu vya kuoteshea miche ya mikarafuu. Katika kitalu cha Weni maji imekuwa ni tatizo kubwa na ilielezwa kuwa maji yanayopatikana katika eneo hilo ni maji yaliyochanganyika na chumvi ambayo si rafiki kwa uoteshaji wa miche.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Serikali kuiingizia Wizara ya Kilimo fedha kwa mujibu wa bajeti iliyopangwa na kwa wakati ili iweze kutekeleza malengo waliyojipangia, ikiwemo ununuzi wa vifaa vya kutendea kazi kama mabero, keni, mapanga, mindu, misaha na vifaa vyenginevyo muhimu vya kilimo vinavyohitajika.
2. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ishirikiane na Mamlaka ya Maji (ZAWA) kwa lengo la kupeleka maji katika vitalu vya kuoteshea miche ikiwemo ya mikarafuu hasa ukizingatia miche hii inahitaji kiasi kikubwa cha maji katika ukuaji wake.
3. Kamati inaiomba Wizara ya Kilimo kushirikisha vitalu vya watu binafsi kwa lengo la kubadilishana uzoefu juu ya mbinu bora za uoteshaji wa miche hii.
4. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuwa wabunifu katika kuanzisha miradi itakayosaidia uoteshaji wa miche iliyo bora.
5. Kamati inaishauri Idara ya Kilimo ijipange kuwalipa watumishi stahiki zao na iache tabia ya kuitegemea Wizara pekee hasa tukizingatia Idara inaingiziwa OC yake na bajeti yake.
6. Kamati inawapongeza wafanyakazi wote katika vitalu vya Chanjaani na Weni kwa juhudi zao kubwa za uoteshaji wa miche ya Mikarafuu na matunda mbalimbali na kuwataka kuongeza juhudi zaidi za uzalishaji hasa tukizingatia kuwa hii ni rasilimali muhimu katika kuwawekea mustakabali mwema wakulima wetu.

7. Kamati inaishauri Wizara kuchukuwa juhudi za makusudi kuhakikisha kuwa inatafuta wataalamu wa kutosha na huyo mtaalamu mmoja aliyepo kwa sasa Wizara ihakikishe kuwa mtaalamu huyu anapatikana kituoni hapo muda wote kwa lengo la kuweza kutatua matatizo yote yanayowakabili wafanyakazi wa eneo hilo.

## TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO (ZARI)

Taasisi hii inafanya kazi sawa kwa vituo vyake vyote vya Unguja na Pemba ambapo kwa upande wa kisiwa cha Pemba, Taasisi ina jumla ya vituo vitano ambavyo ni Matangatuwani, Wesha, Tumbe, Fundo na Weni. Kwa upande wa Unguja Taasisi hii ina jumla ya vituo vinane (8), ikiwa ni pamoja na Kijichi, Selemu, Bambi, Mwera na vyenginevyo.

Kamati katika ziara zake za kikazi, ilifanya ziara katika baadhi ya vituo vya Unguja na Pemba na kuelezwa mafanikio kadhaa yaliyopatikana tokea kuanzishwa kwa taasisi hii.

## MAFANIKIO YA TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana tokea kuundwa kwa taasisi hii ni kama ifutavyo:-

1. Kamati ilielezwa kuwa taasisi imefanikiwa kuyaendeleza baadhi ya mashamba ya viungo likiwemo shamba la viungo Kizimbani, ambapo shamba hilo limekua kwa kiasi kikubwa likiisaidia Serikali kuongeza mapato kupitia ujio wa watalii ambao huingia kwa wingi shambani na kupelekea kuongezeka kwa pato la taifa.

2. Taasisi imefanikiwa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watendaji wake. Mafunzo hayo yalihusisha watafiti sita, '***supporting staff'*** wawili na wawezeshaji wawili.

3. Pia taasisi imefanikiwa kuboresha miundombinu katika baadhi ya vituo vya uzalishaji miche ya mazao na matunda kama kituo cha uzalishaji miche cha Wesha.

## CHANGAMOTO ZA KITUO CHA UTAFITI WA KILIMO – MATANGATUWANI NA KIZIMBANI

Kamati ilipofanya ziara katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo kwa Pemba na Unguja ilielezwa changamoto kadhaa ambazo zinakwamisha utekelezaji wa malengo yaliyopangwa kufanyika katika taasisi hii kama ifuatavyo:-

1. Taasisi ya Utafiti wa kilimo iliielezea Kamati kuwa inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa fedha za kutosha za kufanyia tafiti mbali mbali za kilimo ambazo zitasaidia kuongeza ufanisi na kuwawezesha wakulima kulima kwa utaalamu wa kisasa. Ukosefu huo wa fedha umesababisha kituo hiki kwa upande wa Pemba kutofanya tafiti kwa miaka mitatu sasa, hali inayopelekea kutotekelezwa kwa majukumu ya taasisi hii kwa wakati kama yalivyopangwa. Sambamba na hilo, Taasisi pia inakabiliwa na changamoto ya kukosa gawio la fedha za maendeleo toka Serikalini. Tatizo hili lipo kwa kiasi kikubwa katika kituo cha Matangatuani Pemba. Ilielezwa kuwa tangu bajeti ya mwaka 2015/2016 hadi leo Kituo hiki hakijapatiwa mgao wa fedha za maendeleo hali inayopelekea ugumu wa kufanya tafiti.

2. Kamati pia ilibaini changamoto ya ukosefu wa wataalamu wa kutosha na vifaa vya maabara katika vituo vyote. Kamati ilielezwa kuwa maabara zilizopo ndani ya vituo hivi hazina wataalamu na vifaa vya kutosha, ambapo kwa upande wa Matangatuani Pemba hakuna mtaalamu hata mmoja jambo linalorudisha nyuma kasi ya maendeleo na kuzorotesha malengo ya kituo hiki.

3. Changamoto ya kukosekana kwa usafiri kwa wafanyakazi katika taasisi hizi ni tatizo linalozorotesha utendaji wa majukumu kwa wafanyakazi wa taasisi hizi.

4. Kamati ilielezwa kuwa katika kituo cha Kizimbani kuna wimbi la wafanyakazi wasiokuwa na uwezo wa kiutendaji, kutokana na uduni wa taaluma walizo nazo hali inayorudisha nyuma kasi ya maendeleo.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inavipongeza vituo vya Kilimo Matangatuwani Pemba na Kizimbani kwa Unguja, kwa kazi nzuri na ngumu wanazozifanya pamoja na changamoto nyingi wanazokabiliana nazo. Hata hivyo, Kamati

inaishauri Serikali kuingiza fedha za bajeti kwa wakati na kama zilivyopitishwa katika bajeti. Aidha Kamati imesikitishwa sana na taarifa ya kukosena kwa fedha za maendeleo hasa kwa kituo cha Matangatuani, ni jambo la kusikitisha sana kuona kuwa fedha hizo zimesekosekana tokea bajeti ya mwaka 2015/2016. Jambo hili halikubaliki na Kamati inaomba kupatiwa maelezo ya kina kuhusiana na suala hili.

2. Kamati inaishauri Serikali kuviangalia vituo hivi kwa upande wa wataalamu na vifaa vya maabara kutokana na umuhimu wake. Tunaiomba Serikali mara tu itakapoanza kuajiri wafanyakazi, iharakishe kuajiri wataalamu watakaojaza mapengo yaliopo katika vituo hivi kwa lengo la kutimiza malengo ya kuanzishwa kwa vituo hivi.

3. Kamati inaiomba Wizara kuwafanyia mpango wafanyakazi wa taasisi hii angalau kuwapatia posho la usafiri ili kusudi waweze kujikimu na kufika katika maeneo yao ya kazi kwa wakati.

4. Kamati inaishauri Wizara kupitia vituo hivi kuwa na mpango maalum wa kuwaendeleza wafanyakazi wake wenye viwango vya chini vya elimu ili waweze kuwatumia ipasavyo ndani ya vituo vilivyomo ndani ya Taasisi hizi.

5. Kamati inaishauri Taasisi ya kilimo kujenga mashirikiano ya karibu sana na Taasisi nyengine kama hizi za ndani na nje ya nchi, kwa lengo la kubadilishana uzoefu na mbinu za kiutendaji. Aidha tunavishauri vituo vyote vya taasisi hii, kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kuvitunza vituo hivi kwa maendeleo ya taifa na kuhakikisha kuwa matokeo ya tafiti zinazofanywa na vituo hivi yanawafikia wakulima kwa lengo la kuwawezesha kulima kilimo chenye tija.

6. Kamati inaipongeza taasisi ya Kilimo kwa kuweza kupata matokeo mazuri ya utafiti wa mbegu za mpunga zinazostahamili maradhi ya manjano ***'Rice Yellow Mottle Virus'*** na ukungu ***'Rice Blast'*** kwa kutumia teknologia ya mionzi (Nuclear Radiation) na kufanikiwa kupata tuzo ya Kimataifa ya mwanasayansi bora katika uzalishaji wa mbegu za mpunga. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati ndugu Salum Faki Hamad alitunukiwa tuzo hii kutoka Shirika la Kimataaifa la Nguvu za Atomiki ***'International Atomic EnergyAgency'*** yenye Makao yake makuu Vienna Austria mnamo mwezi Septemba mwaka 2021. Kamati inachukuwa nafasi

hii kumpongeza kwa dhdti mwanasayansi wetu huyu kwa kupata tuzo hii muhimu kwa maendeleo ya taifa letu.

Baada ya kueleza kwa kina mafanikio na changamoto za Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, sasa naomba tutoe maelezo kuhusiana na baadhi ya maeneo yaliyoimarishwa na taasisi hii ambayo Kamati iliyatembelea kwa lengo la kuona utekelezaji wa malengo yaliyopangwa.

Baadhi ya maeneo yaliyotembelewa na Kamati ni pamoja na:-

i) Shamba la Makuwe;

ii) Shamba la Viungo Kizimbani;

**SHAMBA LA MAKUWE NA SHAMBA LA VIUNGO KIZIMBANI**

Shamba la Makuwe ni shamba la Serikali liliopo chini ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ambalo kwa sasa linasimamiwa na Idara ya Kilimo. Shamba hili liko Mkoa wa kaskazini Pemba ambalo limeingia katika Wilaya ya Wete na Micheweni.

Pia shamba la Viungo liliopo Kizimbani ni shamba linalosimamiwa na Taasisi ya Kilimo ambalo kama tulivyoeleza huko juu shmba hili limekua ni kivutio kikubwa cha watalii ambalo linaiingizia Serikali fedha nyingi kwa maendeleo ya Taifa letu.

Baada ya ziara ya Kamati, changamoto zifuatazo zilibainika na kuelezwa ambazo kwa namna moja ama nyengine zinakwamisha maendeleo ya mashamba hayo.

**CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA**

1. Kamati ilielezwa kuwa shamba la Makuwe linakabiliwa na uhaba mkubwa wa wafanyakazi. Kamati ilielezwa kuwa kuna wafanyakazi saba tu hali inayopelekea kuchelewa kutekelezwa kwa majukumu ya kila siku. Shamba ni kubwa sana ambapo lina ukubwa wa hekta 79.9 sawa na eka199.75. Kutokana na ukubwa wa eneo hilo ni wazi kuwa wafanyakazi saba waliopo sasa hawatoshelezi kufanyakazi za usafi na nyenginezo peke yao.

2. Kamati katika ziara yake katika mashamba yote ilibaini changamoto ya uhaba mkubwa wa fedha za kuendeshea mashamba hayo ambapo

milioni mia nne zinahitajika kwa upande wa shamba la Makuwe pekee ili ziweze kutumika kuliimarisha eneo lote la shamba hilo.

3. Katika ziara ndani ya shamba la Makuwe, Kamati ilisikitishwa na kushitushwa na taarifa ya ukodishwaji wa shamba hilo ambalo ilielezwa kuwa kwa msimu wa karafuu uliopita. Kamati ilielezwa kuwa msimu huo shamba la makuwe lilikodishwa kwa shilingi milioni tano tu jambo ambalo liliishangaza na kuishitua sana Kamati. Kamati inatoa msisitizo wa mshituko huo kutokana na taarifa kuwa shamba hilo hapo awali liliwahi kukodishwa hadi shilingi milioni mia tatu jambo ambalo ni la kushangaza na kusikitisha kusikia kuwa msimu uliopita shamba hili lilikodishwa kwa feha hizo.

4. Katika mashamba yote mawili kuna changamoto ya kukosekana kwa uzio wa kuyalinda maeneo ya mashamba hayo. Changamoto hii inasababishwa na kukosekana kwa fedha za kutosha ambazo zingesaidia kuweka uzio wa uhakika na hatimae kuyalinda maeneo hayo. Kukosekana kwa uzio kunasababisha baadhi ya wananchi kuvamia baadhi ya maeneo na kuharibu mazao na maeneo mengine muhimu ya mashamba hayo.

5. Kamati katika shamba la Makuwe ilielezwa kuwa kuna changamoto ya kukosekana kwa hati miliki ambapo ni miaka miwili sasa tangu Wizara iwasilishe maombi ya hati Miliki ya eneo hilo lakini hadi Kamati inafika katika eneo hilo bado haijapatikana.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Serikali kuliangalia upya suala zima la ajira za watumishi wapya kutokana na baadhi ya taasisi za Serikali zikiwemo baadhi ya taasisi za Wizara ya Kilimo kukosa wafanyakazi wa kutosha jambo linalopelekea mzigo mkubwa kuwaelemea wafanyakazi wachache waliopo katika taasisi hizo. Pamoja na maamuzi ya Serikali ya kusitisha ajira, Kamati inaiomba Serikali endapo itaamua kufanya uhamisho wa baadhi ya wafanyakazi na kuwapeleka katika taasisi nyengine basi miongoni mwa taasisi zitakazopelekewa wafanyakazi na taasisi za Wizara ya Kilimo ziingie.

2. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kufanya mazungumzo ya haraka na Wizara ya Fedha na Mipango

ili 30% ya fedha zilizoombwa kwa lengo la kuliimarisha shamba la Makuwe ziweze kupatikana na maendeleo ya shamba hilo yaweze kuonekana na kulinufaisha taifa kwa ujumla.

3. Kamati baada ya kufanya ziara katika shamba la Makuwe iliona taarifa ya Serikali ambayo ilitoa muongozo wa kusitisha ukodishwaji wa mashamba yote ya Serikali. Kupitia taarifa hii ya Kamati tunaipongeza sana Serikali kwa uamuzi na hatua yake hiyo ya haraka ambayo imelenga kuokoa rasilimali za taifa letu.

4. Kamati ilipofanya ziara katika shamba la Makuwe ilielezwa kuwa ukodishwaji wa shamba hili hauridhishi. Pamoja na maamuzi ya Serikali ya kuyaweka mashamba hayo katika usimamizi wake, Kamati inashauri shamba hilo na mashamba mengine ya Serikali ambayo hayajakodishwa yakabidhiwe kwa Shirika la Biashara la Taifa (SZTC) ili yaweze kutumika kikamilifu katika uzalishaji wa karafuu na endapo kama itafaa hata mazao mengine ya biashara. Kamati inatoa ushauri huu kutokana na maelezo iliyoyapata ilipofanya ziara katika Shirika la Biashara kuwa huko nyuma Shirika liliwahi kuomba kupatiwa shamba la Makuwe lakini jambo hilo lilishindikana kutokana na sababu mbali mbali.

5. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kufanya utaratibu wa haraka ambao utayawezesha mashamba yote mawili kupata fedha za kuweka uzio wa uhakika katika maeneo yake ili maeneo hayo yasalimike na uvamizi wa baadhi ya wananchi.

6. Maelezo ya kukosekana kwa hati miliki ya shamba la Makuwe yaliisikitisha sana Kamati hasa ikizingatiwa kuwa taasisi zote ni za Serikali ambazo zinafanya kazi kwa pamoja, hivyo Kamati kupitia taarifa hii inaiomba taasisi husika inayotoa hati miliki kutoa kipaumbele kwa taasisi zote za Serikali katika suala zima la hati miliki ili kuepusha migogoro na wananchi inayoweza kuepukika .

7. Kamati inaishauri serikali kuongeza upandaji wa miche ya Mikarafuu katika vitalu vyake, kwa lengo la kuongeza tija katika uzalishaji.

**PROGRAMU NDOGO YA KUENDELEZA MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI MAJI**

Programu hii imetekelezwa kwa kuzingatia shabaha zake ikiwemo ujenzi wa misingi mikubwa na midogo ya kumwagilia maji yenye urefu wa jumla ya mita

5,170, utengenezaji wa matuta kwa ajili ya ujenzi wa mitaro ya umwagiliaji maji katika bonde la Kibokwa, Chaani, Kinyasini, Cheju, na Kilombero.

***Ziara ya kukagua mradi wa ujenzi wa mabwawa katika bonde la Mlemele na miradi ya umwagiliaji katika bonde la Saninga kwa Pemba na bonde la Cheju na Kilombero kwa Unguja.***

**MRADI WA UJENZI WA MABWAWA KATIKA BONDE LA MLEMELE**

Ujenzi wa Mradi wa mabwawa ya Umwagiliaji Maji katika bonde la Mlemele ni miongoni mwa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo. Utekelelezaji wa Mradi huu ulianza mwezi April, 2019 na unatarajiwa kumalizika mwezi Aprili, 2022 kupitia mkopo kutoka Benki ya (EXIM Bank) ya Korea na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**CHANGAMOTO ZA MRADI**

Katika utekelezaji wa mradi huu, kuna changamoto kadhaa zinazokwamisha kwa namna moja ama nyengine maendeleo ya mradi huu kama ifuatavyo:-

1. Kamati ilielezwa kuwa utekelezaji wa mradi huu ulichelewa kuanza kutokana na kutokuwepo kwa zana nzito pamoja na Mshauri Elekezi kutokuwa na wataalamu wa kutosha wa kusimamia kazi hiyo. Aidha, Kamati ilipofanya ziara katika mradi huu haikumkuta mshauri elekezi katika eneo lake la kazi jambo ambalo Kamati inaona ni changamoto hasa ukihitajika ushauri wa kitaalamu wa haraka haraka na yeye akiwa hayupo kazini.

2. Changamoto nyengine ambayo Kamati ililezwa ni Ujenzi wa misingi yote midogo ya ndani ***'tertiary canals'*** ambapo ilielezwa kuwa misingi hiyo ilipangwa kujengwa kwa kiwango cha udongo kutokana na bajeti ndogo ya utekelezaji wa mradi. Hali hiyo itapelekea kukosekana kwa ufanisi, kupotea kwa maji na gharama kubwa za uendeshaji na matengenezo ya mara kwa mara misingi hiyo.

3. Kamati pia ilielezwa changamoto ya kutokuwepo kwa bajeti ya usimamizi na ufuatiliaji katika gharama za utekelezaji wa mradi huu, jambo linalorudisha nyuma ari ya wasimamizi kwa upande wa Wizara kutokana na kutolipwa stahiki zao kwa wakati. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa Wizara imeingiza kifungu cha malipo baada ya saa za kazi kwa

wasimamizi hao na imeahidi kuwalipa wasimamizi stahiki zao kadri fedha za ***OC*** zitakavyopatikana.

4. Changamoto nyengine iliyoelezwa ni kwa wakulima walioathirika na ukataji wa vipando vyao katika eneo litakalojengwa misingi ya kumwagilia na ujenzi wa ploti. Ilielezwa kuwa baadhi ya wakulima katika eneo hilo bado hawajalipwa fidia za mazao na vipando vyao jambo ambalo ni changamoto kubwa kutokana na ukweli kwamba ili ujenzi huo uendelee ushirikiano na wananchi wa eneo hilo unahitajika. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa mchanganuo wa gharama za fidia hizo bado upo kwa Mthamini Mkuu wa Serikali.

**BONDE LA UMWAGILIAJI MAJI LA SANINGA**

Kamati pia ilifanya ziara katika bonde la Saninga ili kujiridhisha kwa upande wa utekelezaji wa Bajeti kama ilivyopitishwa na Baraza la Wawakilishi.

**MAFANIKIO YA MRADI KATIKA BONDE LA SANINGA**

Katika utekelezaji wa mradi huu, mafanikio yafuatayo yalielezwa:-

1. Mradi umefanikiwa kutoa mafunzo kwa wakulima juu ya mbinu bora za kilimo, takribani wakulima 120 walipatiwa mafunzo hayo.

2. Kuanzishwa kwa vishamba vya maonesho (shamba darasa) kwa wakulima.

3. Wakulima walipata fursa ya kutembelea vituo mbalimbali vya wakulima kama vile Tanzania Bara na hapahapa kwetu visiwani kwa lengo la kuchota uzoefu kwa wakulima wenzao.

**CHANGAMOTO ZA MRADI KATIKA BONDE LA SANINGA**

Kamati ilipofika katika bonde hilo ilibaini changamoto zifutazo ambazo nyengine zilielezwa na wakulima wanaotumia eneo hilo.

1. Baadhi ya wakulima kutoshuka katika maeneo ya kazi ambapo maeneo hayo yanakua tayari yamefanyiwa kazi ya kuhuishwa na Wizara jambo ambalo linaitia hasara kubwa Serikali na baadhi ya wakati maafisa wa Wizara hulazimika kutafuta wakulima kutoka maeneo ya mbali kwa lengo la kuwataka kuyafanyia kazi maeneo hayo.

2. Baadhi ya miundombinu iliyopo katika bonde hilo haiko vizuri hasa mitaro, ambapo katika kipindi cha mvua baadhi ya mitaro hujaa maji na kuathiri mazao ya wakulima wa eneo hilo na kupelekea baadhi ya wakulima kuacha kilimo na kujikita katika zao la mwani.

3. Kamati pia ilibaini changamoto ya kutosafishwa kwa mitaro ya kusukumia maji jambo linalopelekea baadhi ya mitaro hiyo kuharibika kutokana na kujaa taka na kupelekea mitaro mengine kupasuka kutokana na mitaro hiyo kutojengwa kwa saruji.

4. Kamati imesikitishwa sana na taarifa iliyotolewa na Idara ya Umwagiliaji kisiwani Pemba kuwa, tokea bajeti ya mwaka huu kuanza Idara hiyo imeingiziwa shilingi milioni 2 na nusu tu kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali ikiwemo uendelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo tayari fedha zake zimeshatengwa.

5. Kamati pia ilielezwa changamoto ya ukosefu wa mabibi na mabwana shamba ambao kwa kiasi kikubwa wanahitajika katika kuwapa muongozo wakulima jinsi ya mbinu bora za kilimo cha kisasa. Ilielezwa kuwa hadi wakati Kamati inafanya ziara **(8/11/2021)** katika eneo hilo, Pemba nzima ina mabibi na mabwana shamba **21** tu wakati wanaohitajika ni **129**.

6. Changamoto nyengine ambayo ilielezwa mbele ya Kamati ni matumizi madogo ya pembejeo za kilimo hasa mbolea na mbegu bora ambazo zinachangia kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa mpunga kuwa mdogo katika bonde hili hali inayoshusha mori ya kufanyakazi kwa wakulima wetu hawa.

7. Kamati pia ilibaini changamoto inayohusisha ukubwa wa eneo linalozunguka bonde hili la Saninga. Ukubwa wa eneo linalotumika kwa kilimo hiki hailingani na idadi ya wakulima waliopo kwa sasa. Bonde ni dogo lenye ekeri **16** ambapo wakulima wanaojishughulisha na kilimo cha mpunga katika bonde hili wanakadiriwa kufikia **160,** hali hii inawaweka wakulima hawa katika mazingira ya kuzalisha mpunga katika kiwango kidogo mno ambapo kwa hali halisi ilivyo Kamati inaona ni vigumu kuweza kujitegemea na kujitosheleza kwa chakula kama Serikali yetu na Wizara ya Kilimo ilivyojipangia.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha kwa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa wakati, kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya Umwagiliaji katika bonde hili ili kuongeza kasi ya uzalishaji wa zao la mpunga kwa vile wakulima wote wanaolima katika bonde hili wanalima kwa ajili ya kuwatosheleza wao wenyewe kwa chakula.

2. Kamati inaishari Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kuandaa utaratibu wa kuwapatia pembejeo za kilimo wakulima wetu kama vile mbolea, angalau kwa kuwakopesha kwani hali za wakulima wetu walio wengi ni duni wanashindwa kununua pembejeo hizi na hatimae kushuka kwa kiwango cha uzalishaji.

3. Kamati inaishauri Wizara kuwa karibu sana na wakulima hawa ili kutoa nguvu za pamoja za kukiimarisha kilimo cha mpunga nchini.

4. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kuchukua juhudi za makusudi kuhakikisha kuwa wakulima hawa wanawapatia pembejeo za kutosha kwa lengo la kuleta tija katika kilimo chao.

5. Kamati inaishauri wizara kufanya kazi ya ziada kuhakikisha wakulima wa bonde hili wanapata maji ya kutosha ya kumwagilia katika mazao yao. Hili likiwezekana kutaboresha uzalishaji wa mpunga na kuweza kujitegemea kwa chakula.

6. Kamati inaishauri serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuwaajiri mabibi na mabwana shamba wa kutosha na kuwaeneza kwa wakulima wetu ili waweze kutoa taaluma juu ya kilimo bora na cha kisasa kwa lengo la kuleta tija kwa wakulima wetu.

7. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Kuifanyia ukarabati mkubwa Miundombinu ya Umwagiliaji iliyomo katika bonde hili ili kuwaondolea hasara na usumbufu wanaoupata wakulima wetu siku hadi siku.

8. Kamati ilipofanya ziara katika bonde la Saninga haikuridhika na jinsi utekelezaji wa mradi huo unavyoendeshwa na Wizara na badala yake Kamati inaitaka Wizara kufuatilia kwa karibu maendeleo ya miradi yote iliyopangwa kutekelezwa na Serikali katika bajeti ya mwaka huu. Pamoja na maelezo yaliyotolewa na Wizara kuwa, uingizwaji wa fedha za utekelezaji hauridhishi, Kamati bado inasisitiza kuwa masuala yote

yanayohusiana na maombi ya fedha za utekelezaji wa mradi wowote ule yafanyike kwa maombi ya maandishi na baada ya kipindi fulani wahusika wakumbushie tena kwa maandishi ili Wajumbe wa Kamati wanapofika katika maeneo ya kazi wanapoomba maelezo uwepo ushahidi wa vielelezo vitakavyothibitisha utekelezwaji wa kazi husika.

**BONDE LA UMWAGILIAJI MAJI LA CHEJU NA KILOMBERO**

Kamati pia ilifanya ziara katika Bonde la Cheju na Bonde la Kilombero kwa hapa Unguja, lengo ikiwa ni muendelezo wa kufuatilia utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji maji.

**MAFANIKIO YA MRADI**

Kamati katika ziara yake hii ilielezwa mafanikio ya mradi kama ifuatavyo:-

i) Kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa Bonde la Umwagiliaji la Kilombero kwa 85% kwa kipindi ambacho Kamati ilifika katika eneo hilo. Aidha kwa upande wa Bonde la Cheju utekelezaji wa mradi huo hadi Kamati inafika ilikua ni 80%.

ii) Mitaro ya kupitishia maji katika mabonde yote ya Kilombero na Cheju ilianza kujengwa kwa kutumia saruji wakati awali mitaro hiyo ilikuwa ijengwe kwa udongo.

iii) Kuchimbwa kwa baadhi ya visima ambavyo maji yake yatatumika katika umwagiliaji ni miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika mabonde yote mawili.

iv) Ushirikiano mkubwa uliopo baina ya wananchi na Wizara hasa wananchi wa Cheju ambao wamekua wakiulinda mradi huo kupitia elimu waliyoipata kuhusiana na umuhimu wa mradi na kuamua kuweka ulinzi katika maeneo yote ya utekelezaji wa mradi.

**CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI KATIKA BONDE LA CHEJU NA KILOMBERO**

Pamoja na mafaniko hayo yaliyoelezwa hapo juu bado kuna changamoto kadha zinazokwamisha utekelezaji wa mradi kama zifuatazo:-

1. Katika Bonde la Kilombero Kamati imesikitishwa sana na hatua wanazozichukua baadhi ya wananchi za kuharibu miundombinu ambayo tayari imeshatengenezwa na kuwekwa katika maeneo ya mradi kwa gharama kubwa. Kamati ilijionea baadhi ya uharibifu huo ambapo baadhi ya wananchi wanachimba mchanga katika maeneo yaliyokwisha wekwa miundombinu na wengine wanapeleka mifugo yao katika maeneo ambayo hayana hata malisho ya wanyama. Pia kuna baadhi ya wananchi wamekuwa wakizitumia njia zilizojengwa kwa lengo la kusafirishia mazao pindi mradi huo utakapokamilika jambo ambalo linaharibu miundombinu hiyo kutokana na kutojengwa kwa umadhubuti wa kuweza kuhimili vishindo vya magari makubwa ya mawe.

2. Kamati pia ilisikitishwa na changamotio ya baadhi ya wananchi kuiba mifuniko ya '***kalvats'*** zilizowekwa jambo ambalo linaitia hasara kubwa Serikali.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri serikali kupitia Wizara ya Kilimo, kuendelea kuwapatia elimu wananchi wetu juu ya umuhimu wa uwepo wa miradi hii kwa maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

2. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na watu wa mradi kuanzisha kamati maalumu ya ulinzi shirikishi itakayosaidia kuyalinda na kuyahifadhi na uharibifu maeneo yote ya mradi ili kupeleka mbele kasi ya maendeleo kwa miradi hii na kuiwezesha kumalizika kwa wakati uliopangwa. Baada ya ziara hiyo na kujionea changamoto zote za uharibifu, Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii ilichukua juhudi za kuiita Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kaskazini 'B' na kuzungumza nayo juu ya hatua ambazo wanapaswa kuzichukua kuyalinda maeneo yote ya mradi huu. Kamati ya ulinzi na Usalam ya Wilaya iliahidi kutoa ushirikiano mkubwa katika ulinzi wa mradi huu endapo tu Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo itatoa ushirikiano wa kutosha kwa kutoa taarifa zote muhimu za mradi. Kupitia ripoti hii, Kamati inaopongeza Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kaskazini 'B' kwa kuitikia wito wa Kamati pamoja na kuonesha utayari wa kuilinda miradi ya Serikali ambayo imegharimu fedha nyingi sana katika utekelezaji wake. Aidha, Kamati inaiagiza Wizara ya Kilimo kutoa ushirkiano kwa Kamati za ulinzi na Usalama za Wilaya na Mkoa ambapo kuna miradi inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo, kwa

kuzishirikisha Kamati hizo katika hatua zote zinazotakiwa za ulinzi wa maeneo hayo.

3. Kamati inaishauri Wizara pale miradi hii itakapomalizika maeneo ya kilimo yagaiwe kwa kuzingatia jinsia zote.
4. Kwa upande wa Bonde la Cheju, Kamati imeridhika na utekelezaji wa kazi zinazoendelea kufanywa pamoja na kuwapa pongezi wananchi wa eneo hilo ambao wanatoa ushirikiano wa kutosha kwa Wizara na kuchukua juhudi za ziada za kuweka ulinzi katika eneo lote la mradi.

**MKUTANO BAINA YA MABIBI NA MABWANA SHAMBA UNGUJA NA PEMBA**

Kamati ilipata nafasi ya kukutana na Mabibi na mabwana shamba kwa lengo kusikia changamoto zinazowakabili na baadae Kamati iweze kushauri na kutoa miongozo ambayo itawasaidia katika utendaji wao.

**MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KWA MABIBI NA MABWANA SHAMBA KWA UNGUJA NA PEMBA**

Katika kikao hicho kulikua na mafanikio yaliyoelezwa na mabibi na mabwana shamba kama ifuatavyo:-

1. Kamati ilielezwa kuwa baadhi ya mabibi na mabwana shamba walipatiwa elimu ya kuwasaidia wakulima jinsi ya kulima kilimo chenye tija.
2. Mabibi na Mabwana shamba walipata fursa ya kujadiliana matatizo yao mbele uongozi wa Halmashauri zao na matatizo hayo yalifanyiwa kazi.
3. Kwa upande wa Pemba, Mabibi na Mabwana shamba walifanikiwa kupata ofisi ambazo walikua wakizitumia katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.
4. Mabibi na Mabwana shamba waliieleza Kamati kuwa walifanikiwa kupata vitendea kazi ambavyo viliwasaidia kwa wakati huo kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

## CHANGAMOTO ZA MABIBI NA MABWANA SHAMBA KWA UNGUJA NA PEMBA

Kamati ilipokutana na Mabibi na Mabwana shamba ilielezwa changamoto zifuatazo:

1. Upungufu mkubwa wa mabibi na mabwana shamba ukilinganisha na maeneo yaliyopo ni miongoni mwa changamoto kubwa Kamati iliyoibaini wakati wa mahojiano na wafanyakazi hao. Kamati ilibaini kuwa kwa hivi sasa bibi /bwana shamba mmoja anahudumia wakulima hadi 2000 wakati anatakiwa kuhudumia wakulima 300 hadi 350. Hali hii inawapelekea watendaji hao kuwa katika wakati mgumu wa kutekeleza majukumu yao. Aidha kwa upande wa kisiwa cha Pemba, kwa sasa kuna mabibi / mabwana shamba 21 tu wakati wanaohitajika ni 129, takwimu hii ya kisiwa cha Pemba ni kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa katika ziara ya Kamati iliyofanyika katika bonde la umwagiliaji la Saninga tarehe (8/11/2021).

2. Kamati pia ilielezwa changamoto ya ukosefu wa vitendea kazi ikiwemo usafiri wa kufikia katika maeneo ya wakulima. Katika maelezo ya mabibi / mabwana shamba, ilielezwa kuwa watendaji hawa hawapatiwi hata mafuta kwa wale wenye vyombo vyao wenyewe, hali inayowaweka katika wakati mgumu wa kufanikisha shughuli zao za kila siku.

3. Kutopatiwa fedha za ziada kama motisha kwa watendaji hawa ni changamoto nyengine iliyoelezwa. Kamati imebaini kuwa hali hiyo inawaondolea ari watendaji hao katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi hasa ikizingatiwa kuwa watendaji hawa wanatekeleza majukumu yao katika mazingira magumu.

4. Kamati ilielezwa changamoto ya maslahi duni kwa mabibi / mabwana pamoja na makato makubwa yanayokwenda katika michango mbalimbali kama vile ZSSF, hali hii inarudisha nyuma kasi yao ya maendeleo kiuchumi.

5. Kamati pia ilielezwa changamoto ya uhaba mkubwa wa fedha za kuendeshea shughuli za kilimo kwa mabibi na mabwana shamba. Ilielezwa kuwa mabibi /mabwana shamba hasa kisiwani Pemba hulazimika kuwapatia chochote wakulima pale wanapokutana nao kwa kuwapatia taaluma kuhusiana na mazao yao, kwa sasa jambo hilo halifanyiki kutokana na kukosekana kwa fedha.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inawashauri mabibi na mabwana shamba kuendelea kuwa wazalendo katika kazi zao na waendelee kuwahudumia wakulima kwa kuwapatia elimu inayofaa juu ya kilimo chao ili waweze kulima kilimo chenye manufaa. Kamati inaiomba Wizara ya Kilimo kuwapatia motisho mabibi na mabwana shamba hao kutokana na kazi kubwa na nzito iliyojaa changamoto pale wanapowahudumia wakulima wetu. Kamati inaiomba Wizara ya Kilimo kuhakikisha kwamba mabibi / mabwana shamba wanakuwa na idadi maalumu ya wakulima wanaowahudumia kwa kuajiri mabibi /mabwana shamba wapya ambao watakwenda kusaidiana na wenzao katika majukumu hayo. Kwa sasa kazi wanayokabiliana nayo mabibi / mabwana shamba ni kubwa na nzito ambayo kwa uchache wao hawawezi kuifanya kwa ufanisi ukilinganisha na mahitaji yaliyopo. Kamati inaishauri Wizara kuandaa mfumo maalum wa kilimo '***kilimo mtandao*** utakaorahisisha mawasiliano kati yao na wakulima wao, hali itakayowezesha kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

2. Kamati inaishauri Wizara kuwapatia motisha mabibi / mabwana shamba kwa lengo la kuwaongezea ari ya kufanya kazi pamoja na kuwapa fedha ya mafuta/nauli ili waweze kufanya kazi zao kwa wakati katika hayo maeneo watakayoweza kutafanyia kazi.

3. Kamati inaishauri Serikali endapo itaona haja ya kufanya mabadiliko ya sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) ifanye mabadiliko hayo kwani mabadiliko ya makato kwa wafanyakazi yaliyopo ndani ya sheria hiyo kimekua ni kilio kikubwa kwa takriban wafanyakazi wengi wa Serikali wakiwemo mabibi / Mabwana shamba na baadhi ya walimu.

4. Kamati inaishauri Wizara kuwahamasisha mabibi na mabwana shamba kuandaa mpango kazi utakaowaongoza katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku na hatimae kuweza kujifanyia tathmini wao wenyewe juu ya mpango kazi huo.

5. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuiingizia fedha za bajeti Idara ya Kilimo kama zilivyopangwa na fedha hizo ziingizwe kwa wakati ili malengo yaliyopangwa yaweze kukamilika.

## MASHAMBA DARASA YA WAKULIMA

Kamati ilipata nafasi ya kufanya ziara katika shamba darasa linalomilikiwa na kikundi cha ushirika cha uzalishaji wa mboga mboga na mazao ya chakula kilichopo Gando kisiwani Pemba (Gando Farmers Group).

Kikundi hiki kilianzishwa mwaka 2017 kikiwa na wanachama 9, wanawake watano 5 na wanaume 4 na kwa sasa kikundi kina wanachama 15 wakiwemo wanaume 6 na wanawake 9.

Kikundi kinajihusisha na kilimo cha mazao ya mboga mboga na mazao mengine ya chakula yakiwemo viazi vitamu, viazi lishe, mahindi, tungule na pili pili boga. Shamba darasa la kikundi hiki linalotumika kwa shughuli hizo lina ukubwa wa nusu eka ambapo wakulima kutoka katika maeneo mbali mbali hupata fursa ya kujifunza namna bora ya kulima kilimo cha kisasa na chenye tija.

**CHANGAMOTO ZILIZOPO KATIKA KIKUNDI HIKI**

Kamati katika ziara yake hiyo ilielezwa na kujionea changamoto zifuatazo:-

1. Kukosekana kwa maji ya uhakika ni miongoni mwa changamoto zinazokwamisha shughuli za uzalishaji katika eneo hilo ambapo Kamati ilielezwa kuwa hadi sasa kikundi hakina chanzo chake binafsi cha maji hali inayopelekea kutumia kisima cha jamii katika kuendesha shughuli za kilimo jambo linalowakwaza na kuwapotezea muda wakulima hao.

2. Changamoto nyengine ni uzalishaji mdogo wa mazao unaotokana na uchache wa mifumo ya umwagiliaji maji. Upungufu wa mifumo ya kisasa ya umwagiliaji maji ***'drips'*** ni muhimu sana katika kilimo cha kisasa ambacho kinalenga zaidi katika upatikanaji wa mazao mengi na bora.

3. Kukosekana kwa mitaji kwa wanakikundi ni changamoto nyengine inayokwamisha juhudi za wanakikundi na kupelekea kutoimarika kwa kikundi na kupiga hatua za kimaendeleo.

4. Changamoto ya kukosekana kwa viwango vikubwa vya elimu kwa wanakikundi ni jambo linalowakosesha fursa wanakikundi hao ambapo wakulima walio wengi hawana taarifa ya fursa zilizopo hivi sasa ulimwenguni zitakazowawezesha wao kupata mikopo na misaada

ambayo kwa kiasi kikubwa ingeweza kuwasaidia katika kukiendeleza kikundi chao.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara inapoamua kuanzisha mashamba darasa kwa wakulima, ihakikishe kuwa inaandaa miundombinu ya uhakika ambayo itawasadia wakulima waweze kufanya shughuli zao kwa uhakika pasi na usumbufu wa aina yoyote. Aidha, Kamati inatoa rai kwa Wizara kuwashirikisha viongozi wa Majimbo katika shughuli hizo ili baadhi ya changamoto zinazojitokeza washirikiane kuzitatua.

2. Kamati inatoa ushauri kwa Wizara kuwa karibu na wanakikundi wanaojitolea kama hawa, ili zinapotokea fursa mbali mbali zenye manufaa kwa wakulima wetu ziweze kuwasaida katika shughuli zao pamoja na kuwasaidia katika mambo mbali mbali ya kitaalamu yanayohitaji ujuzi wa ziada.

## UJENZI WA MAGHALA YA KUHIFADHIA CHAKULA

Miongoni mwa shabaha zilizoelezwa katika kitabu cha Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri katika Programu ya Maendeleo ya Kilimo, Programu ndogo ya Maendeleo ya Huduma za kilimo na Uhakika wa Chakula ni kujenga maghala mawili ya kuhifadhia chakula kwa Unguja na Pemba.

## UJENZI WA GHALA JIPYA LA KUHIFADHIA CHAKULA PEMBA

Kamati ilifika katika eneo linalojengwa Ghala jipya la kuhifadhia chakula kisiwani Pemba na kupewa maelezo kuhusiana na ujenzi wa ghala hilo ambapo ilielezwa kuwa mkandarasi yuko nyuma kwa muda wa miezi miwili.

Kamati baada ya kufanya ziara katika ghala hilo haikuridhika na kuamua kufanya ziara kwa mara ya pili tarehe 17/01/2022 kwa lengo la kuangalia maendeleo ya ujenzi huo.

Hadi kufikia tarehe iliyotajwa hapo juu, utekelezaji wa mradi huo ulikua umefikia 40% tu tofauti na makubaliano ya kimkataba yalivyo. Kutokana na hali hiyo na maelezo kutoka pande zote mbili (Mteja ambae ni Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Mkandarasi) Kamati iliamua kumuita Mkandarasi ili aje atoe ufafanuzi wa kwanini ujenzi wa mradi huo haukufikia malengo yaliyokusudiwa ambapo

ilielezwa kuwa jengo hilo lilitarajiwa kuekewa jiwe la msingi katika sherehe za Mapinduzi zilizopita.

Mkandarasi aliieleza Kamati kuwa hana fedha za kutosha na anadai fedha zake jambo ambalo lilikanushwa na msimamizi wa mradi ***'Coordinator'*** ambae aliieleza Kamati kuwa Mkandarasi hakua akidai fedha ya aina yoyote na badala yake yeye ndie anaedaiwa kazi alizoahidi kuzitekeleza. Ifahamike kwamba mradi huu unasimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia mradi wa kudhibiti Sumukuvu Tanzania (TANPAC) ambapo mradi huu unajenga maghala 14 Tanzania nzima na mawili yanajengwa hapa Zanzibar, moja Pemba (Dodeani) na moja Unguja (Kizimbani).

Baada ya kupokea taarifa kutoka pande zote na kufanya kikao na mkandarasi, Kamati inatoa ushauri ufuatao.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati iliishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa kushirikiana na msimamizi wa mradi ***'Coordinator'*** waandae ripoti itakayokua na maazimio ya kumbana mkandarasi kwa kueleza lini atamaliza kazi ya ujenzi na kuikabidhi Serikalini.

2. Kamati inaishauri Wizara na msimamizi wa mradi ***'Coordinator'*** wajifunze kupitia changamoto zilizojitokeza katika mradi huu kwa kufanya uchunguzi wa ziada **'extra vetting'** kwa wakandarasi na wasiamini **'document'** pekee zinazowasilishwa na wakandarasi wakati wa tenda ya kuomba kazi kwani wengi wao wanawasilisha '**document**' za uongo.

3. Kamati inachukua nafasi hii kuwashauri wakandarasi wazalendo kuwa waaminifu na kufanya kazi zao kwa umakini ili wasiiangushe Serikali kwa imani iliyowapa. Kamati inayazungumza haya kutokana na ushahidi kwamba kampuni nyingi za kizalendo hazifanyi vizuri pale zinapoaminiwa kupewa kazi za miradi mbali mbali ya kimaendeleo hapa nchini.

4. Kupitia ripoti hii, Kamati inaiagiza Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kutoa taarifa kwa Kamati ya kila hatua ya ujenzi inayoendelea kuanzia sasa. Kamati inatoa agizo hilo, kutokana na makubaliano yake na Mkandarasi ya kwamba hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Februari

mwezi ambao alipaswa kumaliza kazi awe angalau amefikia 80% ya ujenzi.

**PROGRAMU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU**

Programu hii inasimamiwa na Idara ya Misitu na ina jukumu la kuwashirikisha wananchi kutunza na kuendeleza rasilimali za misitu na wanyama pori pamoja na kusimamia uhifadhi wa misitu, mashamba ya Serikali, viumbe hai pamoja na mazingira yao, sambamba na kusimamia mahitaji ya soko na matumizi endelevu ya rasilimali misitu.

Programu hii inajumuisha Program ndogo mbili ambazo ni Program ndogo ya Maendeleo na Uhifadhi wa Misitu.

**PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO NA UHIFADHI WA MISITU**

Programu hii inalengo la kusimamia na kuhifadhi misitu, wanyama pori pamoja na mzingira yao. Katika kufuatilia utekelezaji wa Programu hii Kamati ilipata fursa ya kutembelea maeneo yafuatayo:-

i) Hifadhi ya Msitu wa Jozani na Ghuba ya Chwaka;
ii) Msitu wa Uzi Ng'ambwa; na
iii) Msitu wa Hifadhi wa Ngezi;

**HIFADHI YA MSITU WA JOZANI NA GHUBA YA CHWAKA.**

Msitu wa Jozani ni miongoni mwa msitu wa hifadhi wenye hadhi ya Kimataifa ambao umeanzishwa mwaka 2004 na kusajiliwa rasmi mwaka 2005. Msitu huu una zaidi ya ukubwa wa hekta 5000 ambapo umezungukwa na vijiji 9 vikiwemo kijiji cha Kitogani, Charawe, Chwaka, Ukongoroni, Unguja Ukuu na Pete. Kamati ilifanya ziara na kupewa maelezo kuwa msitu huu unaendelezwa kwa mashirikiano na jamii yote ya vijiji vilivyotajwa hapo juu na kuelezwa mafanikio kadhaa yaliyopatikana kama ifuatavyo:-

**MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA HIFADHI YA MSITU WA JOZANI NA GHUBA YA CHWAKA**

Kamati ilielezwa mafanikio yafuatayo:-

1. Idara ya Misitu imeweza kuweka uhusiano mzuri na wana vijiji vyote vinavyozunguka hifadhi ya msitu huu kwa kugawanya asilimia kadhaa ya mapato kwa wanavijiji hao kupitia Kamati zao walizoziunda wenyewe ambazo zimekua mstari wa mbele kuhamasisha uhifadhi wa maeneo yote ya msitu.
2. Idara kwa kushirikiana na Kamati za wana vijiji zinafanya juhudi ya kubuni vivutio vipya ndani ya msitu ambavyo vitasaidia kuongezeka kwa mapato na kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaotembelea msitu huo.

**CHANGAMOTO ZA MSITU WA JOZANI NA GHUBA YA CHWAKA**

Pamoja na mafanikio hayo kuna changamoto zifuatazo zilizoelezwa mbele ya Kamati kama ifuatavyo:-

1. Wananchi waliozunguka msitu wa hifadhi wana tabia ya kuchoma moto msitu hali inayopelekea kupoteza viumbe hai vilivyomo katika msitu huu ambavyo ni rasilimali kubwa kwa taifa letu. Aidha, Kamati ilielezwa tabia ya baadhi ya wananchi kuvamia maeneo ya hifadhi ya Msitu kwa lengo la kukata kuni, kulima na wengine kuvuna asali, hali inayoharibu uhalisia na uasili wa msitu huu.
2. Kamati ilielezwa changamoto ya kutopimiwa na kukosekana kwa hati miliki ya baadhi ya maeneo ya wananchi kwa ajili ya kilimo.
3. Kamati ilielezwa changamoto ya kutolipwa kwa baadhi ya wananchi wa Pete baada ya kufanyika kwa ujenzi wa daraja na ardhi ya wananchi hao kuchukuliwa.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inashauri wadau wote waliouzunguka msitu waongeze wigo wa kutoa elimu zaidi kwa jamii juu ya umuhimu wa kuuhifadhi na kuulinda msitu huu kwa faida ya taifa zima.

2. Kamati inaishauri Idara ya Misitu kufanya juhudi za kuyapatia maeneo yote ya msitu hati miliki ambayo itasaidia uhifadhi mzuri wa eneo lote la msitu.

3. Kamati inauagiza uongozi wa Msitu wa Jozani kuvitangaza vivutio vilivyomo ndani ya msitu huu kwa lengo la kuwavutia zaidi watalii wa ndani na wa nje, hii itasaidia sana kuukuza uchumi wa taifa letu kwani tunafahamu fika kuwa uchumi wetu unasaidiwa sana na sekta hii ya utalii.

4. Kamati inashauri kutangazwa kwa maajabu yaliyomo ndani ya msitu huu wakiwemo wanyama adimu kama vile, Kima punju, paa nunga nakadhalika pamoja na kufanya utafiti kuhusiana na asali inayopatikana ndani ya msitu huu. Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza kutangazwa kwa maajabu ya msitu huu ikiwemo kutangaza maajabu ya '***mahogany trees'*** ya Jozani. Hayo yote yatawezekana kwa Idara kutafuta wafadhili au kwa kushirikiana na Wizara kufanya utafiti wa kina kuhusiana na mambo haya.

5. Kamati imebaini kuwa miti inayopatikana katika Msitu wa Jozani ni ya kipekee, hivyo Serikali kupitia taasisi husika ina wajibu wa kuutangaza upekee huo kwa wageni na kwa wenyeji kwa kuwapatia utambulisho maalum utakaoweza kuacha athari popote watakapokuwa ili kutoa taswira halisi ya msitu huu. Aidha, Kamati inaiagiza Idara ya Misitu kufanya utaratibu kwa kubuni kitu ambacho kitaacha alama au athari kwa watalii wanaokuja kutembelea eneo la hifadhi ya Msitu huu.

6. Kamati ilipata fursa ya kutembelea mabwawa ya kufugia samaki ndani ya hifadhi ya msitu huu wa Jozani na kujionea hali halisi ya ufugaji. Kupitia mradi huu Kamati inaishauri Serikali kupitia taasisi husika kufanya tafiti katika mabwawa haya kwa lengo la kupiga hatua ya kimaendeleo ndani ya miradi hii, ni vyema tafiti hizo zikafanywa na taasisi yenyewe na tuache tabia ya kusubiri wataalamu kutoka nje.

7. Kamati inaiomba Jumuiya inayomiliki mabwawa haya ya kufugia samaki kutoa ujuzi huu walionao kwa vijana wengine huko nje, lengo ni kuwawezesha vijana hao kujiajiri wenyewe kwani miradi kama hii ina nafasi kubwa ya kutoa ajira kwa vijana wengi.

8. Kwa vile ndani ya mabwawa haya kumeambatana na mfumo wa maji chumvi ya bahari, Kamati inawaomba wamiliki wa mabwawa hayo waandae andiko kwa wafadhili ili waweze kusaidiwa kupata '***Screen mashine'*** ambayo itawekwa ndani ya bwawa kwa lengo la kuchunguza mambo yanayotendeka ndani ya mabwawa hayo.

9. Kamati inaiagiza Idara ya Misitu kuzidisha ushirikiano wake na wananchi pamoja na zile taasisi ambazo zina mashirikiano ya moja kwa moja na Idara hii, ili kuimarisha ulinzi katika maeneo ya Msitu kwa lengo la kunusuru uharibifu unaoendelea kufanywa na wananchi waishio karibu na msitu huu.

**MSITU WA UZI NG'AMBWA**

Msitu huu ni miongoni mwa misitu ya jamii wenye urefu wa hekari 110, ulioanzishwa katika mwaka 2011 kwa makubaliano baina ya wanakijiji waliozunguka msitu huu na Wizara ya Kilimo.

**MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KUPITIA MSITU WA UZI NG'AMBWA**

Kamati kupitia hifadhi ya msitu huu ilielezwa mafanikio yafuatayo:-

1. Baadhi ya wananchi wameweza kupatiwa mafunzo ya jinsi ya kuutunza, kuusimamia na kuutumia msitu huu kwa lengo la kujiletea maendeleo yao ya kila siku.

2. Wananchi wanaozunguka eneo la msitu waliweza kushirikishwa katika mambo yote muhimu yanayohusiana na msitu huu.

3. Wanakijiji wanaozunguka msitu huu walifanikiwa kuunda Kamati ambayo inahusisha vijiji vyote vya jirani ya eneo la msitu yenye lengo la kuulinda na kuuhifadhi.

**CHANGAMOTO ZA MSITU WA UZI NG'AMBWA**

Pamoja na mafanikio hayo kuna changamoto zifuatazo katika Msitu wa Uzi Ng'ambwa:-

1. Kamati ilisikitishwa sana kuona hadi Kamati inafika katika eneo hilo Idara ya Misitu na Maliasili imeshindwa kuupandisha hadhi Msitu huo na kuwa Msitu wa Hifadhi pamoja na kwamba Serikali ilisharidhia na kuidhinisha fungu la fedha kwa utekelezaji wa suala hili.

2. Kamati ilipatiwa taarifa ya msitu na kuelezwa kwamba Idara ya Misitu na Maliasili bado haijatumia fursa ya matumizi ya rasilimali zilizomo ndani ya msitu huo ambazo zingesaidia kuongeza pato la Tiafa. Fursa hizo ni kama vile wanyama adimu wanaopatikana katika msitu huo. Miongoni mwa wanyama hao ni kama vile kimapunju, paa wadogo, nyoka, aina tofauti za ndege, wadudu, sehemu za matambiko (sehemu za jadi), makaburi na hata koko.

3. Kamati ilifahamishwa kwamba, Msitu huu hadi sasa unakabiliwa na changamoto ya uvamizi. Wageni wanaingia katika Msitu na kufanya uharibifu kwa kukata miti kwa matumizi yao binafsi. Changamoto hii inasababishwa na umbali wa maeneo ya makaazi ya wanakijiji wanaouzunguka msitu huu.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kutokana na rasilimali zilizomo ndani ya msitu huu, Kamati inaishauri Serikali kupitia Idara ya Misitu na Maliasili kuupandisha hadhi msitu huohasa ukizingatia fungu lake la bajeti tayari limeshatoka mda mrefu.

2. Kutokana na uharibifu unaofanywa ndani ya msitu huu, Kamati inaishauri Idara ya Misitu kuimarisha ulinzi katika msitu huu kwa lengo la kuondokana na uharibifu unaoendelea kufanywa na wananchi.

3. Kamati inaipongeza Idara ya Misitu kwa juhudi ilizozichukuwa za kuwapatia elimu wanajamii kuhusu umuhimu wa kuusimamia na kuutunza msitu huu kwa matumizi endelevu.

**MSITU WA HIFADHI WA NGEZI**

Msitu wa Hifadhi wa Ngezi ni moja wapo ya misitu ya hifadhi ambayo Kamati ilipata nafasi ya kuitembelea na kujionea hali halisi ya maendeleo ya Msitu huo.

**MAFANIKIO YANAYOPATIKANA KUPITIA MSITU WA NGEZI**

1. Kamati ilielezwa kuwa kupitia msitu wa hifadhi wa Ngezi wananchi wanaozunguka msitu huu wanapatiwa asilimia ya fedha ambayo inatokana na pato linalopatikana kupitia msitu huo. Fedha hizo zinawasaidia wananchi katika shughuli zao mbali mbali za maendeleo ambapo kupitia vikundi vyao huweza kufanya shughuli za maendeleo kupitia fedha hizo.

**CHAMNGAMOTO ZINAZOUKABILI MSITU WA HIFADHI WA NGEZI**

Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati, Msitu huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

1. Kamati ilielezwa changamoto ya wizi na udokozi wa baadhi ya maliasili ziliomo ndani ya Msitu huu. Hili ni tatizo linaloitia hasara kubwa sana Serikali yetu, baadhi ya wananchi huuvamia msitu huu kwa lengo la kukata na kuchukua maliasili ziliomo ikiwemo miti ya asili kama vile mivule, minunga ambayo ni hazina kubwa iliyomo katika Msitu huu. Aidha, kuna changamoto ya kutosafishwa kwa wakati kwa mipaka yote inayolizunguka eneo la msitu na kusababisha changamoto ya baadhi ya

wanavijiji kuvamia baadhi ya maeneo ya msitu kwa shughuli zao za kijamii.

2. Kamati pia ilielezwa changamoto ya mashirikiano madogo yaliopo kati ya vyombo vya usalama kama vile Polisi na uongozi wa Msitu. Hii inajidhihirisha pale uongozi unapopeleka malalamiko ama kesi kituoni na vyombo hivi kushindwa kutoa hukumu kwa wahalifu kwa mujibu wa sheria zilizopo.
3. Msitu unakabiliwa na changamoto ya kuungua moto mara kwa mara hususani kwa siku za kiangazi. Baadhi ya wananchi huvamia msitu kwa lengo la kuvuna asali, kuwinda wanyama kama vile paa, kuvuta sigara hali inayoitia hasara kubwa Serikali. Kamati ilielezwa kuwa hivi karibuni eneo lenye urefu wa takribani hekta 4.1 limeungua moto na kuathiri viumbe hai vilivyomo katika Msitu huo.
4. Changamoto nyengine iliyoelezwa ni ile ya upungufu mkubwa wa walinzi katika eneo la msitu. Hadi Kamati inafika katika eneo hili, ilielezwa kuwa kuna walinzi sita tu wanaofanyakazi katika eneo lote la msitu jambo ambalo linawapa wakati mgumu wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi hasa zikilinganishwa na kazi wanazozifanya za kulinda eneo lote la hekta 2900.
5. Changamoto nyengine ni matumizi ya silaha duni kwa walinzi wa msitu huu. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati, walinzi hawa kawaida hutumia mapanga katika kukabiliana na wahalifu wanaouhujumu maeneo yote ya msitu.
6. Upotevu wa wanyama adimu ndani ya Msitu wa Ngezi ni tatizo ambalo kwa kiasi kikubwa linaweza kuathiri uchumu wetu hasa ukizingatia msitu huu ni kivutio kikubwa cha utalii. Baadhi ya wanyama wanasadikiwa kutoweka kabisa ndani Msitu huu akiwemo nguruwe ambae inasadikiwa alikua akipatikana ndani ya msitu huu.
7. Tatizo jengine kubwa linaloonekana katika uendelezaji na uhuishaji wa Msitu wa Ngezi ni ukosefu wa miradi jambo linalopelekea kutofika kwa watalii kwa wingi katika eneo hilo. Hadi Kamati inafika katika msitu huu ilielezwa kuwa hakuna mradi hata mmoja unaoweza kusaidia katika kuingiza mapato.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Wizara kupitia Idara ya Misitu Pemba kuimarisha ulinzi ndani ya Msitu wa Ngezi. Kamati inaona ni busara uongozi wa Msitu kuishirikisha kikamilifu jamii iliyozunguka eneo lote la msitu huu kwani wao ndio wadau wakuu wa Msitu huo. Kamati inaamini kuwa uvamizi huo unaweza kuzuia kupitia vijiji vinavyozunguka eneo la msitu ambavyo ni vijiji kumi. Kwa umoja wao vijiji hivyo vinaweza kuzuia wimbi la uharibifu unaofanywa kwa makusudi na wahalifu wa eneo hilo.
2. Kamati inavisisitiza vyombo vya ulinzi na usalama kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Kilimo hasa katika suala zima la ulinzi katika maeneo yetu yote yenye rasilimali za Taifa. Aidha tunavisisitiza vyombo hivyo pale wanapopelekewa wahalifu na malalamiko na Wizara wayafanyie kazi kwa kuchukua hatua stahiki kwa wahalifu hao kama sheria zinavyoelekeza.
3. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kukaa pamoja na wenzetu wa vyombo vya ulinzi na usalama na kujadiliana juu ya kuweza kuwakabili wahalifu na wahujumu wa Msitu wa Ngezi kwa kuwapatia adhabu inayostahiki kwa makosa wanayoyatenda .
4. Kamati pia inaishauri Wizara kupitia Idara ya Misitu Pemba, kufanya usafi wa mara kwa mara katika mipaka ya eneo lililozuzunguka Msitu wa Ngezi, hii itasaidia kuepusha migogoro kati ya Idara na wananchi walio pembezoni mwa Msitu huo.
5. Kamati inaishauri Wizara kupitia Idara ya Misitu, kwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia kwa kuwapatia walinzi wa eneo la msitu silaha za kisasa ambazo wataweza kuzitumia katika kukabiliana na wale wote wanaohujumu msitu huo. Aidha, Kamati inashauri Wizara, iisaidie Idara ya Misitu kupata ulinzi wa uhakika kutoka katika vikosi vyetu vya SMZ.
6. Kamati inaishauri Wizara kupitia Idara ya Misitu kuwa wabunifu na kuweza kubuni miradi itakayoweza kuwavuta watalii wa nje na wa ndani, lengo ni kuongeza pato linalotokana na msitu huo. Aidha, Kamati inaisisitiza Wizara kupitia Idara ya Misitu kuvitangaza vivutio vilivyomo katika msitu huu kwa lengo la kuwavutia watalii wa nje na wa ndani na kuongeza pato la Taifa.
7. Kamati inaishauri Wizara kupitia Idara ya Misitu kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa Msitu wa Ngezi. Kamati inafahamu uwezo mdogo walionao Wizara kifedha kuwapaleka wafanyakazi wake nje ya nchi basi inapenedekeza japo kuwapeleka katika Msitu wa Jozani ili kuangalia maendeleo yaliyopatikana katika msitu huo na kuweza kuchukua uzoefu.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO

Programu ya Maendeleo ya Mifugo jukumu lake kubwa ni kuendeleza sekta ya mifugo na kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake.
Programu hii imeundwa na program ndogo mbili ambazo:

i) Programu ndogo ya uzalishaji wa mifugo; na
ii) Programu ndogo ya utibabu wa mifugo.

## ZIARA ZA KAMATI KUANGALIA MAENDELEO YA PROGRAMU YA UZALISHAJI NA UTABIBU WA MIFUGO

Programu hii inalenga kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake.

Kamati ilifanya ziara katika kituo cha kuzalisha gesi ambacho pia kinahifadhi mbegu za ng'ombe wa sindano ambacho kipo Maruhubi Unguja. Kamati ilifanya ziara katika kituo hiki ambacho ni kituo tegemezi kwa wafugaji wetu ambao kwa kiasi kikubwa wamekua wakikitegemea katika shughuli zao za ufugaji. Kituo hiki kina mtambo wa kuhifadhia gesi za upandishiaji wa ng'ombe wa sindano ambao ulinunuliwa mwaka 2008 kwa gharama ya shiingi milioni 400 kutoka nchini Uholanzi.

## MAFANIKIOYALIYOPATIKANA KATIKA KITUO CHA KUZALISHA GESI

Kuna mafanikio kadhaa yaliyoelezwa kwa Kamati kama ifuatavyo:-

1. Kituo kilifanikiwa kuwasaidia wananchi wasiokua na uwezo mkubwa kuweza kupata huduma zinazotolewa kwa bei nafuu jambo ambalo liliwasaidia kuwa na mifugo bora na ya uhakika.

2. Kituo kiliiwezesha Idara ya Mifugo kupata mapato kupitia fedha walizokua wakilipa wananchi wanaopata huduma za kupandishia ng'ombe wa sindano.

3. Kituo kilifanikiwa kutoa elimu kwa wafugaji hasa wa vijijini kupitia shehia zao ambapo wafugaji hao waliweza kupata mifugo bora na yenye afya.

**CHANGAMOTO ZINAZOKIKABILI KITUO**

Kamati katika ziara yake ilielezwa changamoto zifuatazo ambazo zimekua zikikwamisha maendeleo ya kituo hicho.

1. Mtambo wa kuzalishia gesi ni wa muda mrefu hali inayopelekea kushuka kwa kiwango cha uzalishaji wa gesi.

2. Kamati ilielezwa kuwa mtambo huo ulikaa muda mrefu bila kufanyiwa ***'service'*** jambo ambalo limepelekea mashine hiyo kuharibika na kusababisha hasara katika uzalishaji wa gesi.

3. Kamati ilielezwa kuwa ng'ombe waliopo kituoni hapo ni wapevu mno na hawawezi kutoa mbegu.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kukifanyia matengenezo kituo cha gesi cha kuhifadhia mbegu za ng'ombe wa maziwa kiliopo Maruhubi kwa vile kituo hicho ni tegemezi kwa wafugaji walio wengi hasa wa vijijini ambao hali zao za kifedha si nzuri. Aidha, Kamati inashauri kituo kiboreshwe kwa kupatiwa ng'ombe kwa wingi hasa madume walio bora ili kituo kiweze kutoa huduma zilizo nzuri na endelevu.

2. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Malisili na Mifugo kukiwezesha kituo hiki kiweze kujiendesha kibiashara na kiachane na kutegemea mapato yatokanayo na mifugo pekee. Kituo

kibadilike kiachane na hali iliyopo na iwatoze wananchi / wafugaji bei kulingana na soko.

3. Kamati inaishauri Serikali kutafuta mbinu zitakazowezesha kila kituo kiwe na mtungi wake wa kuhifadhia gesi kwa lengo la kuondoa usumbufu kwa wafugaji wetu.

4. Kamati inaishauri Serikali kununua mtambo mwengine mpya wa kuhifadhia gesi na kuachana na kuufanyia matengenezo mtambo uliopo sasa hasa ikizingatiwa kuwa mtambo huo ni wa muda mrefu na vifaa vyake vimeshachakaa. Kuendelea kuufanyia matengenezo mtambo huo ni kujitia hasara. Hivyo, Kamati inaishauri Idara ya Maendeleo ya Mifugo kufanya haraka kuandika waraka Serikalini na kuelezea mahitaji ya kununua mtambo mpya.

**KIKUNDI CHA WAFUGAJI NG'OMBE WA MAZIWA PIKI-TUNDWA**

Kamati ilifanya ziara yake katika kikundi hiki kilichopo Piki Tundwa na kujionea hali halisi ya wafugaji hao, ambao kwa kiasi kikubwa wamefanikiwa katika ufugaji wao. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana na kikundi hiki ni kama:-

1. Kamati ilielezwa kuwa wafugaji wa kikundi hiki walifanikiwa kuongeza idadi ya lita za maziwa kutoka lita 20 hadi lita 70 kwa siku. Hali hiyo inatokana na elimu nzuri ya kitaalamu waliyopatiwa na Idara ya Mifugo.

2. Kikundi cha wafugaji wa maziwa waliopo Piki - Tundwa walifanikiwa kutanua kikundi chao ambapo waliweza kuongeza kituo chengine cha ufugaji wa ng'ombe.

3. Wafugaji wa ng'ombe walifanikiwa kupatiwa mafunzo ya afya ya mifugo elimu ambayo imewasaidia sana katika kutekeleza majukumu yao.

4. Kikundi cha ufugaji wa ng'ombe kimefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuwaelemisha wananchi wenzao wa maeneo ya karibu jambo lililopelekea ushirikiano wa hali ya juu hasa katika suala zima la ulinzi wa mifugo.

**CHANGAMOTO ZINAZOKIKABILI KIKUNDI CHA WAFUGAJI NG'OMBE WA MAZIWA PIKI-TUNDWA**

1. Kamati ilielezwa kuwa vituo vingi vya wafugaji wa ngombe wa maziwa vimegatuliwa na kukabidhiwa kwa Halmashauri tokea mwezi Machi 2014 kwa kipindi ambacho Kamati ilifanya ziara. Kutokana na uhalisia na uzowefu wa kazi za Wizara ya Kilimo, Kamati inaamini kuwa kuna changamoto nyingi sana zinazowakabili wafugaji hao ambao ni wananchi wanyonge wa Taifa hili wanaohitaji msaada wa Serikali.

2. Changamoto nyengine ambayo Kamati ilielezwa na wafugaji hawa ni ile ya kukosekana kwa soko la uhakika la kuuzia maziwa yanayozalishwa ndani ya kikundi hiki. Changamoto hii inawaathiri sana wafugaji hawa kwa vile wanunuzi wa maziwa yanayozalishwa hawakidhi haja na hatimae kikundi hiki kinangia hasara kubwa. Takribani lita 70 za maziwa huzalishwa kwa kila siku ndani ya kikundi.

3. Kuyumba kwa vituo vya uuzaji wa maziwa ni changamoto nyengine inayowakabili wafugaji hawa. Kwasasa vituo hivi vinakabiliwa na ukosefu wa majenereta ambayo yangeweza kutumika pale umeme unapozimwa, pia kuna tatizo la upungufu wa mafriza ya kuhifadhia maziwa. Mafriza yaliyopo hivi sasa hayakidhi mahitaji. Aidha Kamati ilielezwa kuwa vituo hivi viligharimu fedha nyingi sana katika matengenezo yake lakini kuna baadhi ya vituo hivyo havifanyi kazi yoyote jambo ambalo Kamati inaona si sahihi.

4. Kamati pia ilelezwa tatizo la upungufu wa upatikanaji wa mbegu bora za kupandishia ng'ombe wa maziwa. Pamoja na upungufu huu, ilielezwa kuwa mbegu hizi ni ghali mno hali inayopelekea uzalisahwaji mdogo wa ng'ombe wa maziwa. Hadi Kamati inafika katika kikundi hiki ni ng'ombe thelathini (30) tu waliopo ambapo kwa mujibu wa muda wa uanzishwaji wa kikundi ilitarajiwa kikundi kiwe kina idadi ya ng'ombe mia moja (100).

5. Kukosekana kwa wataalamu waliopatiwa mafunzo ya upandishaji wa ng'ombe wa maziwa ni changamoto nyengine inayowakabili wafugaji hao. Kamati ilibaini kuwa baadhi ya wakati nafasi za kujifunza kwa wafugaji hawa zinachukuliwa na wakubwa na kuwakosesha fursa wanazostahiki, jambo linalorudisha nyuma muitiko na ari kwa wafugaji wetu.

6. Usafiri wa uhakika kwa wafugaji kuyasafirisha maziwa kutoka katika vikundi vya kuzalisha hadi katika vituo vya kuuzia maziwa, ni tatizo ambalo wakati mwengine husababisha maziwa kuharibika njiani kabla ya kufika vituoni kwa kuuzwa hali inayowatia hasara kubwa wafugaji hawa.

7. Bei ya maziwa hairidhishi kulinganisha na gharama za uzalishaji. Hii ni changamoto nyengine ambayo wafugaji wanakabiliana nayo ambayo kwa kiasi kikubwa inarejesha nyuma kasi ya ufugaji na uzalizalishaji wa maziwa.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa kuyaona madhaifu yaliyokua katika dhana nzima ya ugatuzi ambapo suala hilo lilipelekea baadhi ya vituo vya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa kuingia katika mkumbo huo. Kamati inayasema hayo kutokana na uchunguzi wake mdogo tu ilioufanya ambapo ilibaini kuwa kabla ya ugatuzi vituo vingi vya wafugaji vilikua vikijiendesha vizuri, lakini mara tu baada ya ugatuzi baadhi ya vituo vilirudi nyuma kimaendeleo na kupelekea zile hatua na juhudi kubwa zilizochukuliwa na Wizara pamoja na wafugaji wetu kupotea bure.

2. Kamati inaishauri Serikali kufanya juhudi za haraka na za makusudi kutafuta soko la uhakika la kuuzia maziwa yanayozalishwa na wafugaji wetu. suala hili limekua ni changamoto sugu sana kwa wafugaji wetu na kupelekea wengine kukata tamaa kwa vile wanunuzi wa maziwa yanayozalishwa hawakidhi haja na hatimae kikundi hiki na wafugaji huingia hasara kubwa.

3. Kamati inaishauri Serikali na Wizara kwa ujumla kufanya juhudi za kuwapatia majenereta na mafriza wafugaji wetu hasa kwa wale waliooneshа nia ya kuendeleza mifugo yao. Jambo hilo litawasaidia katika shughuli zao na kuondoa malalamiko mengi yaliyopo hivi sasa.
4. Kamati inaishauri Wizara kuendelea na juhudi zake za kuwasaidia wafugaji wetu kwa kuwasaidia kupata wafadhili na misaada mbali mbali itakayowasaidia wafugaji wa ng'ombe wa maziwa katika shughuli zao.

5. Kamati haikuridhika na taarifa iliyopewa wakati wa ziara katika kikundi cha wafugaji wa Piki – Tundwa kuwa kuna baadhi ya nafasi za mafunzo wanazichukua **'WAKUBWA'** nafasi ambazo wangezipata wahusika hasa wafugaji zingewasaidia kupata elimu ambayo wangeitumia kuendeleza mifugo yao. Kamati inachukua nafasi hii kulikemea vikali jambo hili na inawataka watendaji wa Wizara kuacha mara moja tabia hizo. Aidha Kamati inaishauri Wizara kuongeza kasi ya kuajiri wataalamu wa masuala ya upandishaji wa ng'ombe wa maziwa pamoja na kufanya juhudi za kuwasomesha zaidi hao waliopo hivi sasa.

6. Kamati inaitaka Wizara ya Kilimo ikae pamoja na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuliangalia upya suala la soko na bei ya maziwa kwa wafugaji wetu hasa ikizingatiwa kuwa wafugaji hawa wanatumia nguvu nyingi katika uzalishaji huo.

7. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, kuliangalia kwa jicho la karibu sana na kulipa msukumu mkubwa suala la upatikanaji wa mbegu bora za ng'ombe wa maziwa ili kusudi tuweze kuwawezesha wafugaji wetu kupata tija katika ufugaji wao.

8. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuwapatia wafugaji wetu usafiri wa uhakika japo kwa kuwapatia usafiri kwa njia ya mkopo ili kusudi waweze kunusuru bidhaa yao hii iweza kufika kituoni ikiwa salama. Kama tujuavyo maziwa ni rahisi kuharibika kuliko kitu chengine chochote hivyo ni vyema wafugaji hawa wakafikiriwa kuhusiana na suala hilo.

9. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kukaa pamoja na wadau wetu wa biashara akiwemo mfanya biashara mkubwa nchini. Ndugu Said Salim Bakhresa ili waweze kubadilishana mawazo na uzoefu katika kupata mbinu bora za ufugaji na upatikanaji wa soko la maziwa la uhakika.

10. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuvifuatilia vikundi vyote vya wafugaji vilivyokufa kwa lengo la kubaini sababu zilizopelekea hali hiyo na kutafuta ufumbuzi wake.

Kuimarika kwa vikundi hivi kutasaidia sana Serikali yetu kuwapatia vijana wetu wengi ajira na kuacha kutegemea ajira kutoka Serikalini.

**UJENZI WA CHINJIO JIPYA LA KISASA KISAKASAKA**

Kamati ilifanya ziara katiika eneo linalotarajiwa kujengwa chinjio jipya la kisasa huko Kisakasaka. Kamati ilielezwa kuwa eneo lina ukubwa wa hekari 20, ambalo ni kwa ajili ya kujenga chinjio la kuchinjia ngo'mbe na mbuzi. Hadi Kamati inafika katika eneo hilo, ujenzi wa chinjio hilo ulikua bado haujaanza kutokana na changamoto mbalimbali.

**CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MRADI WA UJENZI WA CHINJIO JIPYA LA KISASA - KISAKASAKA**

1. Kamati ilielezwa kuwa katika kufanikisha ujenzi wa chinjio hilo, Wizara ilifanya juhudi za kupeleka mchoro wa eneo hilo kwa wahusika wa ZBA, hata hivyo, mchoro huo haukufanyiwa kazi kwa wakati. Kamati ilielezwa kuwa tokea mwezi Juni 2020, Wizara ya Kilimo iliipelekea mchoro huo ZBA lakini hadi Kamati inafika katika eneo la ujenzi bado mchoro huo ulikua haujafanyiwa kazi jambo linalokwamisha na kupelekea kuchelewa kuanza kwa ujenzi.

2. Kamati iliibaini changamoto ya ukosefu wa hati miliki katika eneo linalotarajiwa kujengwa chinjio hilo ambapo ilielezwa kuwa eneo lipo mikononi mwa Wizara ya Kilimo kwa muda mrefu sasa, lakini jambo la kushangaza ni kwamba hadi Kamati inafika katika eneo hilo kulikoseakana hati miliki inayothibitisha umiliki wa eneo hilo jambo linalopelekea wananchi kupata nafasi ya kulivamia eneo kwa shughuli zao za kijamii.

3. Kamati iliarifiwa kuwa tokea miaka ya 1980 eneo hili lilianza kuvamiwa na wananchi kwa shughuli za kijamii kama vile kujenga nyumba za makaazi. Pamoja na uvamizi huo wananchi wanafanya uharibifu wa miundo mbinu iliyowekwa kwa ajili ya kulihifadhi eneo hili kama vile kukata senyenge zilizowekwa kama uzio.

4. Kamati pia ilielezwa changamoto ya kukosekana kwa mpango kazi wa mradi huu ambapo ni miezi mitano imeshapita tokea bajeti ya mradi huu kupitishwa.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Katika kikao cha Majumuisho ya Wizara ya Kilimo kilichofanyiika tarehe 18/11/2021, Kamati ilihitaji kukutana na wahusika kutoka Wakala wa Majengo (ZBA) ili kupata ufafanuzi kuhusiana na suala zima la ucheleweshaji wa kupitia michoro ya ujenzi wa chinjio hilo. Kamati ilipata maelezo kutoka pande zote mbili na ilipewa taarifa kuwa mchoro umekamilika kufanyiwa mapitio Wizara wanapaswa kuendelea na kazi zinazofuata katika utekelezaji wa ujenzi huo. Kutokana na maelezo yaliyotolewa na pande zote mbili, Kamati ilibaini kuwa kuna tatizo kubwa la mawasiliano katika Wizara zetu. Hivyo, Kamati inachukua nafasi hii kuzishauri taasisi zote za Serikali zinazofanya kazi pamoja kushirikiana katika hatua zote za utekelezaji wa majukumu yao ili malengo yaliyopangwa na Serikali yaweze kukamilika kwa wakati.

2. Kamati inaishauri Wizara kufanya juhudi za kulipatia hati miliki eneo Iote la Kisakasaka ili kuepusha usumbufu wa wananchi wanaovamia eneo hilo.

3. Kamati inaishauri Wizara inapoandaa miradi yake yote ya maendeleo ihakikishe kuwa inaandaa mpango kazi ambao utakua ndio muongozo na ndio utakaoonesha hatua za maendeleo ya ujenzi wa miradi hiyo.

**WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA**

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda inaundwa na Idara na taasisi mbali mbali ambazo kwa pamoja zina lenga kutoa huduma kwa wananchi wote bila ubaguzi wowote.

**IDARA ZA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA**

1. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
2. Idara ya Sera na Utafiti
3. Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko
4. Idara ya Maendeleo ya Viwanda
5. Afisi ya Afsa Mdhamini Pemba.

**TAASISI NA MASHIRIKA YA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA**

1. Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC)
2. Wakala wa Usasjili wa Biashara na Mali
3. Baraza la Taifa la Biashara (ZNBC)
4. Taasisi ya Viwango zanzibar (ZBS)
5. Mamlaka ya Usimamizi wa leseni
6. Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo vidogo, vidogo na vya Kati (SMIDA)
7. Tume ya Ushindani Halali wa Biashara
8. Baraza la Ushindani wa Biashara
9. Wakala wa Vipimo.

Wizara hii katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku inajiendesha kupitia Programu kuu zifuatazo:

i. Programu kuu ya ukuzaji na uendelezaji wa biashara
ii. Programu Kuu ya Uendelezaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Mendeleo ya Viwanda
iii. Programu Kuu ya Viwango na Tathmin na Ubora

**PROGRAMU KUU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA BIASHARA**

Programu hii inaundwa na program ndogo zifuatazo:-

i) Programu ya ukuzaji wa masoko na usafirishaji;

ii) Programu ya ushindani halali wa kibiashara na kumlinda mtumiaji;

iii) Programu ya urahisishaji biashara na ukuzaji biashara za ndani;

iv) Programu ya usimamizi wa usajili wa biashara na mali;

**ZIARA ZA KAMATI KUANGALIA MAENDELEO YA PROGRAMU ZA WIZARA**

Kamati katika kazi zake ilifanya ziara maeneo mbali mbali kwa lengo la kukagua na kujionea hali halisi ya mafanikio na juhudi zinazochukuliwa ambapo Kamati katika Programu hii ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara ilifanya ziara katika maeneo yafuatayo:-

i) Wakala wa Mizani na Vipimo; na

ii) Tume ya Ushindani Halali wa Biashara.

**PROGRAMU NDOGO YA USHINDANI HALALI WA KIBIASHARA NA KUMLINDA MTUMIAJI**

Programu ndogo ya ushidani halali wa kibiashara na kumlinda mtumiaji inasimamiwa na Wakala wa Vipimo Zanzibar na Tume ya Ushindani halali wa kibiashara na kumlinda mtumiaji. Programu hii ina jukumu la kusimamia masuala ya ushindani halali wa biashara baina ya wafanyabiashara na makampuni, kuzuia mienendo ya biashara isiyo ya ushindani pamoja na kudhibiti bidhaa bandia katika soko.

**MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU HII**

Kamati ilipofanya ziara katika Tume ya ushindani halali wa kibiashara ilielezwa mafanikio yafuatayo ambayo yamepatikana tokea kuundwa kwa Tume hii.

1. Kupitia Tume ya Ushindani Halali wa Biashara program ndogo ya ushindani halali wa kibiashara na kumlinda mtumiaji kupitia Idara ya Rasiliamali watu Mipango na Utawala imefanikiwa kulipia gharama za

stationary,mafuta, internet,kufanya pertition ya ofisi ya Unguja na Pemba, ununuzi wa samani kwa ofisi za Unguja na Pemba.

2. Programu pia kupitia Idara ya Miungano ya Kampuni katika Tume ya Ushindani halali wa kibiashara imefanikiwa kukusanya, kupitia, na kuzifanyia uchambuzi taarifa za maombi ya ununuzi wa hisa za kampuni ya Zantel Telecom Public Limited, Kampuni ya Zantel Mobile Financial Services Solution Limited na Kampuni ya Jubilee General Insurance.
3. Tume kupitia Idara yake ya kumlinda mtumiaji imefanikiwa kukagua maduka 527, maghala 24, Supermarket 2, vyote hivyo ni sawa na asilimia 84.
4. Katika ukaguzi wa maduka uliofanywa na Tume, Tume imefanikiwa kukamata bidhaa za vyakula vya makopo, kemikali, na bidhaa za matumizi ya nyumbani ambazo muda wa matumizi yake umeshapita. Bidhaa hizo zina thamani ya Tsh. **784,000.** Miongoni mwa bidhaa zilizokamatwa ni pamoja na blueband, juisi, soda, sabuni ya unga na pampers.
5. Katika eneo la ukaguzi, Tume imefanikiwa kuwakamata wafanyabiashara **20** wakiuza saruji kinyume na bei elekezi iliyotangazwa na Serikali.
6. Pia Tume ilifanikiwa kukagua mikataba ya watoa huduma **46** na kuendelea na hatua nyengine za kiusajili.

**CHANGAMOTO ZA TUME YA USHINDANI HALALI WA KIBIASHARA**

Kamati ilipofanya ziara yake katika Tume ya Ushindani halali wa kibiashara ilibaini changamoto zifuatazo:-

1. Kamati ilibaini changamoto ya ufinyu wa ofisi ambapo ofisi inayotumika kwa sasa ni ndogo na haikidhi mahitaji.
2. Changamoto nyengine iliyoelezwa ni uhaba mkubwa wa wafanyakazi unaoikabili Taasisi hii ambapo ilielezwa kuwa kwa upande wa Pemba kuna wafanyakazi watano (5) tu ambao kiuhalisia hawawezi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

3. Changamoto nyengine iliyoelezwa kwa Kamati ni maslahi duni ya wafanyakazi wa Tume ambapo wafanyakazi hao hukumbwa na misuko suko mikubwa pindi wanapotimiza majukumu yao ya kila siku ikiwemo kushambuliwa na baadhi ya wafanyabiashara wanapokutwa na makosa katika bidhaa zao na baadhi ya bidhaa hizo kutakiwa ziangamizwe. Hali hii ni ya kusikitisha sana na haikubaliki hata kidogo.

4. Changamoto nyengine ni ukosefu wa usafiri katika Tume ya Ushindani halali wa biashara. Kwa sasa hakuna gari na kazi nyingi za Tume hii zinafanyiika nje ya ofisi na kila Idara inahitaji usafiri ambapo kwa sasa zipo Idara tatu ambazo zinahitaji usafiri katika kutekeleza majukumu yake ya ukaguzi wa bidhaa mbali mbali.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kufanya mipango ya kujenga jengo litakalojumuisha ofisi za Wizara nzima ili matatizo ya ukosefu wa nafasi katika Taasisi zetu nyingi katika Wizara hii liweze kuondoka.

2. Kamati inaishauri Serikali kuajiri wafanyakazi wapya wenye utaalamu na vigezo vinavyohitajika ili wafanyakazi hao waweze kutimiza majukumu yao kwa ufanisi pamoja na kuziba pengo kubwa la uhaba wa wafanyakazi liliopo sasa katika ofisi hii.

3. Kamati inaishauri Serikali kuiangalia vyema na kwa umakini miundo ya Taasisi zote za Serikali na iwaongezee maslahi wafanyakazi wake. Kamati inatoa ushauri huu kulingana na kazi kubwa na ngumu wanazozifanya wafanyakazi wetu Serikalini. Aidha, tunaiomba Serikali kwa wale wafanyakazi ambao wana ujuzi adimu Serikali iwaangalie zaidi kwa kuwaongezea maslahi ili waweze kubakia hapa nyumbani na kulijenga taifa letu.

4. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kuipatia Taasisi hii usafiri wa uhakika kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa majukumu yao iliyojipangia hasa tukizingatia kwamba, taasisi hii kazi zake nyingi utekelezaji wake unafanyika nje ya ofisi. Aidha kupitia ripoti hii, tunaiomba Serikali kuliangalia upya suala la kubakisha makusanyo yanayokusanywa na taasisi hii japo kwa asilimia Fulani ili baadhi ya changamoto taasisi iweze kuzitatua yenyewe likiwemo suala la usafiri, endapo fedha

zinazokusanywa na Tume zingelikua zinabakishwa japo kidogo basi Kamati inaamini kuwa suala la changampoto ya usafiri ingetatuliwa japo kwa kununua gari kwa awamu.

5. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuwawekea ulinzi madhubuti wafanyakazi wa Taasisi hii hususani pale wanapofanya ziara ya kukagua katika maduka ya wafanyabiashara ili waweze kufanya kazi zao za ukaguzi kwa usalama na mafanikio.

**WAKALA WA VIPIMO ZANZIBAR**

Kamati ilipofanya ziara katika Wakala wa Vipimo Zanzibar ilielezwa kuwa taasisi hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa vipimo vinakua sahihi na vinatumika kama vinavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo ili biashara hizo ziweze kufanyika kwa usahihi.

**MAFANIKIO YA WAKALA WA VIPIMO KWA UNGUJA NA PEMBA**

Katika utekelezaji wa Programu ndogo ya ushindani halali wa kibiashara na kumlinda mtumiaji kupitia Wakala wa Vipimo, Kamati ilielezwa mafanikio yafuatayo:-

1. Wakala wa Mizani na Vipimo ilifanikiwa kufanya uhakiki wa Mizani 723 sawa na asilimia 88% pamoja na kufanya uhakiki wa matangi ya kuhifadhia mafuta katika vituo mbalimbali vinavyomilikiwa na kampuni ya Gapco Zanzibar Ltd, Zanzibar Petrolium (ZP), na United Petrolium (UP). Jumla ya matangi 39 yalihakikiwa katika kampuni hizo.

2. Wakala wa Mizani na Vipimo ilifanikiwa kuhakiki mita ndogo za kuuzia mafuta (fuel Dispenser) katika vituo vinavyomilikiwa na Kampuni za Gapco Zanzibar Ltd ambapo jumla ya vituo 63 vilihakikiwa sawa na 105%.

3. Uhakiki wa bidhaa zilizofungashwa ulifanikiwa kufanyika katika viwanda vya Looth Group Companies Ltd, Zainab Bottlers na Oryx gas. Jumla ya viwanda vitatu vilihakikiwa sawa na 23% ya matarajio.

4. Wakala ilifanikiwa kufanya uthibitisho wa uwekaji wa alama za Vipimo kwa matangi ya kuhifadhia mafuta katika Bohari ya Kampuni ya Zanzibar

Petrolium na Kampuni ya Gapco Limited ambapo jumla ya matangi matano yalifanyiwa uthibitisho huo wa vipimo.

5. Wakala imefanikiwa kupokea na kuhakiki ujazo wa mafuta yanayoingizwa nchini na Kampuni ya Gapco, United Petrolium, Zanzibar Petrolium na Puma Energy.

**CHANGAMOTO ZA WAKALA WA VIPIMO**

Kwa upande wa Wakala wa Mizani na vipimo Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-

1. Wakala wa Mizani na vipimo ina changamoto ya kupatiwa ruzuku ndogo kutoka Serikalini isiyokidhi mahitaji katika kutekeleza majukumu iliyojipangia.

2. Kamati pia ilielezwa changamoto ya ufinyu wa ofisi kwa Wakala wa Mizani na Vipimo. Kamati ilipofanya ziara katika Wakala hii kwa Unguja na Pemba ilishuhudia sehemu inayotumika kwa matumizi ya ofisi ikiwa ni ndogo sana (vichochoro) ambayo haikidhi mahitaji ya wafanyakazi wa Wakala hii. Sambamba na hilo, Wakala pia inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa wafanyakazi ambapo kwa sasa Wakala ina jumla ya wafanyakazi kumi na saba tu , kumi na mbili kwa upande wa Unguja na watano kwa upande wa Pemba. Uchache huu wa wafanyakazi haukidhi mahitaji ya kazi ziliopo katika taasisi hii hali inayopelekea kuzorota kwa utekelezaji wa majukumu ya kila siku. Uhaba huo wa wafanyakazi unapelekea baadhi ya vipimo kutofanyika kwa bidhaa zinazozalishwa toka nje ya nchi hali inayozua mgogoro kwa wafanya biashara wa ndani kujiona kana kwamba wao wanaonewa.

3. Aidha, kwa upande wa wataalamu wa Vipimo, Wakala pia inakabiliwa na upungufu mkubwa wa wataalamu, Kamati ilielezwa kuwa Zanzibar nzima ina wataalamu wa vipimo watano tu ambapo kwa sasa ni wataalamu wanne ndio waliopo katika taasisi hii jambo ambalo linaipa wasiwasi mkubwa Kamati.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Serikali kuingizia ruzuku ya kutosha katika Taasisi hii ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa wakati kwa maslahi ya wananchi na taifa kwa ujumla.

2. Kama tulivyoshauri katika Tume ya Ushindani Halali wa Biashara kuhusiana na suala zima la maslahi ya wafanyakazi pamoja na jengo la ofisi, Kamati inarudia tena ushauri wake ule ule ilioutoa katika Tume kuwa Serikali kupitia Wizara ya Biashara ifanye maarifa ya kujenga jengo la ofisi pamoja kuiangalia miundo ya wafanyakazi kwa lengo la kuwaongezea maslahi yao. Kamati ilipofanya ziara katika taasisi hii ilisikitishwa sana na eneo linalotumika sasa kama ofisi kwa Wakala wa Mizani na Vipimo ambapo jengo moja wanatumia pamoja ofisi zaidi ya mbili jambo ambalo kwa hadhi ya Wakala ilivyo Kamati inaona haliko sawa.

3. Kamati inaishauri Serikali kuendeleza juhudi zake za kuwaendeleza baadhi ya wafanyakazi pamoja na kuibua vijana wapya, watakaoweza kusomea fani ya vipimo ili hapo baadae watakapomaliza masomo yao waweze kuisaidia taasisi hii muhimu hapa nchini. Aidha, Kamati inasisitiza suala la ajira mpya kwa wafanyakazi katika Wakala wa Mizani na Vipimo kwa vile kuna upungufu mkubwa sana wa wafanyakazi.

4. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuchukua juhudi za makusudi kuweza kuzipima bidhaa zinazozalishwa nje ya nchi, kwa lengo la kuweka uwiano ulio sawa na kuondosha migogoro inayojitokeza siku hadi siku miongoni mwa wafanyabiashara.

5. Pamoja na yote hayo, Kamati inaipongeza Wakala wa Mizani na Vipimo kwa mashirikiano yao ya karibu waliyonayo na Wakala wa Vipimo Tanzania Bara. Kamati inaiomba Wakala iendeleze mashirikiano yao hayo, hasa tukizingatia kuwa Taasisi hii ni mpya na wenzetu ni wakongwe na wana ujuzi wa muda mrefu ili tuweze kufikia malengo tuliyojipangia kwa manufaa ya taifa letu.

6. Kamati inaishauri Taasisi hii kushiriki kikamilifu katika siku ya Wakala wa Vipimo duniani, kwa lengo la kuitumia fursa ya kuitangaza taasisi hii na majukumu yake. Kuitangaza Taasisi hii kutatoa fursa kwa jamii kuielewa vyema na kutoa ushirikiano wa kutosha pale unapohitajika

7. Kamati pia iwajibike kutoa elimu kwa wafanyabiashara na wajasiriamali kwa lengo la kuwawezesha kuingia katika masoko mbalimbali duniani kama vile soko la Afrika ili biashara zetu ziweze kufika mbali na faida ipatikane.

**TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS)**

Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) imeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya Viwango ya Zanzibar Namb. 1 ya mwaka 2011. Taasaisi hii imeanza kazi zake rasmi mwezi Septemba 2012 na iko chini ya usimamizi wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda. Majukumu yake makuu ni kuweka viwango, kusimamia ubora wa bidhaa na huduma nchini.

**MAFANIKIO YA TAASISI YA VIWANGO**

***Ujenzi wa jengo jipya la maabara na ofisi za ZBS***

Kamati ilijionea mafaniko ya taasisi hii ya kujenga jengo jipya na la kisasa linalohusisha maabara nane (8) ikiwa ni pamoja na maabara ya vifaa vya ujenzi ambapo ujenzi huo pia utajumuisha na ofisi za wafanyakazi wa Taasisi hii. Hadi Kamati inafika katika eneo hilo, ilielezwa kuwa ujenzi umefikia 85% na unategemewa kumalizika katika mwezi wa Septemba 2021.

Kamati iliridhika na maendeleo ya ujenzi huo na inatoa pongezi kwa taasisi hii na Serikali kwa ujumla kwa kulizindua jengo hili hivi karibuni katika shamrashamra za sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar.

**CHANGAMOTO ZA TAASISI YA VIWANGO (ZBS)**

Katika ziara hii Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-

1. Kamati ilielezwa changamoto ya ufinyu wa ofisi kwa maeneo yote ya Wete, Chake chake na Mkoani. Kamati ilielezwa kuwa kwa sasa taasisi hii inatumia chumba kimoja katika utekelezaji wake wa majukumu yake yote ya kiofisi.

2. Changamoto nyengine ni upungufu mkubwa wa wafanyakazi ambapo Kamati ilielezwa kuwa, taasisi ina wafanyakazi wanane tu ambao wamejigawa katika ofisi tatu ziliopo Mkoani, Wete na Chakechake kwa upande wa Pemba.

3. Kamati ilielezwa changamoto ya kukosekana kwa wakaguzi wa kutosha katika maeneo ya bandari, masoko, maghala na kukagua wajasiriamali pamoja na maeneo yote yenye viwanda.

4. Changamoto ya ukosefu wa maabara ya uhakika na ugumu wa kupatikana sampuli na majibu ya haraka ni vitu vilivyoishangaza sana Kamati kutokana na umuhimu wake katika shughuli zote zinazotekelezwa na taasisi hii kisiwani Pemba. Aidha, changamoto hii inakwenda sambamba na changamoto ya kukosekana kwa vitendea kazi kama vile kompyuta jambo ambalo limekuwa ni kikwazo kikubwa cha utekelezaji wa majukumu ya wafanyakazi wa taasisi hiyo.

5. Kamati ilielezwa kuwa taasisi kwa upande wa Pemba ina tatizo la kukosekana kwa muundo wa taasisi, jambo ambalo limeishangaza Kamati hasa kwa vile Taasisi ni moja kwa Unguja na Pemba.

6. Changamoto nyengine inayoikabili Taasisi hii ni ufinyu wa bajeti. Kamati imebaini kuwa, kwa upande wa Pemba Taasisi hii haiingiziwi fedha kwa wakati jambo linalopelekea kuchelewa kutekeleza baadhi ya majukumu ambapo Taasisi hulazimika kuomba fedha makao Makuu Unguja ili iweze kutekeleza shughuli zake zote.

7. Ilielezwa kuwa Wajasiriamali wengi wanakiuka masharti ya kupatiwa leseni ya ubora kwa vile wanashindwa kuendelea na uzalishaji mara tu wanapopatiwa alama ya ubora, hali inayorudisha nyuma juhudi za Taasisi hii.

8. Taasisi pia inakabiliwa na changamoto ya wananchi kuwa na uelewa mdogo kwa wajasiriamali juu ya kuitambua miongozo itakayowasaidia katika kuzitambua dalili za ubora wa bidhaa zao pamoja na elimu kubwa inayotolewa na taasisi.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri ZBS kama ilivyofanya juhudi za kujenga jengo zuri la ofisi Ungua ijipange kujenga jengo jipya la ofisi na maabara ksiwani Pemba ili kuondoa tatizo la ufinyu wa ofisi na maabara ya uhakika.

2. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya fedha kuhakikisha kuwa inatoa fedha zilizotengwa katia bajeti kwa wakati kwa taasisi nyeti kama hii,

kwani kukosekana kwa fedha hizo kunasababisha shughuli muhimu kutofanyika kwa wakati.

3. Kamati inazidi kuisistiza Taasisi ya Viwango Zanzibar kujitanga kwa wananchi pamoja na kutoa elimu kuhusiana na umuhimu wa taasisi hii, kufanya hivyo kutasaidia kutambulika kwa taasisi pamoja na kuongeza uelewa wa wananchi ambao wengi wao hawajui umuhimu wa taasisi hii na badala yake baadhi ya wajasiriamali wanakiuka masharti ya kupatiwa leseni ya ubora.

4. Kamati ilipofika ZBS Pemba ilishangazwa na taarifa kuwa hakuna muundo wa taasisi kwa upande wa Pemba. Kamati ilishangazwa na jambo hilo kutokana na ukweli kwamba taasisi hii kwa Unguja na Pemba ni taasisi moja, ni jambo la kushangaza kusikia kuwa Unguja kuna muundo wake na Pemba kuna muundo wake. Hivyo, Kamati ilishauri na inaendelea kushauri kurekebishwa kwa suala hilo ambalo kiutaratibu haliko sawa.

**PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI**

Programu kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali inaundwa na program ndogo mbili ambazo ni:-

i) Programu ndogo ya ukuzaji viwanda; na

ii) Programu ndogo ya Maendeleo ya wajasiriamali.

**ZIARA ZA KAMATI KUANGALIA MAENDELEO**

Katika program hii, Kamati ilifanya ziara sehemu zifuatazo:-

i) Idara ya Maendeleo ya Viwanda;

ii) Wakala wa maendeleo ya viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati (SMIDA)

iii) Kiwanda cha sabuni cha Inaya;

iv) Kiwanda cha unga wa ngano (Zanzibar Milling Corporation);

v) Kiwanda cha nguo (Basra Textile Mills Co. Ltd)

vi) Kiwanda cha kusarifu chumvi;

vii) Kiwanda cha Sukari Mahonda; na

viii) Eneo la Uwekezaji lililopo Chamanangwe.

## PROGRAMU NDOGO YA UKUZAJI VIWANDA

Programu ndogo ya ukuzaji viwanda inasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda ambayo ina jukumu la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Viwanda pamoja na kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya ukuzaji ujasiriamali (MSME Policy).

## MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU HII

Utekelezaji wa program hii umefanikiwa kupitia idara ya Maendeleo ya Viwanda ambapo Kamati ilipofanya ziara katika Idara hiyo ilielezwa mafaniko yafuatayo:-

1. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa program na mikakati ya maendeleo ya viwanda.
2. Kufuatilia ukuaji wa sekta ya viwanda na utendaji wake kwa kubaini vikwazo vinavyoikabili sekta hiyo na kuchukuwa hatua za kuviondoa.
3. Kukusanya taarifa za masuala ya viwanda na kuzisambaza kwa wakati.
4. Kutoa ushauri na elimu ya ujasiriamali kwa wazalishaji wadogo wadogo.
5. Kushajihisha tija katika uzalishaji na utendaji wa miradi ikiwa ni pamoja na

kuhimiza ubora wa bidhaa zinazozalishwa na matumizi ya teknolojia mwafaka.

ikwa ni pamoja na kuboresha vifungashio ***'packaging'*** na njia nyengine za

Uhifadhi wa bidhaa.

## CHANGAMOTO ZA IDARA YA MAENDELEO YA VIWANDA

Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Idara ya Maendleo ya Viwanda na kubaini Chagamoto zifuatazo:-

1. Kamati ilielezwa na kujionea hali halisi ya changamoto ya ufinyu wa nafasi za kufanyia kazi ambapo sehemu za kufanyia kazi ni finyu na mazingira yake hayaridhishi hasa ikizingatiwa unyeti wa Idara hii.
2. Idara inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa baadhi ya wataalamu ambapo wataalamu wanaokesekana ni pamoja na Mwanasheria, Mhasibu na Maafisa wenye fani ya uchumi. Hali hii inailazimu ofisi kuazima

wafanyakazi hawa kutoka katika taaasisi nyengine jambo linalozorotesha utekelezaji wa shughuli za ofisi kwa wakati na kwa ufanisi.

3. Kamati pia ililezwa changamoto ya ufinyu wa bajeti jambo linalopelekea Idara baadhi ya wakati kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu.
4. Changamoto nyengine ni uvamizi wa maeneo tengefu kwa ajili ya ujenzi wa viwanda. Kamati imeelezwa kwamba kuna baadhi ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kujenga viwanda tayari yameshaanza kuvamiwa na wananchi kwa matumizi yao ya kijamii kama vile ujenzi wa nyumba.

5. Changamoto nyengine ni kuwepo kwa wafanya biashara wengi wasiorasmi ambao hawana leseni wala vibali vya kuwatambulisha juu ya bidhaa wanazozizalisha, hali inayopelekea kuinyima Serikali mapato.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaiomba Serikali kupitia Idara ya Maendeleo ya Viwanda kuwapatia mafunzo ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wa idara hii kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Aidha Kamati inaishauri idara kutafuta wataalamu wa Sheria na kuwatumia ndani ya Idara yao kwa lengo la kurahisisha utoaji wa miongozo katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku.

2. Kamati inaiomba Serikali kupitia Idara ya Maendeleo ya Viwanda kuwa na mashirikiano ya karibu sana na wakuu wa Shehia, Wilaya na Mikoa kwa lengo la kuhakikisha kwamba, maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili kujenga viwanda yanalindwa na kuhifadhiwa muda wote.

3. Kamati inaishauri Serikali kuongeza fedha katika bajeti yake kwa Idara ya Maendeleo ya Viwanda ili iweze kufikia malengo yaliyopangwa kwa wakati.

4. Idara ya Maendeleo ya Viwanda ihakikishe kwamba viwanda vyetu vinazalisha bidhaa zilizo na ubora ili ziweze kushindana na zile zinazotoka nje ya nchi kwa lengo la kuvilinda na kuvinusuru visijepoteza uzalishaji wake.

5. Serikali yetu inatumia fedha nyingi sana katika kugharimia miradi yenye lengo la kuwanufaisha wananchi kama vile ujenzi wa viwanda. Kamati inaiomba Idara ya Maendeleo ya Viwanda kuisimamia miradi hii kwa nguvu zake zote na kuhakikisha kwamba miradi hii inakamilika kwa wakati na inawanufaisha wananchi kama ilivyokusudiwa.

6. Kamati inaishauri Idara ya Maendeleo ya Viwanda kufanya haraka kuwafikia wafanya biashara wote, kuwahakiki na kuwatambua kwa lengo la kurahisisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

7. Idara iwe na ubunifu katika kupanga miradi inayokwenda na wakati kwa lengo la kuleta tija.

8. Kamati imebaini kuwa '***brand'*** yetu ni muhimu, hivyo Idara ya Maendeleo ya Viwanda ijitahidi kuitangaza brand hii kwa jamii, lengo ni kuongeza kipato kwa taifa.

**WAKALA WA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO VIDOGO, VIDOGO NA VYA KATI (SMIDA)**

Wakala wa Maendeleo ya Viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati (The Zanzibar micro small and Medium Industrial development Agency) ni chombo kilichoanzishwa kwa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi ( Sheria No . 2 ya mwaka 2018) kama taasisi inayojitegemea kiuwezeshaji chini ya mwamvuli wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda.

**CHANGAMOTO ZA WAKALA WA VIWANDA VIDOGOVIDOGO, VIDOGO NA VYA KATI**

1. Kamati ilielezwa changamoto ya kutoingizwa kwa wakati fedha za bajeti iliyoapangwa hasa katika miradi mbali mbali ya Wakala hii, jambo linalopelekea kutofanyika kwa shughuli nyingi za kimaendeleo kwa wakati.
2. Kamati ilibaini changamoto ya baadhi ya vituo vya uratibu wa mafunzo kwa wajasiriamali kufanya kazi zaidi ya moja jambo ambalo Kamati inaona si sahihi hasa kutokana na unyeti wa mafunzo hayo kwa wajasiriamali wetu.
3. Kamati ilipofanya ziara katika eneo la ujenzi unaoendelea wa ofisi za Wakala wa Maendeleo ya Viwanda (mzunguko wa kwanza wa kazi za Kamati), ilielezwa changamoto ya kukosekana kwa mchanga mzuri na

wa uhakika pamoja na changamoto ya kutolipwa mkandarasi fedha zake za ujenzi kwa hatua ya mwanzo.

4. Changamoto ya kukosekana kwa maeneo yenye kukidhi viwango kwa lengo la kuwapatia wajasiriamali wasiokuwa na maeneo ya uzalishaji ilielezwa kwa Kamati, hali hii imepelekea baadhi ya wajasiriamali kukosa mbinu mbadala zitakazowawezesha kukabiliana na ushindani wa kibisahara uliopo hivi sasa pamoja na kushindwa kuzalisha bidhaa bora na za kisasa.
5. Kamati imesikitishwa na taarifa iliyotolewa na Wakala kwamba kuna upungufu mkubwa wa baadhi ya wafanyakazi wakiwemo wa Idara ya Teknolojia pamoja na Karakana ya viwanda. Aidha, Kamati ilielezwa kwamba Wakala kisiwani Pemba ina wafanyakazi wawili tu.
6. Kamati ilielezwa changamoto ya baadhi ya wajasiriamali kuchelewa kurejesha mikopo kwa wakati, hali inayowanyima fursa wajasiriamali wengine kukopeshwa fedha hizo kwa ajili ya kufanya shughuli zao, Kamati ilielezwa kuwa hadi sasa fedha iliyorudishwa ni chache mno.

Kamati pia ilifanya ziara katika baadhi ya Viwanda kwa lengo la kujionea mafanikio pamoja na changamoto zilizopo kwa sasa. Viwanda vilivyotembelewa ni pamoja na Kiwanda cha Sabuni cha Inaya, Zanzibar Milling Coporation Ltd pamoja na Basra Textile Mills Co. Ltd.

Katika ziara hiyo, Kamati imefurahishwa sana na utendaji kazi wa viwanda hivyo na inapenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wawekezaji wa viwanda vyote hivyo kwa uamuzi wao wa kuwekeza katika nchi yetu na kupelekea kupatikana kwa ajira kwa baadhi ya vijana wetu, naomba Wizara mtufikishie salam zetu hizi na tunawaahidi kufanya nao kazi bega kwa bega kwa lengo la kuhakikisha tunafanikisha maendeleo ya Taifa letu. Hata hivyo, Kamati ilielezwa na kubaini yafuatayo:-

**KIWANDA CHA SABUNI CHA INAYA**

**CHANGAMOTO**

1. Kamati ilielezwa changamoto ya kukosekana kwa baadhi ya malighafi muhimu sana zinazotumika katika utengenezaji wa sabuni hapa Zanzibar, jambo linalopelekea mwekezaji wa kiwanda hiki kuamua kuagiza malighafi hizo nje ya nchi. Aidha, mwekezaji aliieleza Kamati kuwa baadhi

ya malighafi zinapatikana hapa nchini lakini zina gharama kubwa ukilinganisha na nchi nyengine jambo linalomlazimu kuchukua malighafi hizo nje. Mfano mzuri aliouleza mwekezaji huyu ni upatikanaji wa mafuta ya nazi ambapo alieleza kuwa mafuta hayo akinunua nchini Mozambique huyanunua kwa dola 4 wakati hapa kwetu anapata kwa dola 17.

2. Pia mwekezaji aliieleza Kamati kuwa anatumia asumini katika kuzalisha bidhaa zake lakini Kamati ilishangazwa na maelezo yake kuwa asumini hizo anazitoa nchini Egypt wakati hapa kwetu miasumini ipo mingi sana, Kamati inaomba kuuliza jee hapa kwetu hakuna asumini za kutosha za kuweza kumuuzia mwekezaji huyo? Kwanini Wizara mpaka leo hii kupitia Idara zake husika hazijihusishi na utafiti wa mahitaji kama hayo kwa wawekezaji wetu?
3. Muwekezaji wa kiwanda hiki bado anakabiliwa na changamoto ya kulipia tozo ya '***import levy'*** ambapo kwa sasa hakutakiwa kulipa tozo hii.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kupitia ripoti hii Kamati inaiomba Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kupitia Shirika la ZSTC kuliangalia suala la upatikanaji wa malighafi ya mafuta ya nazi nchini na endapo kukiwa na uhakika wa kupatikana kwa mafuta haya hapa nchini kwetu basi ni vyema tukafanye nae mazungumzo mwekezaji huyo na kumuuzia mafuta hayo ili kumuondolea usumbufu anaoupata hivi sasa.
2. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuanzisha kilimo cha miasumini hapa visiwani mwetu kwa lengo la kukitangaza kilimo hiki kuwa ni kilimo cha biashara.
3. Kamati inaishauri Serikali kumuondolea muwekeazji huyu tozo ya '***import levy'*** ikiwa sheria zetu zinaruhusu kufanya hivyo kwa lengo kumuinua muwekezaji huyu na kumtia hamasa ya kuweza kuzalisha zaidi.

**KIWANDA CHA UNGA WA NGANO (ZANZIBAR MILLING CORPORATION).**

Zanzibar Milling Coporation ni moja katika viwanda vikongwe vya Mzee said Bakhresa ambapo kiwanda chake hili kilianza mwaka 1980, kwa wakati huo kiwanda kilikuwa kikizalisha unga wa ngano pamoja na unga wa mahindi. Kiwanda kilifanya kazi hiyo hadi mwaka 1995 kilipofungwa na kufunguliwa tena

mwaka 2011 kikiwa sasa kinazalisha unga wa ngano pekee. Kamati ilikitembelea kiwanda kilichopo Mtoni na kubaini mafanikio yafuatayo:-

**MAFANIKIO YA KIWANDA CHA UNGA WA NGANO (ZANZIBAR MILLING CORPORATION).**

1. Kiwanda kimefanikiwa kuajiri wafanyakazi wengi ambao ni wazawa.
2. Kuongezeka kwa uzalishaji wa unga wa ngano hadi kufikia tani 370 za ujazo kwa siku, hivyo kiwanda kimeweza kukidhi mahitaji ya wateja kwa kiwango kizuri sana.
3. Kiwanda kimefanikiwa kuzalisha pumba ***'polland'*** ambayo inakuwa kama '***by product'*** ambapo bidhaa hii husafirishwa nje ya nchi na kampuni kujipatia fedha za kigeni.

**CHANGAMOTO ZA KIWANDA CHA UNGA WA NGANO**

1. Kamati ilipofanya ziara katika kiwanda hiki, ilielezwa changamoto ya meli inayoleta malighafi za kiwanda kukaa sana bila ya kufunga gati nje ya bandari, jambo linalopelekea mwekezaji kuingia hasara ya kulipa fedha nyingi na baadhi ya wakati kiwanda kinashindwa kufanya kazi kutokana na kukosekana kwa malighafi hizo.

2. Pia Kamati ilielezwa changamoto ya baadhi ya wafanyabiashara wa jumla wanaochukua bidhaa hii kiwandani kukataa kushusha bei hata kama unga huo wameupata kwa bei rahisi kiwandani.
3. Katika Kisiwa cha Pemba kuna tatizo la kupanda kwa bei ya bidhaa hii ya unga wa ngano. Kamati imebaini kuwa bei ya unga wa ngano kwa Unguja ni tofauti kabisa na kule kisiwani Pemba hali inayowaongezea ukali wa maisha wananchi wa kisiwa hiki.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Serikali kupitia Taasisi na Idara inayohusika kulifuatilia suala la meli kukaa nje muda mrefu bila ya kufunga gati kwa lengo la kurahisisha uteremshaji wa mizigo na kuondokana na tatizo la ukosefu wa malighafi katika viwanda vyetu.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kutoa elimu kwa wafanyabiashara wote wa unga wa ngano kuuza bidhaa hii kwa mujibu wa bei elekezi iliyotolewa na Serikali.
3. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuharakisha ujenzi wa viwanda kama hivi kisiwani Pemba kwa lengo la kuwapunguzia ukali wa maisha wananchi wanaoishi katika kisiwa hiki.

**KIWANDA CHA NGUO (BASRA TEXTILE MILLS CO. LTD)**

Huu ni Mradi uliosajiliwa Zanzibar na kuanzishwa kupitia Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji (ZIPA) mwaka 2019. Katika hatua zote ulizopita, mradi umekuwa ukipata mashirikiano makubwa kutoka Serikali kuu na taasisi zake mbalimbali, hasa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, jambo ambalo limewezesha kupiga hatua kubwa na za haraka licha ya athari za Maradhi ya Covid 19 yaliyochelewesha kwa muda fulani kuwasili kwa mafundi na vifaa muhimu kutoka China.

Kamati ilifanya ziara katika kiwanda hiki na kujionea hali halisi ya uzalishaji wa bidhaa unavyofanyika.

**CHANGAMOTO ZA KIWANDA CHA NGUO (BASRA TEXTILE MILLS CO.LTD)**

1. Kiwanda kinazalisha bidhaa zake kikitegemea kuingiza sokoni bidhaa hizo baada ya kuthibitishwa na Taasisi ya Viwango ya hapa kwetu Zanzibar, hata hivyo mwekezaji aliieleza Kamati anapata changamoto ya kusafirisha bidhaa zake kwenda Dar es salaam kwa ajili ya kupimwa kimaabara na kuthibitishwa kiwango cha ubora wa bidhaa hizo jambo ambalo ni usumbufu mkubwa kwa mwekezaji huyu. Imeelezwa kuwa ZBS haina uwezo wa kimaabara wa kupima "***Textiles***".

2. Kamati pia ilijionea changamoto ya mazingira magumu na hatarishi ya kazi kwa wafanyakazi wa kiwanda hichi. Aidha, Kamati ilibaini uwepo wa hewa nzito kiwandani hapo, hali inayoweza kuhatarisha afya za wafanyakazi kiwandani hapo.

3. Stahiki za wafanyakazi ni chagamoto ambapo Kamati ilipata fursa ya kuzungumza na wafanyakazi na kubaini kuwa wengi wao wanafanyakazi

hadi muda wa ziada lakini uongozi bado haujaona umuhimu wa kuwapatia stahiki za ziada jambo linaloweza kurudisha nyuma utendaji wa shughuli ndani ya kiwanda hiki muhimu kwa maendeleo ya Zanzibar.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inachukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Biashara na Manedeleo ya Viwanda kwa hatua ilizozichukua mara tu baada ya ziara ya Kamati ambapo changamoto ya kwanza iliyoelezwa ya kukosekana kwa ruhusa ya TBS itayowawezesha kusafirisha bidhaa za kiwanda hiki Tanzania Bara imetatuliwa na kwa taarifa iliyotolewa kwa Kamati ni kwamba tayari ruhusa imeshatolewa na bidhaa za kiwanda hiki sasa zinaingia Tanzania Bara.
2. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kupitia Taasisi yake inayohusika na usimamizi wa viwanda hivi, kuhakikisha kuwa uongozi wa **BASRA TEXTILE MILLS CO. LTD** unaharakisha ufungaji wa viyoyozi ndani ya kiwanda kwa lengo la kupunguza hewa nzito iliyomo ndani na kuwawekea mazingira salama wafanyakazi hao.
3. Kamati inaishauri Serikali kupitia Idara ya kazi kufuatilia kwa karibu sana malipo ya stahiki za wafanyakazi wa kiwanda hiki cha nguo, lengo ni kuwapa hamasa ya kutekeleza majukumu yao muda wote.
4. Kamati inatoa pongezi za pekee kwa wawekezaji wa kiwanda hiki, na inawaomba wasichoke kuwekeza hapa nchini kwetu pamoja na kuendelea kutoa ajira kwa vijana wetu.

**KIWANDA CHA KUSARIFU CHUMVI**

Kamati ilifanya ziara katika kiwanda cha kuzalisha chumvi pamoja na kukutana na wakulima wa zao hili kisiwani Pemba ambapo ilielezwa kuwa, wakulima hao wapo chini ya mwamvuli wa jumuiya yao ijulikanayo kwa jina la **AZASPO** (Association of Zanzibar Salt Processing Organization).

Kwa sasa jumuiya hii inafanya uzalishaji kwa kushirikiana na kampuni ya ***Swahili Coast Salt*** kwa lengo la kuendeleza uzalishaji bora wa chumvi.

Katika ziara hiyo, Kamati ilielezwa changamoto mbali mbali zinazowakabili wazalishaji hao wa chumvi kama ifuatavyo:-

1. Kamati ilielezwa changamoto ya kukosekana kwa mtaji wa kukiendeleza kiwanda hali ambayo inakwamisha maendeleo ya kiwanda hiki.

2. Kamati pia ilifahamishwa changamoto ya kukosekana kwa maabara itakayotumika kupimia kiwango cha madini joto yaliyomo ndani ya chumvi. Kukosekana kwa maabara hiyo kunahatarisha afya za watumiaji wa zao chumvi, ifahamike kwamba matumizi ya chumvi yasiyo sahihi yanamadhara makubwa kwa mtumiaji na ieleweke kuwa chumvi bila ya kuingizwa madini joto huweza kuleta maradhi mengi yakiwemo goita, tezi dume, ufahamu mdogo na hata kupoteza kumbukumbu kwa watumiaji.

3. Changamoto nyengine ambayo Kamati iliibaini katika uzalishaji wa chumvi ni kukosekana kwa maeneo mengi ambayo yangewezesha wakulima wengi zaidi kujihusisha na uzalishaji wa chumvi, changamoto hii inapelekea hao wazalishaji kidogo waliokuwepo kutofikia lengo la kiwango cha uzalishaji kilichowekwa na kampuni ya ***Swahili Coast Salt***. Kamati ilielezwa kuwa uzalishaji wa chumvi bado uko chini ukilinganisha na mahitaji ya kiwanda ambapo kiwanda kinahitaji tani 17,000 wakati wazalishaji wetu wanazalisha tani 6000 tu.

4. Changamoto ya ughali wa madini joto ilielezwa kuwakabili wazalishaji wa chumvi hali inayopelekea wakulima wengi kuuza chumvi bila ya kuingiza madini hayo na kuhatarisha afya za watumiaji.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Manedeleo ya Viwanda kutafuta wafadhili watakaowasadia wazalishaji wa chumvi kutatua changamoto zao ikiwemo changamoto ya kukosa mtaji pamoja na ukosefu wa maabara ya kupimia madini joto.
2. Kamati inawashauri wananchi hasa wale ambao maeneo yao yanaruhusu uzalishaji wa chumvi kujitokeza kwa wingi na kuingia katika kilimo hiki ili lengo la kampuni ya ***Swahili Coast Salt*** la kupata tani 17,000 liweze kutimia. Kamati inatoa ushauri huu ili fursa hizi zisiweze kupotea kwa kuja kuchukuliwa na wageni ambao hawatozingatia sana suala la ajira kwa wananchi wazalendo.

**KIWANDA CHA SUKARI MAHONDA**

Kamati ya Kilimo Biashara na Utalii ilifanya ziara katika kiwanda cha Sukari Mahonda kwa lengo la kujionea mafanikio na changamoto mbali mbali zilizopo ili lengo la kuanzishwa kiwanda hiki liweze kutimia. Kamati kabla ya kukutana na uongozi wa kiwanda hicho, iliamua kufanya kikao na wakulima wa miwa waliopo Mahomnda kwa lengo la kusikia changamoto mbali mbali zinazowakabili wakulima hao katika kilimo hicho cha miwa.

**MKUTANO BAINA YA KAMATI NA WAKULIMA WA MIWA.**

Kamati ilifanya kikao na wakulima wa miwa kutoka katika Shehia mbali mbali za Unguja ambapo wakulima hao waliieleza Kamati changamoto mbali mbali wanazokabiliana nazo katika uzalishaji wa miwa. Wakulima hao walieza changamoto zao kama ifuatavyo:-

1. Ilielezwa kwa Kamati kuwa, wakulima wanakosa umoja ambao unaweza kuwasaidia kuwaunganisha pamoja na kuweza kujadili matatizo yanayowakabili katika shughuli zao.

2. Wakulima waliieleza Kamati kuwa wanafanya shughuli nyingi na zinazotumia muda mwingi na nguvu za ziada lakini malipo wanayolipwa ni madogo ukilinganisha na kazi kubwa wanazozifanya. Aidha, wakulima walilalamika kuwa bei wanayouza miwa kwa muwekezaji ni ndogo sana ukilinganisha na gharama za kilimo pamoja na makato makubwa wanayokatwa mwanzoni na muwekezaji.

3. Wakulima walieleza kuwa uongozi wa kiwanda cha miwa unachelewa kuvuna miwa na kuwatia hasara kubwa wakulima. Kwa mujibu wa maelezo ya wakulima hao, baadhi ya wakati miwa hukaa shambani zaidi ya miaka miwili bila ya kuvunwa jambo ambalo ni hasara kubwa kwao.

4. Wakulima walilalamika kuwa malipo ya bidhaa zao baada ya kuvunwa na kupelekwa kiwandani huchelewa sana, jambo linalowavunja moyo hasa ikizingatiwa kuwa wengi wa wakulima hao ni masikini sana na hutegemea fedha hizo kwa ajili ya kukidhi mahitaji yao ya msingi.

5. Kamati pia ilielezwa kuwa Wizara ya Kilimo Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo haina mashirikiano ya karibu na wakulima. Ilielezwa kuwa wakulima hawana elimu ya kitaalamu juu ya uzalishaji sahihi wa kilimo cha miwa jambo linalowapelekea kutozalisha kitaalamu.

6. Wakulima wa miwa waliieleza Kamati kuwa, wanakabiliwa na changamoto ya kukosa vitendea kazi vya kisasa ambavyo vitawawezesha kuzalisha katika kiwango kikubwa kulingana na matakwa ya sayansi na teknolojia.

7. Wakulima walilalamika kuwa wafugaji huyaathiri sana mashamba ya miwa kutokana na kuiacha mifugo yao katika mashamba ya miwa na kupelekea uharibifu mkubwa.

8. Wakulima wa miwa walieleza kuwa wanakabiliwa na changamoto ya usafiri wa kuwafikisha katika maeneo yao ya kazi. Ilielezwa kuwa wakulima wanakaa mbali na maeneo yao ya kazi na hivyo kukosekana kwa usafiri ni changamoto kubwa sana kwao.

9. Kamati ilelezwa kuwa kumekuwa na uchelewaji wa kusafirisha miwa baada ya kuvunwa kutoka katika mashamba ya wakulima hadi kiwandani jambo ambalo linapelekea kupungua kwa uzito wa tani za miwa na kupelekea hasara kwa wakulima hawa.

**KIWANDA CHA SUKARI MAHONDA**

Baada ya kikao na Wakulima hao, Kamati ilipata fursa ya kukutana na uongozi wa Kiwanda cha Sukari Mahonda na kujionea hali halisi ya uzalishaji wa sukari.

Kamati ilielezwa kuwa mripuko wa maradhi ya corona ulisababisha athari kubwa kwa uzalishaji wa sukari lakini uongozi uliweka mikakati mizuri ambayo iliweza kukisaidia kiwanda katika uzalishaji pamoja na kuwawezesha wafanyakazi kupata maslahi yao kama kawaida.

Kamati ilielezwa changamoto zifuatazo ambazo zinakikabili kiwanda hicho:-

1. Kiwanda kinakabiliwa na changamoto ya uhaba wa maeneo ya kilimo ambapo ilielezwa kuwa maeneo mengi yanalimwa kilimo cha mpunga na mengine yapo wazi bila ya kulimwa kitu chochote.

2. Kamati ilielezwa changamoto ya baadhi ya wakulima wa miwa kutotaka kubadilika kutokana na kuendelea na kilimo walichokizowea ambacho

hakiendani na mabadiliko ya sayansi na teknolojia na matokeo yake ni kushuka kwa uzalishaji wa miwa.

3. Kamati ilielezwa pia changamoto ya bei ndogo ya sukari ukilinganisha na gharama za uzalishaji. Kiwanda kinatumia gharama kubwa katika uzalishaji na uendeshaji wake. Hivyo, wawekezaji wa kiwanda hiki waliiomba Serikali kuifikiria tena bei ya sukari japo kwa kiwango kidogo.

4. Wawekezaji wa kiwanda cha sukari walilalamika kuwa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo haitoi ushirikiano wa kutosha kwa uongozi wa Kiwanda cha Sukari ambapo ilielezwa kuwa Wizara ya Kilimo ndio wanaohusika na maeneo mengi ya kilimo.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

Kamati baada ya kukutana na wadau wote wa zao la sukari kupitia ripoti hii inapenda kuchukua nafasi hii kuomba radhi wakulima wa zao la miwa pamoja na wadau wote kutokana na ahadi iliyoweka ya kurudi tena kufanya kikao na wadau wote pamoja Wizara ya Kilimo, ili baadhi ya changamoto zilizojitokeza ambazo zinazihusisha Wizara za Serikali ziweze kuchukuliwa hatua na zile zinazokihusu kiwanda cha sukari na wakulima ziweze kupatiwa ufumbuzi kwa pande zote mbili kufaya kazi kwa maridhiano.

Baada ya maelezo hayo Kamati inapenda kutoa mapendekezo yafuatayo:-

1. Kamati inawashauri wakulima wa zao la miwa, kuanzisha umoja wao ambao utakua ndio mwamvuli wa kuwasaidia kutatua baadhi ya changamoto zao zikiwemo za usafiri, kushughulikia suala la bei ya miwa kwa kukubaliana na matakwa ya wakulima na kiwanda cha sukari, suala la kuangalia upya gharama za makato makubwa wanayokatwa wakulima mwanzoni na muwekezaji kwa kukubaliana na muwekezaji utaratibu mzuri ambao hautoleta malalamiko kwa pande zote mbili. Kamati inasisitiza umoja huu ujumuishe wakulima wa shehia zote kwa kila shehia kutoa mjumbe angalau mmoja.

2. Kamati inashauri kusimamiwa kwa haki zoezi zima la uvunaji wa miwa ili kuepusha malalamiko kutoka pande zote mbili ambapo wakulima wanalalamikia suala la kuchelewa kuvunwa kwa mazao yao.

3. Kamati inatoa pendekezo kwa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kusimamia vyema na kwa umakini biashara ya miwa inapofanyika kati ya wakulima wa miwa na wamiliki wa kiwanda cha sukari ili biashara inapofanyika fedha za wakulima hao ziweze kupatikana kwa wakati. Kamati inayasema hayo kutokana na ukweli kwamba wakulima wengi wa zao la miwa ni masikini na hali zao ni duni na wanapofanya biashara hii hutegemea kupata fedha zao kwa wakati kwa lengo la kuweza kujihudumia kutatua matatizo yao.

4. Kamati inatoa agizo kwa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kutoa ushirikiano wa kutosha kwa wakulima wa zao la miwa ili wakulima hao waweze kuzalisha kitalaamu. Kukosekana kwa wataalamu wa Wizara ya Kilimo katika kilimo hiki kunapelekea uzalishaji usio na tija na baadhi ya wakati wakulima hao huonekana kama hawataki kubadilika katika kilimo hicho. Kamati inaamini kuwa, ushiriki mzuri wa Wizara ya Kilimo katika zao hili, utaleta mabadiliko chanya yanayokwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika kilimo.

5. Kamati inatoa wito kwa wananchi wote wa Zanzibar, kuwa na uzalendo na kuona umuhimu wa kilimo cha miwa na kilimo chengine chochote kwa kudhibiti mifugo yao kutoingia katika mashamba ya miwa. Aidha tunatoa wito kwa wakulima wa miwa kupitia umoja watakaouunda, kuweka ulinzi madhubuti ambao utayalinda maeneo yao pamoja na kuchukua hatua stahiki kwa mwananchi yoyote atakayeruhusu mifugo yake kuingia katika mashamba hayo.

6. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuangalia uwezekenao wa baadhi ya maeneo ya kilimo yaliyo wazi kama yapo na kuyakabidhi kwa wamiliki wa kiwanda cha sukari ili maeneo hayo yaweze kutumika katika kilimo hicho. Aidha, Kamati inatoa agizo kwa Wizara ya Kilimo kutoa ushirikiano wa kutosha kwa wawekezaji wa kiwanda cha miwa ili changamoto ndogo ndogo zinazoweza kutatulika ziweze kupatiwa ufumbuzi ili tusiweze kumpoteza muwekezaji huyu ambae anatusaidia kutatua baadhi ya changamoto zikiwemo za ajira pamoja na kuondosha tatizo la upatikanaji wa sukari.

**ENEO LA UWEKEZAJI CHAMANANGWE**

Kamati ilifanya ziara katika eneo maalum la uwekezaji kisiwani Pemba lililopo Chamanangwe ambalo lina ukubwa wa hekta 55.5. Kamati ilielezwa kuwa katika eneo hilo Serikali katika mipango yake, inategemea kujenga ***"Industrial Park"*** jambo ambalo litasaidia sana kuwavuta wawekezaji kwa kufika katika maeneo hayo na kuweka miundombinu yao tu kwa vile maeneo tayari yatakua yameshajengwa.

Katika eneo hilo, Kamati ilijionea uwekezaji uliokwishaanza kwa sasa ambapo Kampuni ya **AMOS INDUSTRY COMPANY LIMITED** imejenga kiwanda cha kuzalisha maji ya kunywa yatakayoitwa **"LULU".** Kamati inachukua nafasi hii kuipongeza Serikali na Wizara kwa ujumla, kwa juhudi ilizochukua hadi mwekezaji yule akafanikiwa kujenga kiwanda ambacho kitakua ni chachu ya maendeleo hasa kisiwani Pemba.

Kamati inaamini kuwa uwekezaji ule, utasaidia sana kupunguza tatizo sugu liliopo hivi sasa la ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana wetu.

**CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KATIKA ENEO MAALUM LA UWEKEZAJI CHAMANANGWE**

1. Kamati ilielezwa kuwa changamoto kubwa iliyopo katika eneo hilo ni baadhi ya wananchi ambao wanamiliki maeneo yaliyomo katika eneo hilo, kugoma kuchukua fedha za fidia kwa ajili ya maeneo yao wengi wao wakihisi kuwa wamekadiriwa fedha kidogo.
2. Upatikanaji mdogo wa fedha za kuanza kujenga maeneo hayo pamoja na mipango ya Serikali ya kutaka kujenga ***"Industrial Park"*** kwa kukopa fedha lakini bado fedha hizo hazijapatikana.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI**

1. Kamati inatoa ushauri kwa Wizara kuweka kumbukumbu zao vizuri kwa wale wote waliokwishachukua fidia za maeneo yao, ili kuepusha migogoro hapo baadae. Aidha, Kamati inatoa wito kwa viongozi wa Majimbo kuwahamasisha wananchi katika maeneo yao kuchukua fidia zao, kwa wale waliokuwa hawajachukua na kuhamasisha uzalendo miongoni mwa wananchi ili uwekezaji uweze kufanikiwa kwa maendeleo ya nchi yetu.

2. Kamati inasisitiza eneo la uwekezaji litakapokamilika na wawekezaji kujitokeza kuwekeza maeneo hayo, suala la ajira lizingatiwe zaidi kwa wazawa wa maeneo hayo, hasa kwa zile kazi ndogo ndogo zisizohitaji utaalamu.

**SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA ZANZIBAR (ZSTC)**

Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) lilianzishwa kwa Legal Notice No.39 ya mwaka 1968. Mnamo mwaka 2011 Serikali ilifanya mapitio ya mfumo mzima wa sekta ya karafuu na muundo wa utekelezaji na majukumu ya Shirika yaliyopelekea kuundwa kwa Sheria ya Shirika la Biashara la Taifa Na.11 ya 2011. Mapitio hayo ya muundo wa Shirika yamepelekea kuundwa kwa mfuko wa Maendeleo ya Karafuu kwa Sheria Nam. 2 mwaka 2014 (Clove Development Act No.2 of 2014).

Kutokana na mwenendo wa Shirika kwa sasa pamoja na umuhimu wa zao la karafuu kwa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa makusudi iliamua kufanya ziara katika Shirika hili kwa Unguja Pemba na tawi la Dar es Salaam kwa lengo la kujionea mwenendo mzima wa biashara na utendaji wa Shirika lenyewe pamoja na kukagua baadhi ya maghala ya kuhifadhia karafuu, mashine za shirika katika kiwanda cha Makonyo Pemba pamoja na kukagua baadhi ya majengo ya shirika ambayo kwa sasa yanatumika kama vitega uchumi vya Shirika hili.

**MAFANIKIO YA SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA**

Kamati ilipofanya ziara katika Shirika la Biashara la Taifa ilielezwa mafanikio yafuatayo:-

1. Katika kipindi cha miaka kumi ya mageuzi (2011/2012 -2020/2021) Shirika la Biashara la Taifa limeweza kutoa bei ya karafuu ya kuridhisha kwa wananchi.

2. Shirika pia katika kipindi hicho cha miaka kumi ya mageuzi limefanikiwa kuanzisha mpango wa biashara jambo ambalo limeliwezesha Shirika kuendelea kutekeleza wajibu wake wa kuuza na kununua karafuu na mazao ya viungo pamoja na hali ngumu ya kiuchumi iliyopo kwa sasa.

3. Shirika pia katika kipindi cha miaka kumi ya mageuzi (2011/2012 - 2020/2021) limefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuchangia katika uchumi wa nchi yetu kutokana na ongezeko la 58.5% ya mauzo ya karafuu ambapo

Shirika limeweza kupata faida ya shilingi Bilioni 512 wakati huko nyuma Shirika lilikuwa likipata shilingi milioni 68 tu. Aidha, katika kipindi cha miezi sita Shirika limefanikiwa kupeleka Serikalini shilingi Bilioni 120 kwa lengo la kusaidia kukuza uchumi wa nchi yetu.

4. Shirika pia limefanikiwa kulipa madeni makubwa ambayo lilikua likidaiwa na taasisi na wadau mbali mbali wa zao la karafuu wakiwemo wateja wa karafuu shilingi bilioni 6.7, ZECO shilingi milioni 708 na Selem Construction shilingi milioni 1.1. Wizara ya Vijana shilingi bilioni 377, 000, 000,00, Madeni ya kiinua mgongo kwa wafanyakazi waliostaafu shilingi Milioni 225.

5. Shirika limeendelea kuimarisha majengo yake ambayo mengine yanatumika kama vitega uchumi na kuingiza mapato ambayo yanalisaidia Shirika hilo katika kutekeleza mambo mbali mbali.

6. Shirika limefanikiwa kuendeleza kuhuisha uhusiano mzuri uliopo baina yake na wadau mbali mbali wa zao la karafuu pamoja na wawekezaji wengine ambao wanavitumia vitega uchumi vya Shirika katika shughuli zao za kibiashara.

**CHANGAMOTO ZA SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA ZANZIBAR (ZSTC)**

1. Kamati ilielezwa kuwa kutokana na kususa sua kwa bei ya karafuu katika soko la dunia, Shirika limekua likikabiliana na changamoto ya kupata hasara baadhi ya misimu ambayo bei ya karafuu dunuani hushuka jambo ambalo hulilazimu Shirika kubeba mzigo mkubwa wa kuwalipa fedha ya ziada wananchi wanaouza karafuu zao.

2. Wakati wa ziara ya Kamati katika mzunguko wa kwanza ilielezwa kuwa Shirika linakabiliwa na changamoto kubwa ya madeni ambapo baadhi ya taasisi za Serikali na binafsi zinalidai Shirika hilo. Kamati ilipatiwa taarifa kuwa Shirika linadaiwa na ZSSF shilingi bilioni 5, PBZ shilingi bilioni 8, wateja wa karafuu shilingi bilioni 6.7, ZECO shilingi milioni 708 na Selem Construction shilingi milioni 1.1. Wizara ya Vijana shilingi milioni 377, 000, 000,00, Madeni ya kiinua mgongo kwa wafanyakazi waliostaafu 225 ambao walikua wakidai takriban shilingi Milioni 225. Hata hivyo, katika kikao cha tarehe **13/02/2022** baina ya Kamati na Shirika ilielezwa kua baadhi ya madeni yameshalipwa ambayo kwa kiasi kikubwa yalikua yakiathiri baadhi ya miradi na kupelekea kusita kwa miradi hiyo ukiwemo ujenzi uliokuwa ukifanywa na kampuni ya Selem Construction kisiwani

Pemba ambao mradi huo ulisita katika hatua ya msingi kutokana na ukosefu wa fedha na deni lililokuwepo awali. Katika kikao hicho, Kamati ilielezwa kuwa kwa sasa Shirika linadaiwa na taasisi mbili tu ambazo ni ZSSF wanaodai shilingi bilioni 5, na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) wanaodai shilingi bilioni 8.

3. Shirika pia linakabiliwa na changamoto ya matumizi makubwa ya umeme unaotumika katika kiwanda cha Makonyo kisiwani Pemba. Aidha, ilielezwa kuwa uchakavu wa mitambo, uchakavu wa kiwanda chenyewe pamoja na upatikanaji wa malighafi kama vile makonyo na majani ya mimea ni changamoto kubwa ambazo zimekuwa zikizidisha hasara kwa Shirika hili.

4. Kamati pia ilielezwa changamoto ya kiwango kikubwa cha Bima ambacho hakilingani na malipo wanayolipwa wakulima wa zao la karafuu wanapopatwa na ajali.

5. Kutochangiwa kwa mfuko wa maendeleo ya karafuu na wadau waliotajwa katika sheria ni changamoto nyengine inayolikabili Shirika hili. Wadau wenyewe ni Shirika la Biashara lenyewe, Serikali na wakulima wa karafuu ambapo hadi sasa wanaolipa fedha hizo ni Shirika la Biashara tu. Hali hii inalirudisha nyuma sana shirika letu katika kufikia malengo yake.

6. Katika ziara ya Kamati tawi la shirika liliopo jijini Dar es salaam, Kamati ilielezwa changamoto ya kodi ndogo ya nyumba ya shirika iliyopo maeneo ya Sinza ambapo wapangaji wa nyumba hiyo wanalipa kodi ndogo kwa mwezi. Kamati ilipatiwa taarifa kuwa nyumba ina wapangaji watatu, mpangaji mmoja aliyepanga vyumba viwili analipa kodi ya shilingi 40,000 kwa kila chumba na mmoja analipa kodi ya shilingi 50,000 kwa chumba kimoja. Aidha tatizo hilo pia lipo kwa upande wa kodi za maduka ya Shirika ambapo maduka yaliyopo katika nyumba ya Sinza ilielezwa kuwa duka moja linakodishwa kwa shilingi 70,000 kwa mwezi kwa mpangaji wa zamani na jengine ambalo mpangaji wake amejitokeza karibuni anakodishwa kwa shilingi 100,000. Kodi hii ni ndogo hasa tukizingatia na unyeti wa eneo hilo ambalo uasili wake ni eneo la biashara.

7. Changamoto nyengine ni uchakavu wa nyumba ambao unatokana na ukongwe wa nyumba yenyewe. Ilielezwa kuwa nyumba hii ilijengwa

tokea miaka ya 80 ambapo kutokana na ukongwe huo nyumba ilianza kujaa maji na kupelekea wapangaji kuihama. Hata hivyo, juhudi mbali mbali zilichukuliwa za kuifanyia matengenezo ya dharura ili iweze kukalika.

8. Kamati ilifika katika maeneo yanayotumiwa na Shirika kwa matumizi ya ofisi na kujionea changamoto ya ufinyu wa eneo hilo linalotumika kwa shughuli za kiofisi. Kamati ilishuhudia sehemu inayotumika kama ofisi kwa Shirika ni ndogo na hairidhishi kwa mazingira ya kiofisi.

9. Changamoto nyengine iliyoelezwa ni gharama kubwa ya kodi ya jengo linalotumika kwa matumizi ya ofisi ambapo ilielezwa kuwa Tawi hili linalipa kodi ya takriban shilingi **2,653,938,000/=** kwa mwezi fedha ambazo ni kubwa mno ukilinganisha na ukubwa wa eneo hilo.

10. Kamati ilielezwa changamoto ya kutopewa nafasi wataalamu wa Shirika kuliendesha Shirika kitaalamu.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

**1.** Kutokana na hasara kubwa ambayo Serikali inaipata kupitia Shirika hili, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kutafuta mazao mbadala ambayo yataweza kusaidiana na zao la karafuu kunyanyua uchumi wetu ambao umekua ni tegemezi katika karafuu na utalii. Mkakati huu wa kuanzisha mazao mengine utasaidia pia kukabiliana na madeni makubwa ambayo Shirika inakabiliana nayo na tunaamini kuwa Shirika likipata mbadala wa mazao haya yataweza kusaidiana na zao la karafuu na halitojiendesha kihasara kama ilivyo sasa.Aidha, Kamati inachukua nafasi hii kulipongeza sana Shirika la Biashara la Taifa kwa kuweza kulipa madeni makubwa yaliyokuwepo ambayo madeni hayo yamelipwa katika kipindi kifupi tu. Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii ilifanya ziara yake ya kwanza katika Shirika hili tarehe **06/04/2021** ambapo ilipewa taarifa ya madeni makubwa yaliyokua yanalikabili Shirika hilo. Hata hivyo, katika mkikao cha tarehe**13/02/2022** baina ya Shirika na Kamati ilielezwa kuwa madeni hayo yote yameshalipwa na zimebakia taasisi mbili zinazodai. Hatua hii ni kubwa sana na Kamati inatoa pongezi za dhati kwa uongozi wa Shirika pamoja na watendaji wake wote.

2. Kamati inalishauri Shirika la Biashara la Taifa kutafuta vyanzo vyengine vya umeme ukiwemo umeme wa jua ili kuepusha hasara iliyokuwepo sasa ambapo kama tulivyoeleza kwenye changamoto kuwa Shirika la Umeme (ZECO) pekee linadai shilingi milioni 708 fedha mabzo ni nyingi sana kwa Shirika letu. Tunaamini kuwa kuna vianzio vingi vya umeme ambapo kama vitaweza kuibuliwa na kutumika ipasavyo gharama hii tunayoingia sasa tunaweza kuiepuka. Ni vyema Shirika kwa kushirikiana na Shirika la Umeme (ZECO) likatafuta wataalamu watakaoshauri aina gani ya umeme inafaa katika matumizi ya viwanda vyetu kwa kuzingatia aina ya mashine tulizonazo.

3. Kamati inaishauri Serikali kuliangalia upya suala zima la Bima ambayo Shirika linafanya juhudi kubwa ya kulipa Bima za wananchi wanaoathirika na mikarafuu mapema ili waathirika wote walipwe kwa wakati. Kamati ilielezwa kuwa utaratibu wa kuwalipa waathirika hao kwa sasa hauridhishi ambapo Shirika la Bima Zanzibar limekua likitumia mfumo usioeleweka kuwalipa waathirika hao na kupelekea kulipwa fedha kidogo ukilinganisha na ajali wanazopata pamoja na kiwango cha fedha zinazopelekwa kutoka ZSTC. Kamati inayasema haya kutokana na maelezo yaliyotolewa na Shirika la Biashara lenyewe kuwa kuna kipindi Shirika lililipa mapema bima za waathirika wa zao la karafuu ambapo msimu wa karafuu kwa kipindi hicho ulikuwa ni mkubwa na kupelekea kuongezeka kwa ajali za mikarafuu na waathirika kupindukia idadi iliyokisiwa na Shirika la biashara. Kutokana na hali hiyo na Shirika la Biashara kutotaka kuwacheleweshea malipo wananch,i liliamua kuliomba Shirika la Bima liwape makisio ya malipo ya wahanga ambao hawakuwemo katika malipo ya Bima ili SZTC walipe wenyewe. Kilichotokea ni makisio makubwa ya fedha za malipo ya wahanga hao ambapo waathirika waliolipwa na Shirika la Bima walilipwa fedha kidogo na wale waliotakiwa kulipwa na ZSTC walikadiriwa fedha nyingi ambapo idadi yao ilikua ni ndogo ukilinganisha na ile ambayo ilikuwepo shirika la Bima.

4. Kamati inasisitiza kuwa kwa vile sheria tumezitunga wenyewe na zinatulazimisha kutimiza wajibu basi ni vyema tukatimiza wajibu huo kama tulivyoelekezwa. Kufuatia changamoto ya baadhi ya wadau kutolipa fedha za maendeleo ya mfuko wa karafuu hasa wale wadau waliotajwa

katika sheria hiyo, Kamati inawashauri wadao wote hao waliotajwa kulipa fedha hizo bila kushurutishwa.

5. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuzinunua karafuu zote walizonazo wananchi kwa kipindi cha msimu na hata pale ambapo msimu ukiwa umemalizika.

6. Kamati inalishauri Shirika na Serikali kwa ujumla kuweka mkakati maalum wa kuliendeleza eneo la nyumba ya shirika hili iliyopo Sinza jijini Dar es salaam kwa kujenga kitega uchumi na kutafuta wawekezaji wa kuingia nae ubia kwa lengo la kujenga kitega uchumi hicho. Hatua hii itasaidia sana kupanda kwa kodi ya jengo litakalojengwa na kuongeza mapato ya Shirika hili. Aidha hatua hii pia itasaidia kuondoa kabisa changamoto ya ufinyu wa ofisi inalolikabili Shirika hili kwa tawi la Dar es salaam.

7. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Biashara kuzitangaza bidhaa zinazozalishwa na Shirika kupitia vyombo mbalimbali vya habari, mabango, mitandao ya kijamii kwa lengo la kutafuta soko ndani na nje ya nchi. Aidha, tunashauri kuanzishwa kwa bidhaa zitokanazo na malighafi tulizonazo hapa nchini ili tuweze kutanua wigo wa biashara.

8. Kamati inaishauri serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuwa na ubunifu katika kuandaa miradi itakayokiwezesha kiwanda cha makonyo kuzalisha bidhaa zilizo bora zaidi kwa lengo la kuweza kujitangaza kitaifa na kimataifa. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kufanya utaratibu wa kukifanyia matengezo kiwanda hicho kwa vile tunakitegemea katika uzalishaji wa mafuta na bidhaa mbali mbali muhimu.

9. Kamati inaishauri Serikali kuchukuwa juhudi za makusudi kumfuatilia mjenzi wa mtambo wa kuzalisha mafuta ya makonyo ili kusudi mtambo huu uweze kuzalisha kama ilivyousudiwa. Kuchelewa kuanza kazi kwa mtambo huu ni kucheleweshа uiingiaji wa mapato yatokanayo na bidhaa zetu.

10. Kamati inachukua nafasi hii kuishauri Serikali kutoa nafasi kwa wataalamu wa Shirika hili kuliendesha Shirika hili kitaalamu na kibiashara.

11. Kamati inaishauri Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Umma, kuwaajiri wataalamu katika fani ya utafiti na masoko, wataalamu ambao

wataweza kukipeleka mbele kiwanda chetu na kuweza kufikia malengo yaliyowekwa.

12. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuliruhusu Shirika kununua malighafi toka nje ya nchi kwa lengo la kuviwezesha viwanda vya Shirika kuzalisha kama inavyotarajiwa.

13. Baada ya ziara ya jijini Dar es Salaam na kujionea changamoto mbali mbali zilizopo katika Shirika hili, Kamati inaona kuwa Shirika halijatoa uzito wa kipekee kuliendeleza tawi lile kutokana na Shirika kutotumia nguvu kubwa ya kuliendeleza tawi lake hilo. Aidha, Kamati inaushauri uongozi wa Shirika kukaa na wataalamu wake na kufanya tathmini ili wajue nini kifanyike kwa lengo kuliimarisha pamoja kuanzisha matawi mengine katika maeneo ya kimkakati wa biashara kwa lengo la kutafuta fursa na vyanzo vyengine vya mapato ili kuepuka kutegemea chanzo kimoja cha mapato.

14. Kamati inalisisitiza Shirika kuendana na kasi ya awamu ya nane kwa kubadilisha mfumo mzima wa ukusanyaji wa mapato kwa kutumia njia za kielectroniki ili kuepusha upotevu wa mapato ya Shirika.

**WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE**

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inaundwa na Idara na taasisi mbali mbali ambazo kwa pamoja zina lenga kutoa huduma kwa wananchi wote ndani ya visiwa hivi bila ubaguzi wowote.

**IDARA ZA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE**

1. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
2. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
3. Idara ya Utalii
4. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale
5. Afisi ya Afsa Mdhamini - Pemba.

**TAASISI ZA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE**

1. Kamisheni ya Utalii.

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inatekeleza majukumu yake ya kila siku kupitia Programu kuu tano (5) kama zifuatazo:-

1. Programu ya kuratibu na kusimamia maendeleo ya Utalii;
2. Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya kale na uhifadhi wa Mji Mkongwe;
3. Programu ya Utawala na Uendeshaji;
4. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii;
5. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Kamisheni ya Utalii

**PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE**

Programu hii inajumuisha program ndogo mbili ambazo ni:-

i) Programu ndogo ya Uendelezaji wa Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe;

ii) Programu ndogo ya Uimarishaji wa Kumbukumbu na Nyaraka.

**ZIARA ZA KAMATI KUANGALIA MAENDELEO YA PROGRAMU ZA WIZARA**

Kamati katika kazi zake ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali kwa lengo la kukagua miradi ya maendeleo na maeneo ya kihistoria kwa lengo la kuona maendeleo yake pamoja na tija inayopatikana kupitia maeneo hayo.

Kupitia program hizi Kamati ilifanya ziara katika maeneo yafuatayo:-

i) Beit Al Ajaib;

ii) Makumbusho ya amani na Makumbusho ya viumbe hai;

iii) Eneo la kihistoria la Fukuchani (Ngome ya Wareno)

iv) Eneo la kihistoria Mwinyi Mkuu – Dunga;
v) Eneo la kihistoria la Rasi Mkumbuu;

vi) Eneo la kihistoria la Kasri la Mkamandume liliopo Pujini;

vii) Eneo la kihistoria chwaka Tumbe, Pango la wanakijiji na Pango la Watoro Makangale

viii) Jengo la kihistoria Ngome Kongwe

ix) Eneo la Kihistoria ya Wahindi – Fufuni

x) Maeneo yaliyoibuliwa vivutio vipya vya Utalii yaliyopo Muungoni Unguja (Sehemu iliyoanguka ndege ya jeshi ya vita vya pili vya dunia na Msikiti wa Kale.)

xi) Masjid Rahman na Mas-haf ya ajabu.

**PROGRAMU NDOGO YA UENDELEZAJI WA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE**

Programu hii inatekelezwa na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale ambayo ina jukumu la kuhakikisha kuwa maeneo ya kihistoria na mambo ya kale yanaendelezwa kwa kuhifadhiwa, kulindwa na kutangazwa.

**MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU**

Kamati ilipofanya ziara katika Idara ya Makumbusho na mambo ya kale kupitia maeneo mbali mbali ya kihistoria iliyoyatembelea ilijionea mafanikio yafuatayo katika utekelezaji wa program hii.

2. Kukarabatiwa kwa baadhi ya majengo ya kihistoria likiwemo jengo la kihistoria la Mwinyi Mkuu liliopo Dunga, ukarabati wa Ngome ya Wareno iliyopo katika eneo la kihistoria la Fukuchani, ukarabati wa jengo la kihistoria la Mkamandume liliopo Pujini Pemba pamoja na kuelezwa mipango mkakati ya kuyafanyia ukarabati maeneo kadhaa ya zamani na yaliyoibuliwa hivi karibuni.

3. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale pia imefanikiwa kuibua vivutio vipya vya Utalii kwa Unguja na Pemba.
4. Idara pia imefanikiwa kuongeza ukusanyaji wa mapato kupitia watalii wanaokwenda kutembelea katika maeneo ya kihistoria na maeneo mengine yenye vivutio vya utalii.

**MAKUMBUSHO YA AMANI NA MAKUMBUSHO YA VIUMBE HAI**

Kamati ilifanya ziara katika Makumbusho ya Amani na Makumbusho ya Viumbe Hai na kuelezwa kuwa sehemu hiyo hapo awali ilikua ikitumika kwa kufanyia maonyesho ya historia ya Zanzibar pamoja na kuhifadhia wanyama aina mbali mbali ambao kwa sasa wametoweka ila juhudi zinafanyika za kukarabati eneo hilo na kurudisha wanyama na vitu vyote vilivyokuwepo hapo awali.

**CHANGAMOTO ZA MAKUMBUSHO YA AMANI NA MAKUMBUSHO YA VIUMBE HAI**

Katika Makumbusho ya Amani na Makumbusho ya Viumbe hai Kamati ilielezwa changamoto zifuatazo:-

1. Kamati ilijionea changamoto ya kubomoka kwa ukuta ingawa changamoto hii ilielezwa kuwa ilisababishwa na ukarabati wa barabara uliokua ukifanyika katika eneo hilo.
2. Pia Kamati ilibaini changamoto ya malipo yanayotozwa kwa wageni kutofautiana. Kubadilika kwa kiwango cha dola '***exchange rate***' inayotozwa kwa wageni ni tofauti na ile iliyopo sasa katika mfumo, pia hakuna uwiano ***'uniformity'*** katika utozaji wa malipo hayo, baadhi ya wageni wanalipa kwa dola na wengine wanalipa kwa fedha ya Tanzania.
3. Katika Makubusho ya Amani, Kamati imebaini uwepo wa jahazi ambayo imewekwa kwa muda mrefu ambapo Kamati ilipofika katika eneo hilo ilielezwa kuwa ni takriban ni miaka miwili jahazi hilo lipo bila ya matumizi yoyote hali inayochafua mazingira halisi ya makumbusho hii.
4. Aidha, Kamati ilibaini uwepo wa mlango wa Zanzibar (Zanzibar Door) uliopo katika sehemu ya maonesho, mlango ambao hauko katika hali nzuri ya kuwakilisha uhalisia wake kwa wageni wanaoingia katika makumbusho hayo.

5. Kamati pia ilibaini uchakavu wa majengo ya Makumbusho yote mawili ambapo katika Makumbusho ya Amani Kamati ilielezwa kuwa jengo hilo kipindi cha mvua linavuja sana. Pamoja na maelezo yaliyotolewa na Wizara kuwa majengo hayo yapo katika mpango wa kuyakarabati, Kamati haikuridhika na hali ya jengo hilo.

6. Eneo la Makumbusho ya Amani lilibainika kuwa na uchafu mwingi jambo ambalo halileti picha nzuri hasa kwa vile wageni mbali mbali wanaingia katika eneo hilo kujionea historia iliyopo hapo.

7. Aidha Kamati ilielezwa changamoto ya kupotea na kuibiwa kwa baadhi ya wanyama waliokua wakipatikana katika makumbusho ya Viumbe Hai, jambo ambalo limeiondoa haiba na dhumuni halisi la Makumbusho hayo.

8. Kamati iliarifiwa kuwa katika Makubusho ya Viumbe Hai kuna uchache wa wataalamu hali inayopelekea kuzorota kwa utekelezaji wa miradi iliyopangwa kama mradi wa kujenga mabanda ya kuhifadhia makobe.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati ilishauri ukuta uliobomolewa kwa ukarabati wa barabara ujengwe wote na kwa sasa ukuta huo tayari umeshajengwa, Kamati inaipongeza hatua hiyo kutokana na eneo lile kua ni miongoni mwa majengo yanayotoa sura halisi ya mji wetu.

2. Kamati inaiomba Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuachana na utaratibu wa kupokea malipo kwa njia ya risiti za mkono na badala yake malipo yafaywe kwa kutumia mfumo wa kielektroniki, kufanya hivyo ni kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais la kukusanya mapato kwa njia ya kielektroniki na hii itasaidia sana kuzuia upotevu wa mapato ndani ya taasisi zetu. Aidha, utaratibu wa malipo ufanywe kwa kuwiana ***'uniformity'*** ili wanaolipa kodi walipe sawa sawa kwa mujibu wa kiwango kitakachowekwa.

3. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuandaa utarartibu wa kuiondosha jahazi iliyopo pembezoni mwa Mkumbusho ya Baitul-Amin kwa lengo la kurejesha haiba na taswira nzuri iliyopo katika makumbusho hayo.

4. Mlango wa Zanzibar door uliopo katika sehemu ya maonesho ufanyiwe ukarabati ili wageni watakapokuja waukute katika uhalisia wake.

5. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuchukuwa hatua za haraka kulifanyia matengenezo makubwa jengo la Makumbusho ya Amani kutokana na uchakavu mkubwa wa jengo hilo, hali inanyohatarisha usalama wa wafanyakazi na wageni wanaotembelea Makumbusho hii hasa kwa kipindi cha mvua kwa vile sekta ya Utalii ndio roho ya Serikali hii. Wageni wanapoingia katika makumbusho hii basi ni vyema wayakute mazingira mazuri na salama muda wote lakini hata wafanyakazi wetu tuwaimarishie mazingira bora na mazuri kwa lengo la kuwamotisha waipende kazi yao.

6. Kamati inazidi kuzisistiza taasisi zinazohusika na masuala ya usafi katika mji wetu kusafisha maeneo yote kwa bidii kutokana na umuhimu wa maeneo hayo hasa ikizingatiwa kuwa maeneo ya Makumbusho haya yanatembelewa na watu wengi wakiwemo wageni na ni vyanzo vya mapato. Haiba ya mji wetu inatokana na usafi wetu, hivyo ni vyema tukazidisha juhudi katika hili kwa kukumbuka kuwa usafi ni afya na kwa kuangalia pia msisitizo wa Mheshimiwa Rais katika suala zima la usafi.

7. Pamoja na maelezo yaliyotolewa na Wizara, Kamati inazidi kusisitiza kurekebishwa na kurudishwa wanyama wote waliokuwepo katika Makumbusho ya Viumbe hai, lengo ni kutimiza matakwa ya kuanzishwa kwa makumbusho hii kinyume chake ni kuivunjia hadhi makumbusho hii.

**ENEO LA KIHISTORIA LA FUKUCHANI (NGOME YA WARENO)**

Eneo la kihistoria la Fukuchani ni eneo alilokuwa akiishi Mtawala wa Kireno katika zama za utawala wake tokea karne ya 16. Jengo hili kwa sasa limefanyiwa matengenezo makubwa kwa kujengwa sehemu ya mapokezi na sehemu ya maliwatoni na kuboresha kuta zilizozunguka eneo hili pamoja na kutiwa milango ndani ya nyumba aliyokuwa akiishi Mtawala huyu.

Eneo hili la kihistoria limezungukwa na makaburi waliyozikwa watu waliokuwa wakiishi katika zama hizo akiwemo mtawala wa wenyeji aliyejulikana kwa jina la Banja Faraja.

Kamati ilipolitembelea eneo hili iligundua changamoto zifuatazo:-

## CHANGAMOTO ZA ENEO LA KIHISTORIA FUKUCHANI

Katika ziara hiyo Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-

1. Mazingira magumu kwa wafanyakazi wa eneo hilo ni miongoni mwa changamoto zlizoelezwa kwa Kamati ambapo sehemu ya mapokezi ya wageni wanayotumia wafanyakazi hao haina AC, madirisha ya eneo la ofisi yako wazi jambo ambalo linaweza kupelekea wadudu hatarishi kuingia ndani ya eneo hilo. Aidha, Kamati ilijionea ufinyu wa chumba kinachotumika kama ofisi kwa wafanyakazi wa eneo hilo.
2. Changamoto nyengine ni maeneo ya vyoo kutokua rafiki kwa watu wenye mahitaji maalum.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inashauri chumba cha mapokezi ambacho kinatumika kama ofisi kwa wafanyakazi wa eneo hilo kiongezewe waya katika madirisha yake ili kunusuru wadudu hatarishi kuingia ndani na kufungwa AC kwa ajili ya kupunguza joto kali hasa kwa siku za kiangazi.
2. Eneo la kihistoria la Fukuchani lijikite zaidi na kutoa huduma za kihistoria kwa kuviboresha vivutio vya utalii vilivyomo ndani ya eneo hilo, lengo ni kuwavutia zaidi watalii ili waweze kuingia kwa wingi na kuiingizia Serikali mapato.

## ENEO LA KIHISTORIA MWINYI MKUU – DUNGA

Kamati ilifafanya ziara katika eneo la Kihistoria la Mwinyi Mkuu liliopo Dunga ambapo ilielezwa historia kuhusiana na eneo hilo. Eneo hilo kwa sasa limefanyiwa ukarabati mkubwa katika maeneo yote ya jengo.

## CHANGAMOTO ZA ENEO LA KIHISTORIA MWINYI MKUU - DUNGA

1. Mkandarasi wa eneo hilo aliieleza Kamati kuwa anakabiliwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha kwa wakati. Ilielezwa kuwa upatikanaji wa fedha haukuwa wa kuridhisha na kupelekea usumbufu mkubwa kwa mkandarasi wa jengo.

2. Kamati pia ilibaini changamoto ya kuwepo kwa mgogoro baina ya wananchi wanaoishi katika maeneo ya jirani ya jengo hilo. Aidha Kamati imegundua kuwa changamoto hii ni ya muda mrefu jambo ambalo limekua ni kikwazo katika kuuendeleza mradi huo.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Serikali kufanya jitihada za makusudi kutoa fedha kwa wakati kwa mujibu wa mkataba walioingia na mkandarasi ili kuepuesha lawama na kucheleweshwa kumalizwa kwa miradi inayojengwa.
2. Kupitia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Kamati inashauri maeneo yote ya kihistoria yalindwe na kuhifadhiwa kwa kuyapatia hati miliki ili kuepusha migogoro na wananchi.
3. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Utalii na mambo ya Kale kuajiri wataalamu wa historia ambao watatumika katika kuielezea historia katika maeneo haya kwa kina pale wageni watakapoingia ndani ya maeneo husika.

**ENEO LA KIHISTORIA LA RASI MKUMBUU.**

Kamati ilifanya ziara katika eneo hili na kuelezwa historia ya eneo hilo ambapo ilielezwa kuwa kulikua na miji ya kihistoria mitatu ambayo ni mji wa karne ya kwanza na mji wa karne ya tano. Ilielezwa kuwa miji hii yote imeshazama na kwa sasa umebakia mji wa karne ya 9 hadi 11.

**CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ENEO LA KIHISTORIA LA RASI MKUMBUU**

1. Kamati ilipofanya ziara katika eneo hili ilibaini ubovu mkubwa wa barabara, Kamati imesikitika sana kutokana na hali ile hasa ukizingatiwa umuhimu wa eneo hilo ambalo linabeba dhima kubwa ya kuhifadhi chanzo kikuu cha umeme wote wa kisiwa cha Pemba.

2. Kamati ilielezwa kuwa eneo hili la Kihistoria linaathiriwa sana na maji ya bahari jambo ambalo litapelekea mji huu uliopo pia kuzama kama miji mengine iliyozama huko nyuma.

3. Pia Kamati imesikitishwa na taarifa kuwa maeneo ya karibu yote ya kihistoria hayana hati miliki likiwemo na eneo hili la Mkumbuu jambo linalowafanya baadhi ya wananchi kuvamia baadhi ya maeneo.

4. Kamati imeskitishwa na taarifa iliyoelezwa kuwa baada ya Benki ya Dunia kuonesha nia ya kulikarabati na kulijenga upya eneo hilo, Serikali imejitoa kabisa katika ukarabati huo jambo ambalo Kamati haikubaliani nalo.

5. Kamati imebaini changamoto ya kutokuwepo kwa maandiko ya kihistoria katika maeneo mengi likiwemo na eneo la Mkumbuu ambapo kwa sasa historia ya eneo hilo inaelezwa kwa mdomo na wahusika wanakaribia kustaafu.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara husika kushirikiana na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuijenga njia yote inayoelekea Mkumbuu kwa kiwango cha lami ili kuongeza kasi ya watalii wanaokwenda kutembelea eneo hilo pamoja na kuweka mazingira mazuri ya vianzio vya umeme vilivyopo katika eneo hilo.

2. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kufanya tafiti zaidi kuhusu mambo yaliyomo ndani ya mji huu na kuchukuwa hatua za haraka za kuuhifadhi mji huu usije kuzama na kutoweka. Aidha Kamati inashauri pia Wizara kujenga ukuta wa mawe ili kuzuia uharibifu wa mawimbi yanayopiga katika maeneo hayo.

3. Kamati inashauri kutafutiwa hati miliki maeneo yote ya kihistoria.

4. Kamati inaishauri Serikali kushirikiana na wafadhili wanaoamua kutusaidia katika kujenga miradi ya maendeleo ya nchi yetu ili tuwape nguvu wafadhili wale waendelee kuwepo na kutusaidia zaidi. Kamati ilishangazwa kusikia kuwa baada ya Benki ya Dunia kuonesha nia ya kutaka kulijenga eneo la Mkumbuu Serikali imejitoa moja kwa moja, jambo hilo si jema na sisi kama Kamati tunasisitiza uwepo wa Serikali katika mradi huo muhimu kwa taifa letu.

5. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa kushirikiana na wadau wote wa historia, wakubaliane utaratibu mzuri wa kuiandika historia ya mji huu na mengineyo yote kwa lengo la kuweka kumbukumbu nzuri vizazi vilivyopo na vijavyo.

**ENEO LA KIHISTORIA LA KASRI LA MKAMANDUME LILIOPO PUJINI**

Eneo la kihistoria la Mkamandume ni miongoni mwa maeneo muhimu ya kihistoria ambalo Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imeanza kulifufua eneo hili kwa kufanya ukarabati wa maeneo yote yaliyomo katika eneo hilo.

Ujenzi wa eneo la Mkamandume ni miongoni mwa miradi inayoendelea tokea bajeti ya 2019/2020 ambapo mradi huu pamoja na kwamba unatekelezwa lakini una mapungufu makubwa ambayo Wizara yenyewe tayari ineshayaona na inayafanyia kazi.

**CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ENEO LA KIHISTORIA LA MKAMANDUME**

1. Kamati ilibaini changamoto ya baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa ukarabati kubomoka wakati maeneo hayo yamekamilika katika ukarabati wake, hata hivyo, Kamati ilirudi kufanya ziara ya kujiridhisha na kuona changamoto hiyo tayari imefanyiwa kazi.

2. Kamati imesikitiishwa sana na kiwango kikubwa cha fedha za ukarabati zilizotumika wakati ilipofika katika eneo hilo kwa mara ya kwanza ambapo thamani ya fedha iliyotumika haikulingana na uhalisia wa matengenezo yaliyofanywa.

3. Kamati katika ziara yake ya mara ya kwanza ilibaini changamoto ya kutokuwepo kwa mkandarasi wa mradi huo katika eneo la kazi kwa zaidi ya mwezi mmoja jambo lililopelekea baadhi ya changamoto kutopatiwa ufumbuzi.

4. Kamati pia ilielezwa changamoto ya kukosekana kwa hati miliki ya eneo ambayo ni changamoto ya muda mrefu jambo linalopelekea baadhi ya wananchi kuvamia eneo hili la kihistoria. Kamati ilielezwa kuwa suala la upatikanaji wa hati miliki limekuwa na changamoto kubwa kwa maeneo mengi ya kihistoria kwa Unguja na Pemba ambapo Wizara ya Ardhi imekuwa ni kikwazo kikubwa katika upatikanaji wa hati miliki hizo kwa maeneo mengi ya kihistoria. Ilielezwa kuwa tokea mwaka 2006 hadi 2007 ni maeneo 14 yaliyopatiwa hati miliki kati ya maeneo **86**. Maeneo hayo yote yapo Unguja na kwa upande wa Pemba hakuna eneo hata moja lililopatiwa hati miliki. Kamati ilisikitishwa sana na taarifa kuwa kuna baadhi ya maeneo yalitolewa fedha na wafadhili kwa lengo la kupimwa na kupatiwa hati miliki lakini kutokana na kucheleweshwa na kuzungushwa kufanywa vipimo hivyo na Wizara ya Ardhi baadhi ya wafadhili hao wamechukua fedha zao.

5. Baada ya ukarabati wa eneo la Mkamandume bado kuna changamoto kubwa ya kukosekana kwa wageni wa kulitembelea eneo hilo ambapo Kamati ilielezwa kuwa, wanaolitembelea eneo hilo kwa wingi hivi sasa ni waganga wa jadi jambo ambalo linakwamisha upatikanaji wa mapato ya kutosha.

6. Kamati pia ilielezwa changamoto ya kukosekana kwa maandiko ya historia ya eneo hili na mengineyo. Imeelezwa kuwa, wataalamu walioihifadhi historia ya eneo la Mkamandume wengi wao wameshastaafu na waliobakia wako ukingoni wanakaribia kustaafu. Aidha, katika eneo hili pia Kamati ilelezwa changamoto ya kukosekana msaidizi wa kutoa maelezo ya kihistoria ambapo kwa sasa yupo mmoja tu ambae anafanya kazi hiyo na siku akidharurika hakutakua na mtu wa kuifanya kazi hiyo.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Baada ya kufanya ziara katika eneo lote la ujenzi Kamati iliiagiza Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuangalia tena mkataba wa ukarabati wa eneo hilo ili kuhakikisha kuwa maeneo yote yaliyobomoka yanakarabatiwa kwa umadhubuti ambao utachukua muda mrefu. Katika ziara ya marudio Kamati ilishuhudia kutekelezwa kwa agizo lake hilo na inachukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa juhudi hizo ilizozichukua.

2. Kamati inachukua nafasi hii kuishauri Wizara na Serikali kwa ujumla kuhakikisha kuwa inapofanya miradi ya maendeleo katika kisiwa cha Pemba inawashirikisha kikamilifu Maafisa Wadhamini wa Wizara husika. Kamati inayasema haya kutokana na maelezo ya awali iliyopatiwa wakati wa utekelezaji wa ukarabati wa mradi huu ambapo katika ukaguzi wa Kamati ilibainika kuwepo kwa changamoto nyingi na Kamati ilipotaka maelezo kutoka kwa Afisa Mdhamini ilielezwa kuwa Afisa Mdhamini hajui chochote kwa sababu hakushirikishwa katika jambo lolote lile linalohusiana na mradi huo, jambo ili halikubaliki.

3. Kamati inaishauri Wizara inapofanya ujenzi wa mradi wowote kuhakikisha kuwa inatafuta wakandarasi makini ambao watakua na uwezo wa kusimamia kazi zao kwa umakini na kufanya kazi kama mkataba unavyoelekeza, ni jambo la kusikitisha sana kusikia kuwa mkandarasi hajaonekana katika eneo lake la kazi kwa zaidi ya mwezi mmoja.

4. Kamati inaishauri Serikali kutoa agizo kwa Wizara inayohusika na utoaji wa hati miliki kutoa hati miliki kwa maeneo yote muhimu ya Serikali ili kuepusha uvamizi unaoendelea kufanywa na baadhi ya wananchi katika maeneo mengi ya kihistoria. Aidha Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kufuatilia mara kwa mara hasa katika maeneo ambayo tayari wamekwisha yaombea hati miliki. Kamati imesikitika sana na taarifa ya kurudishwa fedha kwa lengo la vipimo vya hati miliki fedha ambazo zilitoka kwa wafadhili. Hii ni aibu kubwa kwa Wizara inayohusika na jambo hilo na Kamati inaomba Serikali kuchukua hatua zinaostahiki kwa wahusika wote.

5. Kamati kupitia ripoti hii, inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote kuwahamasisha wananchi wetu Majimboni kujikita katika utalii wa ndani kwa kutembelea katika maeneo yetu ya kihistoria ambayo mengi yao yameimarishwa kwa sasa na yapo vizuri kutembelewa. Aidha, tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe kwa wale wenye nafasi katika maeneo mbali mbali duniani kujitahidi kuvitangaza vivutio vyetu vya utalii kwa lengo la kuongeza idadi ya watalii hapa nchini.

6. Kamati inaeNdelea kuisistiza Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kufanya juhudi za kuiandika historia ya maeneo yote muhimu ya kihistoria ili kuihifadhi vizuri na kuirithisha kwa vizazi vijavyo. Aidha, ni vyema Wizara ikfanya tafiti zaidi ili kugundua athari nyengine ambazo zipo katika eneo hili

7. Kamati inaishauri Wizara kutilia umuhimu miradi inayoanzishwa kwa lengo la kulinda utalii wa ndani na wa nje kwa maslahi ya nchi yetu.

**ENEO LA KIHISTORIA CHWAKA TUMBE, PANGO LA WANAKIJIJI NA PANGO LA WATORO - MAKANGALE**

Kamati ilifanya ziara katika maeneo hayo ya kihistoria na kujionea hifadhi ya maeneo hayo ambayo ni maeneo tegemezi kwa wananchi wanaozunguka maeneo hayo.

Kamati ilipendekeza kuhifadhiwa kwa historia za maeneo hayo ili vizazi vijavyo viweze kunufaika na historia hiyo.

**CHANGAMOTO ZA MAENEO YA KIHISTORIA CHWAKA TUMBE, NA PANGO LA WATORO**

1. Eneo la kihistoria la Chwaka Tumbe limevamiwa na wananchi kwa kujenga nyumba za makaazi, kufuga wanyama na hata shughuli za kilimo hali inayopelekea kuharibifu kwa maeneo ya kihistoria. Aidha, suala la kukosekana kwa walinzi wa kutosha ndani ya maeneo ya kihistoria ni changamoto nyengine ambayo Kamati imeibaini hali inayopelekea kuongezeka kwa uharibifu wa mazingira na uvamizi.

2. Kamati ilielezwa kuwa hadi sasa maeneo mengi ya kihistoria hayajapatiwa hati miliki. Hali hii ni hatari sana kutokana na uhalisia kuwa baadhi ya wananchi waliovamia wanataka kulipwa fidia.

3. Changamoto nyengine ambayo Kamati iliibaini ni kukosekana kwa mabango yanayoonesha maelezo kamili juu ya historia ya maeneo hayo. Mabango haya ni muhimu sana hususani kwa wageni wanaofika ambao lengo kuu la kufika kwao hapo ni kujipatia elimu na historia ambayo itawasaidia katika shughuli zao zikiwemo tafiti mbali mbali wanazozifanya.

4. Changamoto nyengine ambayo ilibainika ni katika utekelezaji wa miradi mingi hasa ya kuimarisha maeneo ya kihistoria ambapo utekelezaji wa uimarishaji huo haufanyiki kama inavyotakiwa na badala yake kinachoimarishwa ni mabaki ya maeneo ya kihistoria.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kulitilia umuhimu suala la hati miliki kwa maeneo yote ya kihistoria kwa lengo la kuepusha migogoro baina ya Wizara na wananchi ambao kwa sasa wanaonekana kuyasogelea maeneo hayo kwa kujihusisha na shughuli za kilimo na ufugaji wa wanyama. Aidha Kamati inaishauri Wizara kuajiri walinzi wa kutosha na kuwaweka katika maeneo ya kihistoria kwa lengo la kuzuia uharibifu unaoendelea kufanywa na wananchi wanaoishi karibu na maeneo hayo pamoja na kujenga uzio.

2. Kamati inaishauri Wizara kuweka mabango katika maeneo yote ya kihistoria yatakayoonesha maelezo mafupi ya historia ya maeneo husika kwa wageni wanaoingia katika maeneo hayo.

3. Kamati inaishauri Wizara inapoamua kutekeleza mradi wowote katika maeneo ya kihistoria, athari ya utekelezaji huo ionekane kwa mujibu wa bajeti yake iliyopangiwa na isiwe kama ilivyo sasa katika miradi mingi Wizara inachokifanya ni kuimarisha mabaki ya maeneo ya kihistoria.
4. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuchukua juhudi za makusudi kuwatunza wasimulizi wa historia waliomo katika maeneo yetu kwa vile uwepo wao ni hazina kwetu.
5. Kiujumla Kamati haijaridhishwa na hatua za maendeleo zilizofikiwa kwa mradi wa Pango la Wanakijiji na Pango la Watoro, hivyo Kamati inaielekeza Wizara kutupatia sababu za msingi zilizopelekea kuzorota kwa ujenzi wa mradi huu.

**JENGO LA KIHISTORIA LA NGOME KONGWE PEMBA**

Kamati ilipofika katika jengo la Ngome Kongwe la kisiwani Pemba ilielezwa kuwa kwa sasa jengo hilo linataka kufanyiwa ukarabati mkubwa kwa kufanyiwa mambo yafuatayo:

- Kuezekwa paa lote;
- Kugonga sehemu yote;
- Kuweka dizaini ya bustani;
- Matengenezo ya vyoo;
- Kuweka dari ya jamvi; na
- Kuweka mabango ya kielektroniki ambayo yataweza kutoa muongozo na kutoa sura ya mji wa kale katika sehemu tofauti za mji wetu.

**CHANGAMOTO ZILIZOPO KATIKA UTEKELEZAJI WA UKARABATI WA JENGO LA NGOME KONGWE PEMBA.**

1. Kamati ilielezwa changamoto ya uchache wa wafanyakazi ambayo inakwamisha utekelezaji wa majukumu yaliyopo katika taasisi hiyo. Hadi kamati inafika eneo hilo, ilielezwa kuwa ni wafanyakazi 22 tu ndio wanaofanyakazi katika Makumbusho hii na wengi wao wanakaribia kustaafu. Aidha, Kamati imebaini kuwa uhaba huu wa wafanyakazi

haulingani na idadi ya maeneo ya kihistoria ambayo kwa sasa tayari yameshafanyiwa utafiti na kutambuliwa rasmi. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa Kamati ni kwamba, maeneo ya kihistoria yaliyopo kisiwani Pemba ni 45. Maeneo haya tayari yametambulika uwepo wake lakini wafanyakazi waliopo ni saba tu na wawili wanatarajia kumaliza utumishi wao hivi karibuni.

2. Idadi ya watalii wanaoingia Kisiwani Pemba bado ni ndogo na hairidhishi. Hali hii inatokana na elimu ndogo waliyonayo wananchi wetu kwa kufanya utalii wa ndani pamoja na uchache wa vivutio kwa wageni kutoka nje.

3. Kamati imebaini changamoto ya Makumbusho ya Ngome Kongwe Pemba kukusanya mapato yake kwa kutumia njia ya risti za mkono hali ambayo haikubaliki kwa sasa.

4. Tatizo la upotevu wa vitabu vya historia ni changamoto nyengine iliyoelezwa ambayo inatokana na wananchi wetu kukosa uaminifu.

5. Kamati pia imebaini tatizo la usafiri kwa wafanyakazi wanaotaka kwenda katika maeneo ya kihistoria ambayo kwa sasa ni mengi na mengine yako mbali hayafikiki kwa urahisi.

6. Wafanyakazi wanafanya kazi katika mazingira magumu kwa kukutana na mambo ya ajabu hasa pale wanapofika katika maeneo ya kihistoria.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuongeza idadi ya wafanyakazi ili wafanyakazi hao waweze kukidhi mahitaji yaliyopo katika taasisi hii. Aidha, Kamati inasisitiza kuwa wafanyakazi watakaopelekwa ni lazima waendane na mzigo mkubwa wa kazi zilizopo kwa kuayaangalia maeneo mapya ya utalii yaliyoibuliwa ili kuepusha kuwachosha na kuwapa mzigo mkubwa zaidi watakaokuwa wanafanya kazi hizo.

2. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuongeza vivutio vya Utalii na kuvifanya kuwa vya kisasa zaidi kwa lengo la kuwavutia wageni toka nje kuweza kuingia kisiwani humo. Aidha, vivutio hivyo vitakapoongezeka Wizara ihakikishe kuwa inavitangaza kupitia vianzio mbali mbali ili watalii na wananchi wote kwa ujumla

waweze kuvijua kiundani na hatimae kuvutika kwenda katika maeneo hayo.

3. Kamati inaishauri Wizara ijipange kwa kuanza kutumia njia ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato yake ili kuzuia upotevu wa fedha za Serikali.

4. Kamati inaishauri Wizara kupitia Makumbusho ya Ngome Kongwe ya kisiwani Pemba kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na historia ya nchi yetu kwa lengo la kuwekeza katika utalii wa ndani na nje ya nchi. Aidha, Kamati inatoa rai ya kuwapa adhabu wale wote watakaokutwa na hatia ya kuiba vitabu vya kihistoria au wale wanaokwenda kuazima na kuvipoteza kwa kuwatoza faini ili iwe ni fundisho kwa kila atakaefanya kosa hilo.

5. Kamati inaishauri Wizara kufanya utaratibu wa kuwapatia usafiri wafanyakazi wa Ngome Kongwe Pemba kwa lengo la kuwarahisishia majukumu yao ili waweze kutekeleza majukumu hayo kwa wakati na kwa ufanisi zaidi. Pia Kamati inashauri wafanyakazi wapatiwe motisha kwa lengo la kuwapa moyo kutokana na madhila makubwa wanayokumbana nayo katika kutekeleza majukumu yao hasa wale wanaokwenda katika baadhi ya maeneo ya kihistoria ambapo ililezwa kuwa baadhi yao hukumbana na mambo ya kishirikina.

6. Kamati inaendelea kuisistiza Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, kujipanga vizuri katika kusimamia ujenzi wa jengo la Ngome Kongwe na majengo mengineyo ili iweze kufikia malengo yalkiyokusudiwa. Aidha Kamati inashauri mkandarasi wa jengo hili asimamiwe ipasavyo ili ujenzi uweze kumalizika kwa wakati uliopangwa.

**NYUMBA YA KIHISTORIA YA WAHINDI FUFUNI**

Kamati ilifika katika eneo la kihistoria la nyumba ya Wahindi iliyopo Fufuni kisiwani Pemba na kuelezwa historia ya eneo hilo pamoja na mikakati ya Wizara ya kulifufua jengo hilo kwa kufanya ukarabati katika baadhi ya maeneo kwa lengo la kufanya uwekezaji ambao utahusisha watalii na wananchi wa kawaida kutembelea katika maeneo hayo ambayo yataiingizia Serikali mapato.

**CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MRADI WA NYUMBA YA KIHISTORIA YA WAHINDI FUFUNI**

1. Kukosekana kwa hati miliki ni miongoni mwa changamoto zilizopo katika eneo hilo jambo linalopelekea baadhi ya wananchi kuingia ndani na kujishughulisha na shughuli za kilimo.
2. Kamati ilishuhudia changamoto ya uchakavu na ubovu wa miundombinu ya barabara jambo ambalo Kamati inaamini kuwa linaweza kukwamisha utekelezaji wa mradi huu.
3. Kamati ilibaini kutokuwepo kwa thamani halisi ya utekelezaji wa mradi huu kutokana na kutokamilika tathmini ya fidia ya wananchi wanaostahili kulipwa.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuharakisha mchakato wa kulipatia hati miliki eneo hili kwa lengo la kuepusha migogoro na uvamizi wa maeneo yaliyobakia.
2. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kushirikiana na Wizara ya Miundombinu kuijenga barabara hiyo ili iweze kufikika kwa urahisi.
3. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kufanya haraka kuweza kutambua thamani ya mradi huu kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wake.

**MAENEO YALIYOIBULIWA VIVUTIO VIPYA VYA UTALII**

Kamati ilfanya ziara katika maeneo yaliyoibuliwa vivutio vipya vya utalii vilivyopo Unguja ikiwa ni pamoja na sehemu iliyoanguka ndege ya Jeshi ya vita vya pili vya dunia na Msikiti wa Kale uliopo Muungoni Unguja.

Vivutio hivi viliweza kuibuliwa kwa mashirikiano baina ya Idara ya Utalii pamoja na Jumuiya ya Maendeleo ya Muungoni iliyopo Mkoa wa kusini Unguja.

**CHANGAMOTO ZILIZOPO KATIKA MAENEO YALIYOIBULIWA VIVUTIO VIPYA VYA UTALII**

1. Katika ziara yake hii Kamati ilibahatika kuona kwa uchache mabaki ya ndege ya vita ya kijeshi ambayo mabaki yake hayapo katika hali ya

kuridhisha kama ni kielelezo cha kihistoria kwa vizazi vijavyo. Kamati ilielezwa kuwa mabaki mengi yameshauzwa vyuma chakavu na yaliyobakia yamo mikononi mwa wananchi wachache.

2. Eneo yaliopo mabaki hayo bado halijahifadhiwa, wananchi wanalitumia eneo hilo kwa shughuli zao mbalimbali za kijamii.
3. Historia ya maeneo haya yote bado haijahifadhiwa katika maandishi. Bado imo ndani ya vichwa vya wazee ambao wanaonekana umri wao tayari umesogea, hali hii itasababisha kuipoteza historia hii.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati baada ya kuona uchache wa mabaki ya ndege ya kivita ya kijeshi haikuridhishwa kuiona hali hiyo imeitaka Wizara ya Utalii kufanya utaratibu mzuri wa kuweza kuyamiliki mabaki hayo ili kuweza kuitunza vizuri historia yetu.
2. Kamati inaishauri Wizara kulihifadhi eneo lote la vivutio vipya vya utalii kwani kufanya hivyo kutaepusha migogoro na wananchi pamoja na kuitunza vyema historia hiyo.
3. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kufanya utaratibu mzuri wa kuyamiliki na kuyahifadhi mabaki ya ndege iliyoanguka katika vita vikuu vya pili vya Dunia ili kuweza kuitunza vizuri historia yetu.
4. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kufanya haraka kuihifdhi historia ya eneo hili hasa ukizingatia wanaoijua historia hiyo ni wachache na ni wazee ambao umri wao tayari umesogea jambo ambalo linaweza kusababisha kuipoteza historia hii.

**MASJID RAHMAN NA MAS-HAF YA AJABU**

Kamati ilifanya ziara katika eneo la Wingwi Mtakuja kwa kutembelea katika eneo la Masjid Rahman ambapo kumehifadhiwa Mas- haf ya ajabu ambayo ina historia kubwa hadi kufikia hatua ya kuhifadhiwa katika mskiti huo. Kamati ilipatiwa historia fupi ya msahafu huo ambao waumini tofauti huutumia kwa maombi pale wanapotanzwa na matatizo mbalimbali katika harakati zao za kila siku za kimaisha.

Katika historia iliyoelezwa mbele ya Kamati, inasemekana kuwa mas-haf hii ina makarama makubwa pamoja na maajabu mengi ambayo wakaazi wa eneo hilo waliyoyashuhudia maajabu hayo wamethibitisha kwa kuieleza Kamati hatua kwa hatua hadi kufikia uamuzi wa kuuhifadhi msahafu huo katika mskiti. Kamati ilielezwa kuwa baadhi ya waumini wa dini ya kiislamu huutumia msahafu huo kwa kufanya maombi kwa Mwenyezi Mungu kupitia kitabu hicho kwa lengo la kutatuliwa shida zao.

**CHANGAMOTO ZILIZOPO KATIKA ENEO HILO**

1. Kamati ilielezwa changamoto ya ufinyu wa eneo la msikiti uliopo kwa sasa ambapo ilielezwa kuwa waumini wa eneo hilo wanafanya ibada zao kwa kujiibana bana. Wakaazi wa eneo hilo kwa kuzingatia umuhimu wa msahafu wa ajabu ambao ni kivutio kikubwa kwa utalii wa ndani na nje ya nchi, wameiomba Kamati na Wizara kwa ujumla kufanya juhudi za makusudi za kutafuta wafadhili wa kuujenga msikiti huo.

2. Changamoto ya miundombinu ni changamoto nyengine iliyoelezwa na waumini wa Masjid Rahman jambo ambalo ni kero kubwa na kwa kuzingatia kivutio cha utalii kilichopo katika eneo hilo.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Wizara kukienzi kivutio hicho cha Utalii kwa kuhakikisha kuwa inatoa mashirikiano makubwa kwa wananchi wa eneo lile pamoja na maelezo ya Wizara kuwa itajitahidi kutafuta wafadhili wa kuujenga mskiti huo na kuweka mipango madhubuti ya kujenga chumba maalum cha kuhifadhia mash-haf ya ajabu ili kuepusha mchanganyiko wa shughuli za utalii na ibada. Kamati inalipongeza sana wazo hilo na inaishauri Wizara mawazo hayo yafanyiwe kazi na yasiishie hewani kwani utalii huo ukikua watakaonufaika ni Serikali pamoja na wananchi wa eneo husika.

2. Baada ya Kamati kupokea changamoto ya wananchi wa eneo la Wingwi Mtakuja inachukua nafasi hii kuishauri Wizara ya Utalii kufanya mazungumzo na Wizara ya Mawasiliano ili njia inayoelekea katika msikiti uliohifadhiwa msahafu wa ajabu iweze kufikika kirahisi angalau kwa kuweka kifusi. Aidha, Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Mawsiliano kuwasaidia wananchi wa eneo lile kwa kuwawekea daraja ambalo liltawasaidia kuvuka katika eneo ambalo linajaa maji katika eneo

la Bonde la Makwararani ambalo wamelilalamikia kujaa maji na kukwamisha shughuli zao za kila siku.

**PROGRAMU KUU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI WA UTALII**

Programu hii imelenga kuongeza uelewa kwa wakaazi wa Tanzania na jamii ya kimataifa kuhusiana na bidhaa na huduma za utalii zilizopo Zanzibar.

Progamu hii inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko yenye jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi.

**KAMISHENI YA UTALII**

Kamisheni ya Utalii imeundwa kwa Sheria namba 9 ya mwaka 1996 ambayo ilifutwa kwa Sheria namba 6 ya mwaka 2009. Kwa sasa Kamisheni ya Utalii inaendeshwa kwa kufuata Sheria No.6 ya mwaka 2009 kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria Na.7 ya mwaka 2012.

**MAFANIKIO YA PROGRAMU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI WA UTALII**

Programu hii imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

1. Programu hii kupitia Kamisheni ya Utalii imefanikiwa kuandaa na kushiriki maonesho, mikutano na makongamano ya Utalii ya kitaifa na kimataifa ili kuvutia wageni kuweza kuvitembelea vivutio vya Utalii vya Zanzibar.

2. Programu hii kupitia Kamisheni ya Utalii imefanikiwa kuwaalika waandishi wa habari za utalii wa kimataifa, wamiliki wa mitandao ya kijamii na watu mashuhuri ili Zanzibar ipate fursa ya kutangazwa kupitia watu hawa kwa gharama nafuu.

3. Programu pia imefanikiwa kuandaa na kutoa matangazo ya utalii katika majarida, televisheni za kitaifa na kimataifa na mabango ya kiektroniki ili kuwavutia watalii wengi zaidi kutoka katika masoko ya asili na mapya.

**CHANGAMOTO ZA KAMISHENI YA UTALII**

1. Kamati ilielezwa kuwa idadi ndogo ya watalii wanaoingia kisiwani Pemba kuwa ni miongoni mwa changamoto kubwa ambapo idadi hiyo inayopelekea kushuka kwa pato la taifa.

2. Changamoto nyengine ni uharibifu wa maeneo ya kihistoria hali inayopelekea kuharibu uasili wa maeneo hayo.

3. Pia Kamati ilielezwa changamoto ya muamko mdogo kwa wazawa kufika katika maeneo ya kihistoria. Kamati imebaini kuwa wazawa wa visiwa hivi vya Zanzibar hawana muamko wa kutembelea katika maeneo ya kihistoria.

4. Changamoto nyengine ni uwepo wa tatizo la ulinzi na usalama kwa watalii. Kamati ilielezwa kwamba, karibu sehemu zote wanazokaa watalii zinalalamikiwa kwa kutokuwa na ulinzi na usalama wa kutosha, hali inayosababisha wageni kusumbuliwa na kukosa utulivu walioutarajia. Watalii wakiwa mapumzikoni huibiwa, huporwa na hata hunyang'anywa baadhi ya vitu vyao vya thamani kama vile fedha, simu na hata kamera.

5. Tatizo la ajira katika sekta ya Utalii ni changamoto kubwa inayowakabili wazawa wa visiwa hivi, hali inayotokana na baadhi ya kasoro zinazojitokeza katika maeneo ya hoteli kama vile ubaguzi katika utoaji wa ajira, ujuzi mdogo wa wazanzibari, maslahi madogo kwa wafanyakazi wetu, kuachishwa kazi na kupewa likizo za lazima bila ya malipo kusikofuata sheria za kazi, kutokuwepo kwa mikataba ya uajiri na kucheleweshwa kwa mishahara.

6. Kutokowepo kwa wafanyakazi wa kutosha wenye elimu na uzoefu unaotakiwa katika sekta ya utalii.

7. Mgongano wa Sheria kwa taasisi ya ZIPA na Kamisheni ya Utalii ni changamoto inayoikabli Kamisheni kwa muda huu. Aidha Kamati imebaini kuwa Sheria ya ugatuzi iliyo chini ya Tawala za Mikoa imekuwa ikisababisha mgongano wa kisheria baina ya Halmashauri za Wilaya na wawekezaji wa sekta ya Utalii.

8. Uhaba wa fedha wa kuendeshea kazi za Kamisheni, hali hii inatokana na ufinyu wa bajeti ambayo inakwamisha utekelezaji wa kazi za Kamisheni.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Serikali kupitia Kamisheni ya Utalii kuharakisha zoezi la kuweka vivutio vya Utalii kisiwani Pemba kwa lengo la kuimarisha utalii na kuongeza kasi ya maendeleo katika kisiwa hiki kama agizo la Mheshimiwa Rais alivyolitoa katika hotuba zake.

2. Kamati inaishauri Serikali kupitia Kamisheni ya Utalii kuimarisha ulinzi katika maeneo yote ya kihistoria kwa lengo la kuyatunza na kuyaimarisha. Aidha, Kamisheni iendelee kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na umuhimu wa maeneo ya kihistoria na faida zake. Kamati inachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa hatua ya kuanzisha kikosi maalum cha Polisi Utalii na Diplomasia kwa lengo la kuweka ulinzi madhubuti katika maeneo yote yenye changamoto kwa watalii. Kamati inaamini kuwa hatua hii itapunguza malalamiko yaliyokua yakitolewa na baadhi ya watalii waliokumbwa na wimbi la ukabaji na uporaji wa mali zao.

3. Kamati inaendelea kusisitiza suala zima la kuendelea kutolewa elimu zaidi kwa wananchi wote wa mjini na vijijini kuhusiana na umuhimu wa maeneo ya utalii jambo ambalo litapelekea muamko kwa jamii na kuwafanya wapende vya nyumbani kwa kutembelea katika maeneo ya utalii.

7. Kamati inaishauri Serikali kupitia Kamisheni ya Utalii kuisimamia vizuri sekta ya Utalii kwa lengo la kuhakikisha sekta hii inaendelea kutoa ajira zaidi kwa wazawa. Aidha, Kamati inawasisitiza vijana wetu kijiendeleza katika fani mbali mbali zikiwemo fani zinazohusika na utalii kwa kutafuta utaalamu zaidi ili waweze kupata ajira katika nafasi za kitaalamu.

8. Kamati inaishauri Serikali inapoamua kuweka sheria katika taasisi yoyote ile iangalie na uwiano wa majukumu ya kazi ya kila idara na ihakikishe kuwa idara hizo haziingiliani kiutekelezaji katika kazi zao. Suala la mgongano wa kisheria liliopo sasa baina ya ZIPA na Kamisheni ya Utalii linaleta changamoto kubwa katika utekelezaji wa majukumu ya kila taasisi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuliangalia hilo kwa kuleta mabadiliko ya sheria, ili kila taasisi iweze kufanya kazi zake kwa uhuru zaidi bila ya kuingiliana. Pamoja na kwamba kwa sasa Serikali imeamua kuzirudisha baadhi ya taasisi zilizogatuliwa katika taasisi zake za awali, bado kuna baadhi ya taasisi zinaingiliana kimajukumu katika hili ambapo Kamati imebaini kuwa Sheria ya ugatuzi iliyo chini ya Tawala za Mikoa imekuwa ikisababisha mgongano wa kisheria baina ya

Halmashauri na Wilaya na wawekezaji wa sekta ya Utalii jambo ambalo ni kero kubwa kwa wadau wa sekta ya utalii, hili nalo tunaishauri Serikali ilirekebishe.

**KITUO CHA UTALII KWA WOTE – BUNGI**

Huu ni mradi ambao unasimamiwa na Kamishemni ya Utalii Zanzibar, Kamati ilielezwa kwamba, mradi huu umegaiwa katika awamu tatu ya utekelezaji ambapo hadi sasa mradi upo katika awamu ya pili.

**CHANGAMOTO ZILIZOPO KATIKA UTEKELEZAJI WA MRADI WA ULATII KWA WOTE**

Kamati ilipofanya ziara katika eneo linalojengwa mradi wa Utalii kwa wote ilielezwa changamoto zifuatazo:-

1. Kamati ilielezwa kuwa awamu ya kwanza ya mradi huu haikutekelezwa kutokana na tatizo la ukosefu wa fedha.
2. Pia Kamati ilibaini changamoto ya uwepo wa tenki ya kuhifadhi maji juu ya paa, jambo linaloondoa haiba nzuri iliyokusudiwa ya ujenzi huu wa kisasa.
3. Kamati ilielezwa changamoto ya uvamizi wa eneo ambapo baadhi ya wananchi wamevamia maeneo ya mradi na kufanya shughuli za ujenzi na kulima jambo ambalo si sahihi hasa kwa vile eneo lote limeshapimwa na mipaka ipo. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa kesi kuhusiana na kadhia hiyo ipo Mahakamani kwa muda wa miaka kumi sasa, lakini cha kushangaza Kamati ilipotaka maelezo kuhusiana na jambo hili ilipewa taarifa kuwa haijulikani kesi hiyo ikoje.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inashauri Serikali inapoamua kutekeleza mradi wowote kuhakikisha kuwa fedha za utekelezaji wa mradi huo zinapatikana kwa wakati ili lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa.
2. Kamati inaishauri Serikali kupitia Kamisheni ya Utalii kulishusha tenki liliopo juu ya paa na kulijengea mnara wake maalumu ili kutoa sura nzuri katika miradi huu.
4. Kamati kupitia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inashauri kuyatunza na kuyaimarisha maeneo yote ya kihistoria kwani ni hazina kubwa kwa taifa

letu. Aidha, Kamati inaiagiza Kamisheni ya Utalii kulifuatilia suala la kesi iliyopo Mahakamani na ijulikane hatma ya kesi hiyo ikoje hadi sasa.

**SEHEMU YA TATU**

**HITIMISHO**

Katika kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Kanuni za Baraza la Wawakilishi na Sheria nyenginezo, Kamati imetoa maelekezo na ushauri wake ambao tunaamini kuwa utasaidia katika kuleta ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu ya Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale. Maelekezo na maoni hayo yalitolewa na Kamati kwa dhamira ya kuwawakilisha vyema wananchi wa Zanzibar na kuona kuwa maslahi ya wananchi hao, kwa mujibu wa sheria yanapewa kipaumbele. Kamati yetu inatumai kuwa maelekezo na maoni yaliyotolewa na Kamati kwa Wizara hizo yatazingatiwa kwa lengo la kutoa huduma zilizotukuka kwa wananchi wa Zanzibar.

Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwanza kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake vizuri, lakini zaidi kwa

ushauri walioupatia Kamati yetu katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu yake.